

**Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA ISHIRINI**

**Kikao cha Kumi na Sita - Tarehe 28 Juni, 2005**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 148

Kufutwa kwa Kodi za Nyumba za Matope

**MHE. STEPHEN M. KAZI** aliuliza:-

Kwa kuwa baada ya Serikali kufuta kodi za majengo/nyumba za matope kwenye maeneo yasiyopimwa Mijini/Vijijini na Jiji la Mwanza likiwemo, ambazo zimetajwa kuwa ni kodi zenye kero kwa jamii:-

- (a) Je, ni halali kwa Halmashauri kutoza kodi kwenye eneo la kiwanja kisichopimwa (*Land Rent*) wakati nyumba iliyojengwa kwenye eneo hilo ni ya tope?
- (b) Kama jibu kwenye sehemu (a) ya swali hili ni ndiyo. Je, kufanya hivyo siyo kupingana na uamuzi wa kufuta aina hiyo ya kodi kwa majengo husika?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sphen Masaba Kazi, Mbunge wa Mwanza Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali za Mitaa zina utaratibu wa kujipatia mapato ya kuendesha shughuli zake ikiwa ni pamoja na kupata ruzuku toka Serikalini na kutoza kodi na ushuru mbalimbali kwa mujibu wa Sheria zilizopo.

Aidha, baadhi ya Sheria zinazotumika ni pamoja na Sheria ya kodi ya majengo ya Mamlaka za Miji Na. 2 ya mwaka 1983 (*The Urban Authorities (Rating) Act No. 2 of 1983*) na pia kwa kutumia Sheria ndogo zinazotungwa na Halmashauri chini ya Sheria ya Fedha za Halmashauri Na. 9 ya 1982. Chini ya Sheria hii na bila kuathiri sheria zingine Mamlaka hizi zinaweza kutoza kodi yoyote inayoweza kuona kuwa ni ya manufaa kwa uendeshaji wa shughuli za Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia misingi hiyo Halmashauri ya Jiji la Mwanza ambayo Mheshimiwa Mbunge ni mjumbe, kupitia kikao maalum cha Kamati ya Mipango Miji cha tarehe 13/3/2001 ilitoa azimio la kutoza kodi ya ardhi kwa kiwango cha sh.2000/= kwa kila nyumba kwenye makazi yaliyojengwa holela ili kuongeza wigo wa mapato ya Serikali. Sensa ya kutambua nyumba zote zilizojengwa kiholela ilifanyika kuanzia mwezi Aprili 2001 hadi tarehe 28 Juni, 2003 ambapo jumla ya nyumba 39,702 ziliainishwa na wahusika wote kupewa namba maalum na kutambuliwa kwa ufasaha.

Aidha utozaji wa kodi ya ardhi katika maeneo hayo ulianza Mei 2005 na jumla ya sh.63,322,000/= zimepatikana kama malipo ya kodi ya ardhi kwa maeneo hayo ambayo mwanzoni yalijengwa kiholela. Kwa kuwashirikisha wananchi wenyewe, hatua za awali za upimaji wa maeneo hayo umeanza kwa maeneo ya Mahango (B) Kata ya Mahina, Mecco Mashariki Kata ya Nyakato na Kata ya Igogo. Lengo kuu ni kuboresha makazi ya wananchi na pia kuhakikisha kodi halali inakusanywa kwa kuzingatia Sheria zilizopo.

(b) Mheshimiwa Spika, utozaji wa kodi ya majengo (*Property Tax*) hufanywa kwa mujibu wa Sheria ya Kodi ya majengo ya Mamlaka za Miji Na. 2 ya mwaka 1983 (*The Urban Authorities (Rating) Act No.2 of 1983*), kama nilivyosema. Kodi ya Ardhi hutozwa kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji Namba 5 ya mwaka 1999 kwa kumilikisha ardhi kisheria katika maeneo yaliyopimwa. Aidha, kwa upande wa ardhi ya Kijiji kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya mwaka 1999 Halmashauri ya Kijiji inayo hiari ya kupanga na kutoza kodi ya pango la ardhi ka wananchi waliopewa hati za kumiliki ardhi kimila.

Kwa mantiki hii kama nilivyoeleza katika sehemu (a) hapo juu msimamo wa Sheria haupingani na uamuzi wa kufuta kodi ya majengo kwa majengo yaliyojengwa kwa tope kwani kodi inayotozwa ni ya ardhi na isitoshe Sheria iliyotumika kutoza kodi hii ni Sheria Na. 9 ya 1982 inayohusu fedha za Serikali za Mitaa.

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Nashukuru sana Mheshimiwa Spika, kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa vile madhumuni ya kufuta kodi ya majengo ilikuwa ni kuondoa kero na kuweza kuwaweka wananchi walio na kipato cha chini waweze kuendesha maisha yao vizuri. Lakini pia isiangelie tofauti na kwamba wananchi pamoja na kutoza kodi hizi wanapaswa wapewe taarifa za kutosha na kupewa elimu kwa

nini kodi hii inatozwa. Sasa nauliza, kwa nini Serikali mpaka sasa tutakuwa tunazunguka kuondoa kodi za kero tunaanzisha nyingine tena?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, tarehe 13 Aprili, nilijibu swali Na.16 la Mheshimiwa Mpesya na lilikuwa linahusiana na jambo hili hili na ufafanuzi tulioutoa ni kwamba hizi nyumba ambazo tunasema ni za tope, si kila nyumba inastahili kupata msamaha huo kama katika utaratibu wa Halmashauri inaonekana kwamba nyumba hiyo inaweza ikawa na thamani ya kiasi fulani kinachotambulika na Halmashauri inayohusika.

Zile nyumba ambazo zinabainika wazi kabisa kwamba hazina thamani kwa maana ya kwamba ni nyumba zilizojengwa na watu ambao uwezo wao ni mdogo kabisa kabisa na zinafahamika wazi. Nyumba hizo ndizo tulisisitiza kwamba kwa kweli zisitozwe ushuru wa namna yoyote kwa sababu walengwa walikuwa ndiyo hao maskini ili kuwapunguzia tatizo.

Lakini nyumba nyingine ambazo pamoja na kwamba zimejengwa kwa tope au tofali mbichi, lakini ina thamani ya kiasi fulani basi tunaweza tukaendeleza zoezi hilo. Na kwa upande wa Mwanza Mheshimiwa Masaba nina hakika kabisa shilingi 2,000/= zilizokubalika na Jiji lako sidhani kama ni fedha nyingi sana kiasi kwamba mtu anaweza akalalamika kuzilipia kwa mwaka mzima. Lakini kama ni kweli ni maskini kiasi hicho bado anaweza akarejesha jambo hilo kwenye Halmashauri yako likazungumzwa na atasamehewa kulingana na taratibu zilizopo.

Na. 149

### **Barabara ya Dar es Salaam – Moshi**

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE** aliuliza:-

Kwa kuwa hapo mwanzo barabara kuu ya Dar es Salaam – Moshi ilikuwa inapita katika kijiji cha Kisangara karibu na reli ya Tanga-Arusha na kwa kuwa barabara hiyo ilipokuwa inawekewa lami ya sasa ilihamishwa na kupita katikati ya kijiji hicho:-

- (a) Je, kwa nini watu wenye nyumba na biashara zao katikati ya eneo la Kisangara wamewekewa alama (X) kuashiria kuvunjwa kwa nyumba kana kwamba wao ndio walioifuata barabara?
- (b) Ili kulinda mali za watu, je kwa nini barabara kuu zinapoingia Mijini/Miji midogo zisitengenezewe barabara za mpito nje ya miji hiyo na zile zinazolingia katikati zikawa barabara za mijini?

- (c) Je, Serikali iko tayari kufidia nyumba na mali za wananchi ambao wanajikuta kwenye *road reserve* baada ya barabara kubadilishwa wakati wa matengenezo mapya?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mbunge wa Mwanga, napenda kutoa maelezo ya jumla kuhusu utaratibu wa ujenzi wa barabara mpya ambayo ujenzi wake utaathiri mali za watu katika ukanda itakamopita.

Mheshimiwa Spika, kila barabara mpya inapotakiwa kujengwa, upembuzi yakinifu hufanywa kwa kina kwa sehemu itakapopita barabara. Upana wote wa hifadhi ya barabara hupimwa na kukaguliwa kwa minajili ya kuhakiki mali zote za wananchi zilizomo ndani ya hifadhi ya barabara na kuzithamini kwa ajili ya kufidiwa ili wahusika wahame na kuuacha wazi ukanda wa hifadhi ya barabara. Hatua hiyo ya awali ikisha kamilika, mtu yeyote atakayejenga ndani ya hifadhi ya barabara atakuwa anakiuka sheria na nyumba au mali yake itakayokutwa ndani ya hifadhi ya barabara itabidi iondolewe bila fidia yoyote.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mbunge wa Mwanga, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, barabara ya Same – Moshi iliyokamilika kujengwa kwa kiwango cha lami kwa mara ya kwanza kati ya mwaka 1963 hadi 1965, iliamishwa kutoka karibu na eneo la reli ya Tanga – Arusha na kupita sehemu iliyopo sasa. Barabara hii wakati inajengwa sehemu ya Kisangara inakopita sasa ilikuwa ni mashamba ya katani tu na hapakuwa na nyumba za wananchi katika eneo hilo ambazo zingeathiriwa na ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami. Barabara hiyo iliwekewa tabaka jipya la lami *rehabilitated* mwaka 1992 na barabara haikuhamishwa kutoka pale ilipokuwepo. Hivyo suala la wananchi kufuatwa na barabara halikuwepo. Ila watu walifuata barabara.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa sehemu ya Kisangara wamewekewa alama ya (X) kwenye nyumba zao zilizopo kwenye hifadhi ya barabara kuashiria kuwa wamekiuka sheria ya hifadhi ya barabara na ni lazima wasogee kwa kiwango kilichowekwa na sheria kwa eneo hilo kwa ajili ya hifadhi ya barabara. Ikumbukwe kwamba wakati wa ujenzi wa barabara hii miaka ya 1963 hadi 1965, hapakuwa na nyumba za wananchi katika eneo hilo. Hivyo hao waliokuja baadaye ni wageni ndani ya hifadhi ya barabara.

(b) Mheshimiwa Spika, barabara zote ziwe za mijini au nje ya miji zina hifadhi ya barabara. Hivyo mwananchi yeyote ambaye atajenga ndani ya hifadhi ya barabara ikiwa mjini au nje ya mji ataathirika endapo hatazingatia vipimo vya hifadhi ya barabara vilivyowekwa na sheria. Suala la kujenga barabara za mpito (*by pass*) halitakuwa ufumbuzi wa kutowavunjia wananchi nyumba na mali zilizomo ndani ya hifadhi ya barabara kwani miji mingi imekuwa baada ya barabara kujengwa na watu kujenga ndani ya hifadhi ya barabara.

Mheshimiwa Spika, uzoefu unaonyesha kuwa mara nyingi barabara inapokamilika kujengwa watu hufuata barabara na kujenga nyumba zao za biashara na za kuishi bila kuzingatia upana wa hifadhi ya barabara uliowekwa kisheria. Mifano hai wa watu kufuata barabara ni Morogoro. Barabara ya kwenda Iringa ilikuwa inapita mjini lakini ikahamishiwa Msamvu ambapo ilikuwa nje ya mji lakini kwa sasa imezungukwa na nyumba. Miji mingine ni Mbeya (*Forest*), Korogwe, Kahama, Sumbawanga (Sumbawanga wenyeji, Misungwi na kadhalika na sasa Nzega inajengwa barabara ya mpito ambapo tayari watu wameshaanza kujenga nyumba za kuishi na za biashara.

La muhimu hapa ni kwa Waheshimiwa Wabunge kuwaelimisha wananchi wao kuwa wanapojenga karibu na barabara wazingatie upana wa hifadhi ya barabara ili wasije wakapata hasara ya kuvunjiwa kwa kutozingatia sheria ya hifadhi ya barabara. Kwa hali hiyo suala la *by pass* siyo ufumbuzi wa tatizo hilo la kulinda mali za watu. Ufumbuzi wa kudumu ni watu kuzingatia sheria na kujenga nje ya hifadhi ya barabara kwa usalama wao na mali zao.

Mheshimiwa Spika, tunawaomba Wabunge wawatumie ma-*Regional Managers* wa *TANROADS* kuwasaidia katika suala hili.

(c) Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye maelezo yangu ya utangulizi, mara zote wakati wa ujenzi wa barabara mpya au ya zamani inapobadilisha mwelekeo (*re-alignment*) mali zote zinazokutwa kwenye hifadhi ya barabara hufanyiwa tathmini na baadaye Serikali hulipa fidia kwa waathirika kabla ya kuanza ujenzi wa barabara husika. Baada ya zoezi hilo kukamilika, yeyote atakayejenga ndani ya hifadhi ya barabara atavunjiwa bila fidia bali yeye mvamizi kisheria atatakiwa kufidia gharama za kuvunjiwa na Serikali.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa jibu lake refu lenye maelezo marefu. Lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika Miji Midogo ya Kisangara, Lembeni na Mwanga barabara kuu inaenda sambamba na reli ya Tanga na kuna majengo mengi katikati ya barabara na reli hiyo na kwamba reli na yenyewe ina *railway reserve* na barabara ina *road reserve* na kwamba kama watatekeleza kuvunja nyumba hizi basi asilimia 20 mpaka 40 ya majengo ya miji hii midogo itaondolewa. Je, Serikali haioni kwamba hali hii ni spesheli na kwamba utaratibu mwinginewa kushughulikia hali hii ufuatwe kwa kuwa hakuna reli au barabara iliyozuiwa na ujenzi ulioko sasa badala ya kuvunja nyumba zao?

Pili, kwa kuwa katika miaka ya vijiji, vijiji vya ujamaa wananchi wengi waliondolewa katika makazi yao walipokuwemo na kuletwa karibu na barabara ili kupata maendeleo. Je, Serikali haioni kwamba ni usumbufu kwa wananchi hawa sasa kuwavunja nyumba wakati waliletwa hapo ili wapate maendeleo? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ile hali ambayo iko kwenye vijiji vya Kisangara, Lembeni na Mwanga ambapo upande mmoja kuna reli na upande mwingine kuna barabara, tumeweka alama za (X) tukiashiria kuwaambia kwamba endapo tutapata pesa za kupanua barabara hii nyinyi mko ndani ya hifadhi ya barabara na huu ndio msimamo wa Serikali. Nyinyi mko ndani ya hifadhi ya barabara. Reli nao wakija kusema na nyinyi mko ndani ya hifadhi ya reli basi itabidi upande ule wa reli nao waondoke. Lakini endapo tutapata pesa za kupanua barabara sasa hivi tumewawekea alama wajue. Kwa hiyo, wale wenye uwezo ambao wanaweza kuamua kuondoka sasa wenyewe, wanaweza kuondoka. Je, waliohamishwa wakati wa vijiji vya ujamaa, sasa hatuoni kwamba ni usumbufu? Wakati wa vijiji vya ujamaa, vijiji vya ujamaa vilivyopimwa vilizingatia sheria zote za nchi hii. Lakini baada ya kupima hivyo vijiji na kuondoka wananchi waliamua kusogea zaidi kwenye barabara. Kwa hiyo, bado pale sheria iko pale kwamba waliopima vijiji na ukiangalia hati ya kijiji itakuambia wazi kwamba barabara imeachwa kwa kiwango hicho cha sheria. Sasa wananchi wale ambao wamehamia kule sisi hatuwasumbui, ila tunawaomba wazingatie sheria kwamba kuna *road reserve*.

Na. 150

### **Barabara Kutoka Shelui – Kidarafa**

**MHE. LEONARD M. SHANGO** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya kutoka mji mdogo wa Shelui Wilaya ya Iramba Kwenda Kidarafa kupitia vijiji vya Mgongo, Sekenke Machimboni, Ntwike, Doromoni, Kidaru, Ndurumo, Ibagi mpaka Kidarafa umbali wa takriban km 120 sasa inahudumiwa na wakala wa barabara wa Mkoa *TANROADS* kuishia kwenye daraja la kijiji cha Sekenke yaani Shelui umbali wa km 18:-

- (a) Je, Serikali ilitumia kigezo gani cha msingi kuamua kuhudumia barabara hiyo kama barabara ya Mkoa yaani kutoka Shelui – Daraja la Kijiji cha Sekenke km 18 na kuacha sehemu kubwa ya barabara inayoendelea mpaka Kidarafa umbali wa km 120?
- (b) Je, Serikali inawaeleza nini wananchi wa bonde hilo maarufu kwa kilimo, madini, uvuvi, ufugaji na misitu asilia, kwani kutoihudumia barabara yote kunawafanya wananchi kwenye bonde hilo waendeleo kutengwa ki-mawasiliano na juhudi zao za kupambana na umaskini zinazoroteshwa?
- (c) Kama Serikali itaona umuhimu wa kutengeneza barabara hiyo km 120 pamoja na madaraja/ *drifts/culverts* ambayo inapitika tu wakati wa kiangazi je, ujenzi huo utagharimu fedha kiasi gani na itanza kutengenezwa lini?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Leonard Mlumba Shango, Mbunge wa Iramba Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*) Mkoa wa Singida inahudumia jumla ya kilometa 21.7 kutoka Shelui hadi Ntwike.

Aidha, sehemu ya barabara iliyobaki kati ya Ntwike hadi Kidarafa, inahudumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Iramba. Vigezo vilivyotumika kupandisha hadhi ya barabara hii kutoka Shelui hadi Ntwike kuwa ya Mkoa ni vile vilivyopo kwa muibu wa Sheria ya Barabara.

Hata hivyo, hivi sasa Wizara yangu inafanya mapitio ya Sheria ya Barabara (*Highway Ordinance – Cap 167*) ambayo ndani yake barabara zote nchini zitawekwa kwenye makundi au madaraja yanayostahili kulingana na vigezo vya kitaalam, pamoja na maombi ya Bodi ya Barabara ya Mkoa husika.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inazifanyia matengenezo barabara zote kulingana na uwezo wake kifedha. Aidha, kulingana na uwezo mdogo wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba, barabara hii imekuwa ikipata matengenezo ya kawaida ambayo hayakidhi hali halisi ya uharibifu.

(c) Mheshimiwa Spika, gharama za ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha changarawe unakadiriwa kufikia shilingi bilioni 1,966 milioni. Aidha, kama nilivyojibu katika sehemu (a), barabara hii inahudumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Iramba.

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza.

Je, Serikali itakuwa tayari sasa kujenga madrift na madaraja katika makorongo katika barabara hii na wananchi watachangia kwa kutengeneza barabara kwa sababu barabara hii haipitiki kabisa kwa wakati wote wakati wa msimu wa mvua?

Pili, barabara ya kutoka kijiji cha Kisiriri kwenda Kidaro kupitia Mlimani ni mbaya sana haipiti kabisa. Je, Serikali itakubali kutengeneza hiyo sehemu ya Mlimani kusudi wananchi wanaotoka Bondeni Kijiji cha Kidaru na vijiji vingine vya Kegelo na Ndulumo waweze kufika kupitia barabara hii kwa kupitisha mazao yao na huduma za jamii? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, katika kitu aghali sana kutengeneza katika barabara ni madrift na makalvati haya ni aghali na ndiyo yanayoongeza bei kubwa sana. Sasa nikikukubalia hapa Mheshimiwa Mbunge kwamba tutajenga ninakuongopea. (*Makofi*)

Tunakwenda kwa Bajeti ambayo itapitishwa hapa na Bajeti hiyo kwa barabara hizi ni Bajeti ya TAMISEMI na Bajeti ya Wizara ya Ujenzi. Ningekuombeni Waheshimiwa Wabunge kutoka Iramba Singida kuwa mjenge hoja juu ya barabara hii mkaipeleke TAMISEMI ili inapotokea fedha za kutoka *ROAD FUND BOARD* basi wafikirie ombi lenu maalum la barabara hii.

Je, tutajenga sehemu mbaya ya makorongo ya Kisiriri hadi Kidaru. Jibu ni lile lile tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sasa hivi hapa nilipo hata kukutamkia ndiyo siwezi, au kukutamkia hapana siwezi. Kwa sababu Bajeti yenyewe haijapitishwa ndiyo hii tunaomba. Nakuomba Mheshimiwa Mbunge ushiriki katika kupitisha Bajeti hii ili tufikirie. (*Kicheko/Makofi*)

**MHE. EMMANUEL E. KIPOLE:** Ninakushukuru Mheshimiwa Spika, kuniona niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri katika jibu lake la msingi amegusia Sheria ya *Highway Ordinance* ya mwaka gani sijui. Kwa kuwa tangu mwaka 2001 amekuwa akizungumzia mapitio ya Sheria hiyo, na mpaka leo haijamalizwa. Hii Sheria ina ukubwa gani na itachukua miaka mingapi kuipitia?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, Sheria ya *Highway Ordinance Cap No. 167* ni kubwa kwa kuijadili na ni kubwa kwa umuhimu. Kwa sababu hii ndiyo sheria inayopanga madaraja yote ya barabara nchini. Kila barabara lazima iwe na namba na lazima iwe na daraja lake. Tukikosea ikija hapa tukaiacha basi barabara hiyo itakuwa pengine haitengenezwi kila wakati na Mbunge yeyote atakuwa analalamika, la kwanza.

La pili, hii sasa wadau wameipitia Sheria hii. Ipo tayari kuja Bungeni, bahati mbaya kipindi hiki haiwezi kuja. Lakini wale watakaorudi wataijadili mapema watakapofika na kuapa na kufungua Bunge. Kwa hiyo, mnamo mwezi Februari mwakani nina hakika kabisa Sheria hii itakuwa mezani na Wabunge wataijadili kwa marefu na mapana.

Na. 151

### **Kompyuta kwa ajili ya Vyuo vya Maendeleo**

**MHE. DIANA M. CHILOLO** aliuliza:-

Kwa kuwa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vimepiga hatua ya kimaendeleo kwa kuboresha majengo, mazingira ya utoaji wa taaluma na kadhalika na kwa kuwa hii ni karne ya Sayansi na Teknolojia ambapo walimu na Makarani wamesomea kompyuta:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka kompyuta kwenye Chuo cha Maendeleo Singida na Chuo cha Maendeleo Msingi ili wahusika waweze kuweka kumbukumbu na kurahisisha utekelezaji wa kazi wa kila siku?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-



Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mbunge Viti Maalum, kwamba hii ni karne ya Sayansi na Teknolojia. Kwa kuzingatia ukweli huo kati ya Vyuo 58 vya Maendeleo ya Wananchi, Vyuo 25 vina idadi ya kompyuta zipatazo 80 ambazo zimepatikana kutoka kwa washiriki mbalimbali, wengi wao wakiwa vyuo rafiki vya Sweden, Finland na Uingereza. Aidha, Vyuo vya Handeni na Mamtukuna vimepatiwa kompyuta na Wabunge wa Majimbo yao. Natoa pongezi kwa Waheshimiwa Wabunge hao ambao ni Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Mramba waliotoa misaada kwenye vyuo hivyo. Vyuo vya Singida na Uyole vimejinunulia kompyuta kwa kutumia fedha za miradi ya uzalishaji mali ambapo Chuo cha Msingi kimepatiwa kompyuta 5 na Shirika la Kimataifa la Mawasiliano (*International Telecommunication Union*) kwa ajili ya mradi wa Mawasiliano (*Telecentre*).

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kujibu swali la msingi la Mheshimiwa Diana Chilolo, kama ifuatavyo:-

Kwa mwaka 2005/2006 Serikali kupitia Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini Tanzania MKUKUTA, itaimarisha mawasiliano kununua kompyuta 20 na kuzipeleka vyuoni. Aidha baada ya ununuzi wa kompyuta hizo Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Singida na Msingi vitakuwa miongoni mwa vyuo vitakavyofikiriwa kupewa kompyuta. Hata hivyo chuo hicho kwa sasa kina kompyuta moja (1) ambayo ilinunuliwa kwa fedha za uzalishaji mali pia chuo cha Msingi kina kompyuta tano (5) ambazo ni msaada kutoka Shirika la Kimataifa la Mawasiliano (*ITU*).

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii nimpongeze sana Mheshimiwa Diana Chilolo, ambaye pia ni mjumbe wa Bodi ya Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Singida, kwa kazi nzuri anazozifanya kwa kushirikiana na wananchi katika kuleta maendeleo zaidi ya Chuo cha Singida.

Ni matumaini yangu kwamba Mheshimiwa Diana Chilolo, Mbunge ataendelea kushirikiana na Wizara yangu katika mchakato mzima wa maboresho ya vyuo kuptia Bodi za Vyuo hadi kufikia viwango vya kuridhisha katika karne hii ya sayansi na teknolojia. Ahsante.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nashukuru kwa kuona umuhimu wa kupeleka kompyuta katika Chuo cha Maendeleo cha Singida Mjini na Chuo cha Maendeleo Msingi kwa lengo lile lile la kuingia katika teknolojia.

Ningependa basi Mheshimiwa Waziri aniambie pia umuhimu wa kupeleka vyerehani vinavyotumia umeme pamoja na vyombo vya useremala vinavyotumia umeme ili tuendane na karne hii ya sasa ya teknolojia? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:**  
Mheshimiwa Spika, umuhimu wa kupeleka vyerehani na hivyo vinginevyo alivyovitaja kama vile vifaa vya ujenzi vipo na umuhimu upo.

Lakini tunapeleka kidogo kidogo kwa ababu ya Bajeti yetu. Lakini pamoja na hilo bado ninapenda kumweleza Mheshimiwa Chilolo kwamba tushirikiane maana wako wadau wengi, wako watu binafsi, wapo pia Waheshimiwa Wabunge na taasisi za dini.

Kwa mfano, Mheshimiwa Said Nkumba pale anaisaidia kweli chuo chake. Mheshimiwa Ndeka pia nilipotembelea pale. Mheshimiwa Mudhihir nilipotembelea kwake ametoa kiasi cha shilingi milioni 17 kwa *FDC* ya Chilala Rutamba kununulia vifaa vya ujenzi na kwa shughuli za mafunzo. (*Makofi*)

Kwa hiyo, naomba wadau tuko wengi, tujitokeze kuvisaidia vyuo hivi. Lakini hapo hapo naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa sababu wameweza kusaidia vyuo vyao kwa namna moja au nyingine katika maeneo yao. Taarifa tunazo kwamba wamefanya kazi nzuri sana. (*Makofi*)

Na. 152

### **Shule za Msingi katika Maeneo mbalimbali**

**MHE. ARIDI M. ULEDI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imekuwa ikizigawa shule za msingi zenye watoto wengi na kuzifanya shule mbili au zaidi na kwa kuwa, yapo maeneo mengi hasa ya vijijini ambayo yana watoto wengi waliofikia umri wa kwenda shule lakini wameshindwa kufanya hivyo kutokana na kukosekana kwa shule:-

- (a) Je, ili shule ya msingi iwe halali kuwepo inatakiwa kuwa na wanafunzi kuanzia wangapi na idadi ya juu ni wangapi?
- (b) Je, kwa nini vijijini mwanafunzi analazimika kutembea umbali gani ili kuifikia shule?
- (c) Kwa yale maeneo ambayo shule ziko mbali sana kwa watoto wadogo kuweza kwenda kusoma. Je, Serikali itakuwa tayari kujenga shujle karibu ili lengo la watoto wote wanaotakiwa kwenda shule kwa umri unaotakiwa liweze kutimia?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Aridi Mwanache Uledi, Mbunge wa Nanyumbu lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, utafiti mbalimbali wa Kitaifa na Kimataifa umeonyesha kuwa upo uhusiano kati ya ufanisi wa kufundisha na kujifunza na wingi wa wanafunzi darasani na shuleni. Aidha uwezo wa kuendesha shule kwa ufanisi wa gharama nafuu bila kuathiri ubora wa elimu inayotolewa unategemea pia ukubwa wa shule na wingi wa wanafunzi. Kwa kuzingatia utafiti huo wa kitaalamu, Wizara yangu imeweka viwango vya wingi wa wanafunzi darasani kama ifuatavyo:-

Wingi wa wanafunzi darasani usizidi 40. Shule za msingi za vijijini zisizidi mikondo miwili sawa na wanafunzi arobaini mara mbili madarasa saba jumla wanafunzi 560 ukubwa wa shule za miji usizidi mikondo mitatu mara wanafunzi 40x7 jumla wanafunzi 840. Endapo shule inafikia kiwango cha juu kabisa yaani 560 kijijini na 840 kwa mijini hapana budi kuanzisha shule nyingine katika eneo litakaloonekana kuwa linafaa ili kuwapunguzia umbali wanafunzi eneo husika kwa kuzingatia *school mapping* na *micro planning* ambayo imefanywa katika kila wilaya na kwa kila shule na taarifa hizo ziko na maafisa elimu wa wilaya.

(b) Mheshimiwa Spika, inashauriwa kuwa umbali wa wanafunzi kutembea kwenda shule usiwe zaidi ya kilomita sita.

(c) Mheshimiwa Spika, pale ambapo watoto wenye umri wa kwenda shule wanashindwa kuifikia shule iliyopo kutokana na umbali upo utaratibu wa kuanzisha shule tegemezi ambayo ukubwa wake utategemea idadi ya watoto wa umri wa kwenda shule waliopo katika eneo hilo. Shule za aina hiyo zinaruhusiwa kuanzisha kwa darasa la kwanza hadi la pili au la nne. Baada ya hapo wanafunzi hujiunga katika shule mama ambayo inafika hadi darasa la saba, kwa kuwa wakati huo umri wao utakuwa unaruhusu kutembea mwendo mrefu, yaani mwendo wa hizo kilomita sita. Shule za aina hii zipo katika baadhi ya maeneo kama ya Vituo vya reli, vituo vya hifadhi za wanyama pori, au kwa wafugaji wanaohamahama na maeneo yalitenganishwa kati ya eneo lenye shule na ng'ambo ya mto mkubwa au msitu mnene.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Pamoja na majibu ya mazuri ya Mheshimiwa Waziri ningependa kuuliza kama ifuatavyo; kwa kuwa tatizo la umbali hasa kwa watoto wa mikoa hii ya Mtwara na Lindi lipo na mara nyingi shule hizo anazosisema tegemezi huwa hazina utaratibu mzuri. Je, Wizara haifikirii kwamba itoe kibali maalum kwamba shule hizi tegemezi baadaye ziwe hasa hasa shule za msingi katika maeneo hayo?

Namba mbili ni kwamba kwa kuwa shule nyingi zilizo mbali hasa vijijini zinashida sana ya walimu. Je, Wizara haikubali sasa kwamba ipo haja ya kuwa na mpango maalum wa kuwamotisha walimu ama kwa fedha ama kwa *promotion* ili waweze kwenda kufundisha katika maeneo haya magumu.

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu maswali yake mawili kama ifuatavyo:

La kwanza, kwamba shule tegemezi iruhusiwe kukua ili iweze kuwa shule ya msingi kamili, hili linawezekana kutegemea na wingi wa wanafunzi naomba ikumbukwe ile namba niliyoisema kwa ajili ya *variability* yaani shule ile kujiendesha kwa unafuu wa gharama. Kama kuna dalili inayoonyesha kwamba shule ile kutokana na ongezeko la watu na ongezeko la watoto katika eneo lile inaweza kukua ikafikia zile namba nilizozungumzia kwa kweli utaratibu unaruhusu kuweza ile shule tegemezi au *satellite school* ifikie kiwango cha shule kamili.

La pili, kwamba katika maeneo ambako tuna shida ya walimu hasa maeneo ambayo tunayaita yako mbali au katika maeneo yaliyojitenga *remote locations* kumotisha walimu. Kwa sasa hivi tunachofanya kumotisha walimu ni kuwajengea mazingira mazuri ya kuishi, maelekezo ambayo Wizara yangu imetoa ni kwamba katika kujenga nyumba za walimu kutokana na ruzuku ya maendeleo inayotolewa chini ya MEM katika kujenga nyumba za walimu, zijengwe nyumba nzuri kwanza katika maeneo hayo kuliko maeneo ya mjini.

Jambo hili naomba sana tushirikiane kulisimamia kwa sababu kuna *tendency* ya kujenga nyumba nzuri katika maeneo ya miji au katika vijiji ambavyo vinajulikana walimu wakikosa nyumba wanaweza kupanga. Tungetoa *focus* kubwa zaidi kwenye maeneo anayozungumzia Mheshimiwa Mbunge ungeweza ukawa ni motisha wa kutosha kufanya walimu wakubali kwenda kukaa ama wasione shida kubwa kwenda kukaa katika maeneo hayo.

Na. 153

### **Nyimbo za Bendi za Muziki**

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Watanzania tunayo sifa kwa kuendeleza Utamaduni wetu wa asili katika lugha, michezo na kadhalika.

- (a) Je, Serikali haioni kwamba zipo baadhi ya bendi za muziki zinazoelekeza kupotosha Utamaduni huo kwa kuelekeza nyimbo zake nyingi katika mwelekeo wa matusi?
- (b) Je, Serikali ina kipimo gani kinachotumiwa kuhalalisha nyimbo hizo kabla ya kurekodi na kurushwa hewani?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mossy Selemani Mussa, Mbunge wa Mfenesini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa zipo baadhi ya bendi za muziki ambazo zinavuka mipaka ya uhuru wao katika kufikisha malengo yaliyokusudiwa kwa jamii kupitia miundo na mitindo ya usanii wanayoitumia, iwe katika ngoma, nyimbo, tungo mbalimbali au tamthiliya, kuwa na mwelekeo wa matusi na hivyo kupotosha Utamaduni wa Mtanzania. Serikali kwa kutambua umuhimu wa wasanii katika jamii huchukua hatua mbalimbali za kurekebisha kasoro hizo, ikiwa ni pamoja na Wizara yangu kupitia Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) kuandaa semina za afunzo za mara kwa mara kwa wasanii zenye lengo la kurekebisha kasoro hizo na kukemea pale inapoibidi kufanya hivyo. Katika mwaka wa 2004/2005 BASATA iliendesha mafunzo kwa wasanii 110 wa sanaa za maonyesho, 120 kwa viongozi wa vikundi na 20 wa muziki wa taarabu juu ya umuhimu wa sanaa katika jamii na umuhimu kwa wasanii kuzingatia maadili na kuwapa wasanii hao mbinu thabiti za jinsi ya kuendesha shughuli zao kibiashara ili kujiongezea mapato.
- (b) Mheshimiwa Spika, nyimbo za bendi hazihalalishwi na Serikali kabla a kurekodiwa na Redio au Televisheni na kurushwa hewani. Vituo vyenyewe ndivyo huweza kukataa kurekodi nyimbo ambazo, kwa uelewa wao wanaona zinakiuka maadili na vigezo vya adabu vya jamii ya Watanzania. Wizara yangu kupitia BASATA, huchukua hatua za kushauri kupitia wahariri wa vyombo husika, nyimbo zinazokiuika maadili na Utamaduni wa Mtanzania zisiimbwe katika maonyesho au kurushwa hewani.

Mheshimiwa Spika, wajibu wa wasanii wakiwemo wanamuziki ni kuelimisha, kuburudisha na kuhamasisha maendeleo na mabadiliko mbalimbali katika jamii. Kwa hiyo, napenda kuchukua fursa hii kutoa wito kwa wanamuziki na wasanii wote kwa ujumla kuwa makini katika tungo zao na katika kufikisha malengo yaliyokusudiwa kwa jamii kupitia nyimbo na mitindo ya Usanii wanayoitumia. Sanaa haiwezi kuelimisha au kuasa jamii iwapo sanaa yenyewe ni potofu.

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba kuuliza kwamba ikiwa Serikali inajitoa katika kuratibu nyimbo na usanii katika vyombo vyetu vya habari Serikali haioni kwamba kutakuwa na mambo ambayo ya matusi ya kupindukia kitu ambacho kitapelekea jamii yetu kupotoka.

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda niseme katika maelezo yangu sikusema kwamba Serikali inajitoa kabisa, Serikali bado inafulsa ya kutoa ushauri moja kwa moja kwa makundi haya mawili;

Moja ni wasanii wenyewe na pili kutoa ushauri kwa vyombo vya habari ambavyo vinawatangaza hawa wasanii. Tunafanya semina kwa makundi yote mawili na kwa kufanya hivyo tunazingatia sheria iliyotungwa na Bunge hili. Endapo Mheshimiwa

Mbunge anapendekeza kwamba Serikali iweke *control* zaidi yaani watu wasitangaze jambo mpaka Serikali ipitishie, basi haya masuala ya kuleta pendekezo tuitizame upya ile Sheria. Lakini mimi wasiwasi wangu ni kwamba tukiingilia mno badala ya kuelimisha na kushawishi tukaweka *control* mno tutaleta ukiritimba. Kama mnavyojua Serikali ikianza kushughulikia maana yake kabla ujangaza wimbo uletwe Serikalini utazamwe unaweza ukakuta kuna mlundikano wa mambo yanayochelewa bila sababu. Kwa maoni yangu jambo hili halijaharibika kiasi hicho, mimi naona tuendelee na utaratibu wa sasa.

Na. 154

### **Mradi wa Umeme wa Gesi ya Songosongo**

**MHE. BAKARI M. MBONDE** aliuliza:-

Kwa kuwa, Miji ya Utete, Ikwiriri, Kibiti na Vijiji kadhaa Wilayani Rufiji vitapata umeme kutokana na mradi wa umeme wa gesi ya Songosongo;

- (a) Je, Maandalizi ya mradi wa kuipata Miji hiyo na vijiji husika umeme yamefikia hatua gani?
- (b) Je, utandazaji wa nyaya za umeme katika miji ya Utete na Kibiti utanza lini?
- (c) Je, ni lini fidia italipwa kwa Wananchi wa Wilaya ya Rufiji watakoathirika na utekelezaji wa mradi huo wa umeme wa gesi ya Songosongo?

**WAZIRI MAWASILIANO NA UCHUKUZI (K.n.y WAZIRI WA NISHATI NA MADINI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bakari Mbonde, Mbunge wa Rufiji, kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuna mpango wa kuipatia umeme wa gesi ya Songosongo miji ya Utete, Ikwiriri, Kibiti na vijiji kadhaa vya Wilaya ya Rufiji chini ya mradi wa umeme unaoitwa *Way leave village Electrification Scheme (WVES)*.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi huu umeanza mwezi Juni 2005 yaani mwezi huu. Baada ya fidia ya mali za Wananchi kulipwa pamoja na matayarisho mengine kufanyika na kuendelea kufanyika. Mpaka sasa Serikali imeingia mikataba mbalimbali kupitia Kampuni ya *TANESCO* kwa kazi zifuatazo:-

- (i) Ujenzi wa *Power House* pamoja na nyumba za wafanyakazi maeneo ya Somanga Funga, Mkataba na Kampuni ya *DB Shapriya (DSM)* umekamilika. Ujenzi unategemewa kuanza mwezi Agosti, 2005.

- (ii) Kutengeneza, kusafirisha na kufunga mashine ya kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilia ya Songo Songo. Majadiliano kabla ya kusaini mkataba na Kampuni ya *Renco* ya Italia yatafanyika tarehe 28/6/2005 yaani leo hii. Ufungaji wa mitambo hii kutategemea kumalizika kwa ujenzi wa *Power House* pale Somanga Funga.
- (iii) Ujenzi wa laini ya kilovoti 33 kutoka Somanga Funga hadi Singino (Kilwa Masoko) na hadi Utete, Ikwiriri, Mchukwi Hospitali, Kibiti na Bungu. Mkataba na Mkataba na Kampuni ya *Eltel Networks* (Sweden) uko katika hatua za mwisho kukamilika. Ujenzi unategemewa kuanza mwezi Agosti, 2005.
- (iv) Ujenzi wa laini ndogo za usambazaji umeme katika maeneo ya Nangurukuru, mchukwi, Somanga Funga, Muhoro, Utete, Hospitali ya Mchukwi, Kijiji cha Kindwitwi, Kibiti na Bungu. Mkandarasi aliyekuwa amepatikana yaani kampuni ya *Roshmoon Private* ya *South Africa*, hakukidhi mahitaji. Hivyo zabuni itatangazwa upya, kwa utaratibu wa kawaida, kama Benki ya Dunia itaridhia, ujenzi utaanza mwezi Desemba au Januari mwakani. Hata hivyo ujenzi wa mradi huu utategemea sana maendeleo ya ujenzi wa mradi wa *line* kubwa ya kilovoti 33.
- (v) Kuvipatia umeme vijiji vitano katika Wilaya ya Temeke na Mkuranga kwa njia ya laini ya kilovoti 11 na 33 vijiji hivyo ni, Chamazi, Mbande, Mwanambaya, Dundani na Mipeko/Kimbangule. Mkataba na Kampuni za *Berkley Contractor Ltd* ukishirikiana na *Harbour and Rural Engineering Limited* umekamilika. Ujenzi unategemea kuanza mwezi Agosti, 2005.
- (vi) Mradi wa kuvipatia umeme vijiji 25 kwa nguvu za Mionzi ya jua umefutwa kutokana na kutokubalika na Wananchi katika vijiji hivi pamoja na kushindwa kupata mkandarasi ambaye angeweza kuusimamia na kuuendesha kwa ufanisi na bila matatizo yoyote. Kazi ya kutayarisha mradi mbadala bado inaendelea.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa fidia ya mali za Wananchi zimeshafanyika kwa takribani asilimia 96. Asilimia 4 iliyosalia ni wale ambao hawakupatikana na wale wenye manung'uniko na fidia waliyopewa. Hivi sasa maafisa kutoka Wizara yangu, Wizara ya Ardhi na *TANESCO* wako huko, kumaliza kero hiyo kabisa.

Mheshimiwa Spika, tarehe 24 mpaka 25 Machi, 2005, Mheshimiwa Dr. Ibrahimu Msabaha, Naibu Waziri wa Nishati na Madini, alitembelea Utete, Ikwiriri na Kibiti, wilaya ya Rufiji kukagua mradi wa kupeleka umeme huko.

Katika ziara hiyo alifuatana na Mheshimiwa Prof. Juma Mikidadi Mbunge wa Kibiti na Mheshimiwa Bakari Mbonde, Mbunge wa Rufiji. Wizara inawashukuru Waheshimiwa Wabunge hao kwa juhudi zao katika kusimamia mradi huu na katika maendeleo ya Wilaya ya Rufiji.

**MHE. BAKARI M. MBONDE:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Waziri kwa majibu yake mazuri sana na swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa vijiji vya Ruwe hadi Mkongo kwenye kata ya Mkongo na Kilima hadi Mloka kwenye kata za Mwasyeni

na Ngorongo katika Jimbo la Rufiji viko mbali na mradi huu wa gesi ya SongoSongo, na kwa kuwa kuna mfuko wa nishati ya vijijini.

Je, Serikali ina mpango gani wakupatia umeme vijiji hivyo ili wananchi hao nao wafaidike na utekelezaji wa sera za Chama cha Mapinduzi zinazojali maendeleo ya wananchi. Je, Mheshimiwa Waziri kama kawaida yake atakuwa tayari tukae kutafakari kwa pamoja suala hili?

**WAZIRI MAWASILIANO NA UCHUKUZI (K.n.y. WAZIRI WA NISHATI NA MADINI):** Mheshimiwa Spika, Serikali ya Chama cha Mapinduzi, ni Serikali sikivu amesema tumesikia tutalizingatia.

Na. 155

### **Umeme Unaotumika Ugunja**

**MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN** aliuliza:-

Kwa kuwa umeme unaotumika katika Kisiwa cha Ugunja unatoka Kidatu na kwa kuwa umeme huo umeunganishwa na *Marine Cable* inayoanza *Ras Kilomoni* hadi kwa Fumba. Je, *Marine Cable* hiyo imewekwa mwaka gani na inaweza kutumika kwa ufanisi kwa miaka mingapi?

**WAZIRI MAWASILIANO NA UCHUKUZI (K.n.y. WAZIRI WA NISHATI NA MADINI):** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba swali la Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan , Mbunge wa Kikwajuni, kama ifuatavyo:-

Umeme unaotumika Ugunja unatoka kituo cha Ubungo kwa njia ya umeme yenye msongo wa kilovoti 132 hadi *Ras Kilomoni* ambapo umeme huo husafirishwa kwa waya maalum unaopita chini ya bahari yaani *Submarine Cable* iliyowekwa mwaka 1980. Waya huu maalum unakadiriwa kufanya kazi yake ya kupitisha umeme kwa ufanisi kwa muda wa takriban miaka 50 tangu ufungwe na baada ya hapo wataalamu wa umeme huchukua vipimo kwa ajili ya kuangalia ufanisi wake. Swali Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan ni la msingi sana kwani waya huu wa umeme ni kielelezo cha ushirikiano katika huduma za kiuchumi kati pande mbili za Muungano, tunamshukuru.

**MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Je, *sub arine cable* hii inasimamiwa na nani kimatengenezo, yaani *TANESCO* au Shirika la Umeme Zanzibar?

**WAZIRI MAWASILIANO NA UCHUKUZI (K.n.y. WAZIRI WA NISHATI NA MADINI):** Mheshimiwa Spika, njia hiyo yaani *submarine cable* ni mali ya *TANESCO*, makubaliano kama yalivyo katika mkataba ni kwamba *TANESCO*



watafanyia matengenezo njia hiyo, lakini vilevile kwa kushirikana na Shirika la Umeme Zanzibar, Shirika la Umeme litatoa vifaa vya matengenezo hayo.

Na. 156

### **Reli ya Mikoa ya Kusini**

**MHE. LYDIA THECLA BOMA** aliuliza:-

Kwa kuwa sababu za Serikali za kuing'oa reli inahudumia Mikoa ya Kusini yaani Lindi na Mtwara zimepitiwa na wakati hasa kwa kuwa siku hizi kuna ushindani mkubwa wa kiuchumi. Je, ni lini Serikali itatoa tamko rasmi la kuanzisha upya mikakati ya kurudisha reli hiyo ili kuharakisha kufufua uchumi wa mikoa hiyo.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Njia za reli kutoka bandari za Lindi hadi Ruo na Mtwara hadi Ruo zilijengwa mwaka 1949 na 1954. Njia hii ilifika Nachingwea mwaka 1949 na Masasi mwaka 1958. Reli hii ijulikanayo kama *The Great Groundnut Line* ilijengwa kwa lengo la kusafirisha zao la karanga pamoja na mazao mengine ya biashara. Hata hivyo lengo hilo halikufanikiwa. Kutokufanikiwa kwa zao hilo la karanga kulisababisha reli hii kung'olewa mwaka 1963.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lydia Thecla Boma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mikoa ya Lindi na Mtwara ni miongoni mwa mikoa iliyopo kwenye Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara yaani Mtwara *Development Corridor (MDC)*. Chini ya ukanda huu Serikali imeandaa mpango kabambe wa kufufua uchumi kwa kuimarisha miundombinu na kutumia rasilimali zinazopatikana katika ukanda huu ikiwemo, madini, mazao ya kilimo, utalii na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kikwazo kikubwa cha maendeleo katika mikoa hii ni ukosefu wa miundombinu ikiwemo barabara, reli na kadhalika. Kwa ajili ya kusafirisha bidhaa mbalimbali kutoka mahali zinapozalishwa hadi kwenye masoko ya ndani na ya kimataifa. Moja kati ya miundombinu muhimu inayohitajika kwa ajili ya kufufua uchumi wa mikoa husika na uchumi wa Tanzania ni kuwa na reli ya Mtwara Songea – Manda.

Napenda nimjulishe Mheshimiwa Mbunge kuwa upo mradi wa reli ya Mtwara Songea – Manda; ambao umebuniwa kwa lengo la uendelezaji wa Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara. Lengo kubwa la mradi huu ni kuweka miundombinu ya reli ili iweze kufikia maeneo husika na kuwezesha usafirishaji wa madini ya makaa wa mawe ya Mchuchuma na chuma cha Liganga baada ya kuchimbwa na kusafirishwa kwenda kwenye soko la kimataifa kupitia bandari ya Mtwara. Reli hiyo pia ina lengo la kuunganisha Tanzania,

Malawi na Zambia iwe Ukanda mbadala. Hivyo basi, *Mbamba Bay* na *Mkata Bay* zitaunganishwa kwa *Wagon Ferry*

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi huu unahitaji mtaji mkubwa ili kuipunguzia Serikali mzigo wa kukopa na kisha kulipa madeni. Mkakati uliopo ni kutekeleza mradi huu kupitia sekta ya wawekezaji binafsi au kwa ushirikiano kati sekta binafsi na sekta ya umma.

**MHE. LYDIA THECLA BOMA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri nipongeze hiyo taarifa ambayo ina mwelekeo kidogo.

Swali la kwanza, kwa kuwa huo mpango wa *Mtwara Corridor* mpaka sasa tangu umeanzishwa ni kuribu miaka arobaini unasuasua, hauendi sawa na malengo. Je, Serikali sasa itakubali kuanzisha mamlaka muhimu ambayo itasimamia *Mtwara Corridor* kusitawisha?

La pili, kwa kuwa wanawake walio wengi nchi hasa mikoa ya Kusini ndio wazalishaji na ndio wenye Serikali hii. Je, Serikali itakubaliana na mimi kwamba haijawatendea haki kwa sababu hata maswali yake hajataja reli itatoka *Mtwara* kwenda mikoa ya kati au Kusini kusafirisha mazao yao.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, mimi nasema kwamba tutawaomba mamlaka inayosimamia suala hili ikiwa ni Wizara ya Ujenzi ilichukue wazo hilo la kuwa na mamlaka kama wataona linafaa. Nafikiri Mheshimiwa Mbunge atapewa taarifa inayofaa.

Mheshimiwa Spika, pili navyoelewa kwamba reli licha kwamba inasaidia kubeba mizigo lakini haibagui, sote ni abiria wetu kina mama, kina baba na jamii yote kwa jumla inapata huduma hiyo reli inapopita.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri napenda kutoa majibu ya nyongeza kwa Mheshimiwa Boma kama ifuatavyo;

Kwanza si kweli kwamba mradi wa *Mtwara Development Corridor* unasuasua, mradi wa *Mtwara Development Corridor* unaendelea vizuri na katika kipindi kilichopita karibu miezi miwili hadi mwezi mmoja uliopita marais wananchi wanne Tanzania, Msumbiji, Zambia na Malawi walikutana katika mji wa Lilongwe kusaini mkataba wa makubaliano ya *Mtwara Development Corridor*.

Lakini katika miradi inayoendelea sasa hivi iliyo ndani ya *Mtwara Development Corridor* ni pamoja na barabara ya kutoka *Mtwara*, Masasi hadi *Mbamba Bay* yenye jumla ya kilomita 826 ambayo *design* yake imekwisha malizika kufanyika, na katika

Bajeti ya mwaka huu zimetengwa zaidi ya bilioni tano za kumalizia *design* na kutangaza *tender* kwa ajili ya kumpata mkandarasi.

Kwa hiyo, huko si kusuasua, lakini pia katika mradi mwingine wa *Unity Bridge* Serikali ya Tanzania na Serikali za *Mozambique* zilisaini makubaliano marais wetu wawili kule Pemba Msumbiji na wameamua kuitengeneza ile barabara kwa kutumia fedha zao.

Daraja hilo *Unity Bridge* litagharimu karibu shilingi bilioni 33 na katika Bajeti ya mwaka huu 2005/2006 kwa Serikali zote mbili zimetenga zaidi ya bilioni 9 na jiwe la msingi la daraja hilo litawekwa mwezi Septemba mwaka huu 2005.

Kwa hiyo, huko sio kusuasua, kwa hiyo nataka kumthibitishia Mheshimiwa Mbunge kwamba mradi wa *Mtwara Development Corridor* hausuisui bado unaenda kwa *speed* kubwa ya moto sana.

Na. 157

### **Uwanja wa Ndege Mkoa wa Karega**

**MHE. DR. DIODOROS BUBERWA KAMARA** aliuliza:

Kwa kuwa wananchi wa Mkoa wa Kagera wanashauku kubwa yakuwa na uwanja wa ndege wa kimataifa na kwa kuwa uwanja huo utasaidia sana kuunganisha mkoa wa Kagera na nchi jirani pamoja na mataifa mbalimbali duniani. Je, Serikali imechukua hatua zipi za kuwezesha kujengwa kwa uwanja wa Kimataifa wa Kajunguti?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Diodoros Buberwa Kamala, Mbunge wa Nkeng, kama ifuatavyo:-

Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi ilipata nafasi ya kujibu swali namba 857 toka kwa Mheshimiwa Lwakatare, Mbunge wa Bukoba Mjini, lenye mantiki sawa na swali hili la leo la Mheshimiwa Dr. Kamala. Kama nilivyojibu kabla kuwa upembuzi yakinifu wa awali ulifanywa na Shirika la *Overseas projects corporation of Victoria* ya Australia, chini ya ufadhili wa *Commonwealth Secretariat* mwaka 1998/1999. Kiwanja kilibainishwa kijengwe katika sehemu mpya ijulikanyo kama Omukajunguti.

Gharama za ujenzi huo zilikuwa ni shilingi 15.863 milioni iwapo uwanja utakuwa na uwezo wa kuhudumia ndege aina ya *Fokker 27* na shilingi 26.982 milioni kwa ndege ya *Boeing 737*. Tunaamini gharama hizo kwa sasa zitakuwa zimezidi. Wizara tayari imeshapeleka tena maombi ya msaada *Secretariat* ya *Common wealth* kwa lengo la kufanya upembuzi yakinifu wa kina na bado ombi hili halijazaa matunda.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania, imeendelea kutafuta Kampuni binafsi ambazo zingelipenda kuwekeza kwenye kiwanja hicho kwa mtindo wa Jenga endesha na baadaye kabidhi (*BOT*). Baadhi ya makampuni toka nje yameonyesha nia hiyo ya kuwekeza ila wangelipenda kupata taarifa ya upembuzi wa kina, kitu ambacho ndicho kilichotukwamisha, yaani uhaba wa fedha. Tuko tayari kupokea ushauri na ushirikiano katika jambo hilo.

**MHE. NJELU E.M. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Mimi nilitaka niulize swali linalofanana na la Mheshimiwa Dr. Diodorus B. Kamala, kuhusu Uwanja wa Ndege wa kule Bukoba. Nilitaka tu kujua, kwa nini katika eneo la Mkoa wa Dodoma hakuna usafiri wa abiria wa ndege? (*Makofi*)

**SPIKA:** Ni swali jipya lakini kama una majibu, nasema ni swali jipya lakini kama Mheshimiwa Naibu Waziri ana majibu ruksa kuyatoa.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kama mtakumbuka Waheshimiwa Wabunge hapo nyuma tulikuwa na huduma za ndege kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma. Huduma hizo zilisita kutokana na kukosa abiria baada ya barabara yetu kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma kuwa nzuri. Kwa hivyo watu wanaamua kuja kwa barabara badala ya kutumia ndege, kwa hivyo ndege zikawa haziji. Iwapo kutaonyesha kwamba bado watu wana kiu, Mashirika tayari tulishawaambia waone uwezekano wa kuanza huduma hizi hasa wakati huu wa kipindi ambacho Waheshimiwa Wabunge wako hapa wanaweza wakapata abiria. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yote yamejibiwa na muda wa maswali umekwisha. Sasa kuna matangazo mawili ya vikao vya leo kama ifuatavyo:-

Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje, anawatangazia Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo tarehe 28 Juni, 2005 kutakuwa na kikao kule *TAMISEMI* katika chumba cha Baraza la Mawaziri. Kamati hiyo itakutana na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mazungumzo ambayo yamepangwa mara baada ya kipindi hiki cha maswali. Kamati ya pili ni Kamati ya Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa Anne Makinda, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, anawatangazia Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo tarehe 28 Juni, 2005, saa 5 asubuhi kikao kitafanyika kwenye chumba cha Kamati Na. 219.

Mwisho wa matangazo ya vikao, ratiba ya leo ni kwamba mjadala wa jumla utaendelea mpaka mwisho wa kipindi cha asubuhi. Lakini tunampa nafasi Naibu Waziri wa Ujenzi ajibu hoja kabla hatujasitisha shughuli saa 7.00 mchana, ili tutakaporudi saa 11.00 jioni, Mheshimiwa mtoa hoja mwenyewe atahitimisha hoja yake na tutaendelea na hatua zilizobaki za kupitisha Bajeti ya Wizara hiyo. Mwisho wa matangazo.

#### **HOJA ZA SERIKALI**

#### **Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2005/2006 Wizara ya Ujenzi**

(Majadiliano yanaendelea)

**MHE. HAMAD R. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Kwanza niungane na wenzangu kutoa pole na rambirambi kwa wenzetu ambao wametangulia mbele ya haki, Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi Amina. Pia namuomba Mwenyezi Mungu atujalie na sisi atupe hatima tufika kwake salama.

Mheshimiwa Spika, pili naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi kwa kazi nzuri waliyoifanya na naomba tu wanisaidie ufafanuzi baadhi ya sehemu wakati atakapojibu hoja hizi.

Mheshimiwa Spika, kwanza katika ukurasa wa 114 wa hotuba yake ameonyesha katika kipindi cha mwaka 1995 mpaka 2005 tumejenga barabara zenye urefu wa kilomita 1,319.07. Sasa kwa kipindi cha miaka 10 maana yake tumejenga barabara kilomita 131.90 sasa ukiangalia mahitaji ya barabara nchi nzima, nakumbuka Katibu Mkuu alitambua mahitaji kamili ni kilomita 85,000. Sasa ukiangalia kwa utaratibu huo wa ujenzi katika kipindi cha miaka 10 kama tunajenga barabara kilomita mia moja thelathini na moja na *point*, ni dhahiri kwamba kilomita 85,000 itatuchukua zaidi ya miaka 100 kuweza kuzijenga. Sasa sina hakika kama mipango yetu ni mizuri ya kutuwezesha kwa kweli kupambana na tatizo la miundombinu ambalo hivi sasa linatukabili.

Mheshimiwa Spika, sasa ukichukua takwimu hizi na takwimu ambazo zimo ndani ya kitabu cha hali ya uchumi, utakuta mahitaji ya barabara yaliyoandikwa humu ni kama kilomita 28,891.72. Sasa kwanza nilitaka ufafanuzi mahitaji halisi ya nchi ya barabara ni kilomita ngapi? Kwa sababu hakuna hata kitabu kimoja kinachoelezea kwa usahihi.

Mheshimiwa Spika, hilo ni la kwanza, lakini la pili ni kwamba ukiangalia kitabu hiki vile vile utaona barabara zisizo na lami, na zilizojengwa kwa changarawe na kadhalika ni kama kilomita 18,629, sasa hizi takwimu kidogo zinatubabaisha ni kilomita 85,000 zinazohitajika katika nchi au ni 28,000? Kwa sababu Kitengo cha Mipango hapa kinaonyesha kama ni 28,000 tulitaka ufafanuzi wa hilo na kwamba kwa *speed* hii ambayo inajengwa ukichukua hiyo 28,000 maana yake ni asilimia 9.23 ndio tunajenga barabara. Kwa hiyo, ni dhahiri tatizo la miundombinu litaendelea kuwepo kwa muda mrefu na kwa maana hiyo kujikwamua kiuchumi na hasa kutekeleza ule mkakati wa MKUKUTA itakuwa ni nadharia tu si hali halisi, kwa sababu huu ujenzi wenyewe ni *slow* sana.

Mheshimiwa Spika, pia nafikiri kwamba Wizara ingejitahidi vile vile kutuonyesha katika kitabu hiki, haituonyeshi ni madaraja mangapi hasa yanahitajika katika Tanzania. Lakini utaona takwimu tu za madaraja yaliyojengwa, sasa kidogo hili haitupi kipimo sahihi, kipimo sahihi tungeambiwa madaraja ambayo yanahitajika kwa kujengwa ni haya na tuliyoyajenga ni haya. Hiyo ingetusaidia sana kutupima ufanisi wetu katika utendaji wa kazi.

Mheshimiwa Spika, la tatu katika hilo ni kwamba ile *performance* na *value for money* katika ujenzi nayo ni kasoro moja kubwa ambayo ipo katika ujenzi wa barabara.

Hili tumelizungumza hata kwenye Kamati ya *Public Accounts Committee* pamoja na *Accounting Officer* kwamba ipo kasoro ya *value for money* katika ujenzi wa barabara na ndio maana barabara inamalizika siku mbili tatu halafu inaharibika.

Mheshimiwa Spika, hilo lilikuwa la kwanza nikitaka atusaidie ufafanuzi. La pili ambalo ningependa ufafanuzi ni kwamba Serikali iliamua kuwa Makao Makuu ya Serikali ni Dodoma. Nakumbuka mwaka 1984 hata mimi nilikuwa mjumbe katika Kamati ya Mheshimiwa Adam Sapi ambaye ni Marehemu sasa, ya kuendeleza Makao Makuu ya Dodoma.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia ujenzi unaofanywa Dar es Salaam wa kupanua maofisi na nyumba zinazojengwa za watumishi wa Dar es Salaam zinalingana hasa kwamba Dar es Salaam bado ni Makao Makuu ya Serikali. Ukiangalia nyumba zinazojengwa Dodoma ambazo ni sawasawa na makambi ya wakimbizi, hazielekei kama kweli tuna nia ya kuhamia Dodoma kama Makao Makuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri tungepata *clear statement from the Government* kwamba je, tumeamua Dar es Salaam ibaki Makao Makuu ya Serikali na Shughuli za Bunge tu zifanyike Dodoma, au tumeamua hasa Dodoma iwe Makao Makuu? Kama ni Makao Makuu yake yawe Dodoma? Kwa nini miradi mizito ya kupanua ofisi, majengo ya ofisi, Wizara ya Ardhi inapanuliwa, Sayansi na Teknolojia na nyingi tu na majengo ya wafanyakazi makubwa makubwa yanajengwa Dar es Salaam. Lakini Dodoma hakuonekani kabisa kama kuna shughuli za Serikali katika kuhamia Dodoma ukiacha Mheshimiwa Spika yeye mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, hilo tungepata ufafanuzi, lakini lingine katika hili ni utumiaji wa rasilimali. Waziri wa Fedha ametuambia kutokana na utaratibu wa *Cash Budget* tumeweza kutumia vizuri sana pesa zetu. Lakini unaweza ukatumia pesa vizuri, yaani kwa kiwango chako kile ulichopata ukanunua pombe ikakuwa na mwingine pesa ile ile akainunulia chakula akasaidia watoto, hakuvuka *ceilings*. Lakini matumizi ya huyo aliyekunwa pombe akauwa watoto na huyo aliyenunua chakula inakuwa tofauti, sasa inaelekea hatuna matumizi mazuri ya fedha. Kama tuna matumizi mazuri ya fedha tusingeweza kujenga miji miwili wakati mmoja, tunajenga Dar es Salaam wakati huo huo tunajenga Dodoma, haiwezekani. Kwa hiyo, hakuna matumizi mazuri ya fedha za umma na hili nafikiri ni moja kati ya ambalo lingekaa Serikali ikatupa maelezo, ni kwa nini tunaendelea kujenga Dar es Salaam wakati tumeamua kuhamia Dodoma? Kama Serikali inabadilisha sera si vibaya watueleze tu, kama vile ambavyo sasa hivi wamekubali kwamba ile miundombinu iliyobaki ya Serikali, kwamba Serikali haitauza hisa zake zote kwenye Mashirika yale ambayo bado hayajabinafsisha.

Mheshimiwa Spika, ni mawazo mazuri tuliyatoa hapa katika Bunge, Wabunge wengi kwa hivyo kama Serikali imepokea na hili basi lipokee, tubaki Makao Makuu Bunge Dodoma na ibaki Serikali Dar es Salaam tuendeshe shughuli. Lakini haionekani kama kweli kuna *seriousness* katika kuhamia Dodoma, hilo lilikuwa la tatu.

Mheshimiwa Spika, hilo lilikuwa la tatu, la nne wakati Serikali imeamua kuuza nyumba za Serikali kulikuwa kumetengenezwa Mkataba kwa bahati mbaya huo Mkataba ukawa na kasoro. Sasa mimi nataka kuiuliza Serikali, hivi Serikali katika kipindi cha miaka 40 haijui kutengeneza mkataba wa kuuziana mali? Maana alipokuja Afisa Mhasibu kwenye Kamati tulimuuliza kwa nini mkataba wa kwanza ulikuwa na kasoro akasema kulitokea makosa. Sasa mimi nafikiri ndio tunataka tueleze, kasoro gani kwanza ilitokea katika mkataba wa kwanza mimi sitaki nielezee hapo atuambie Waziri. Kwa nini baadaye mkaandika mkataba wa pili? Lakini kubwa ni kwamba Serikali inauza nyumba huku inajenga nyumba *contradiction* kidogo mimi nataka ufafanuzi zaidi.

Mheshimiwa Spika, pili tunayo *Procurement Acts* ambayo inataka mali zote za Serikali ziuzwe kwa utaratibu huo, kwa nini haiukufuatwa hiyo? na hilo nafikiri tungepata ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, jingine ambalo ningetaka kusadia Serikali sasa, ni namna gani ya kujikwamua katika hili la barabara. Hivi sasa yako makampuni makubwa Duniani ambayo yana mitaji mikubwa ya fedha na ambayo yanatoa mikopo ya muda mrefu miaka 10. Ukichukua Bajeti hii tuliyonayo ukaifanya kama ni asilimia 15 ya *down payments* na wao wakatoa asilimia 85, unaweza ukapata wastani wa dola 1.4 bilioni. Kwa hiyo ukitumia hiyo *theory* ambayo nimeisema na bahati nzuri taarifa hii tayari Waziri wa Fedha anayo. Kwa hiyo nafikiri tukitumia utaratibu huo tunaweza kujenga wastani wa kilomita kama 3,000 mpaka 4,000 kwa mwaka kwa kutumia utaratibu huo. Sasa mimi nilifikiria labda huo ungekuwa utaratibu bora zaidi wa kuweza kutukwamua hapa tulipo badala ya kutumia huu utaratibu wa sasa ambao tunaujenga hivi sasa, hatuwezi kuondokana na tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, la mwisho sina maneno mengi sana lakini nilikuwa nataka tu kupata ufafanuzi kwa Waziri ni kwamba, kuna viongozi wengi wa Kitaifa ambao bado wanakaa kwenye mahoteli na Serikali inagharimika na imetokea hiyo baada hizi nyumba za Serikali kuuzwa. Labda tungefahamishwa sasa hivi ni kiasi gani Serikali inatumia kwa viongozi hao wanaokaa kwenye nyumba za Serikali wako pale Morogoro viongozi wa Usalama wa Taifa wengine bado wanakaa mahotelini hawajapata nyumba na kadhalika. Kwa hiyo, tungepata maelezo ya Serikali ni kiasi gani cha gharama za kukaa hoteli viongozi hawa baada ya kukosa nyumba kwa zile sehemu ambazo nyumba za Serikali zimeuzwa.

Mheshimiwa Spika, sina matatizo na hoja ya Waziri. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Spika na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika hoja ya Waziri wa Ujenzi. Lakini kabla ya yote nichukue nafasi hii kutoa salamu zangu za rambirambi kwa wananchi wa Jimbo la Kilombero kwa kufiwa na Mbunge wao mpendwa ndugu yetu Hayati Abu Kiwanga. Pia nitoe salaamu za rambirambi kwa wananchi wa Mkoa wa Rukwa kwa kufiwa na Mbunge wao mpendwa wa Viti Maalum Mheshimiwa Margareth J. Bwana ambaye kifo chake kimetupa mshtuko mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na salamu za rambirambi hizi nichukue nafasi nyingine kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu *Engineer* Kijazi

kwa kazi nzuri wanayofanya katika Wizara ya Ujenzi katika nchi yetu hii ya Tanzania. Nawapongezeni sana na hongereni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwapongeza napenda kuchangia katika hotuba ya Waziri wa Ujenzi sehemu kubwa tatu. Ya kwanza sehemu inayohusu ujenzi wa barabara za Kitafa. Mheshimiwa Waziri ametupa taarifa katika kitabu chake hiki cha ujenzi wa barabara mpya ambazo zimejengwa katika kipindi hiki cha mwaka huu wa fedha unaokwisha na barabara ambazo anatarajia kuzijenga katika kipindi cha mwaka huu wa fedha ambao anaomba fedha. Mipango yake yote aliyofanya na ambayo anataka kufanya ni mizuri sana. Lakini nipende kumpa changamoto kwamba kwa sababu barabara ni msingi mkubwa wa uchumi wa nchi, itakuwa vizuri katika siku sijazo ninaamini kwamba yeye akiwepo au mwingine akiwepo atalikumbuka hilo kwamba angetupatia na *evaluation* na *economic impact* ya barabara hizi katika maeneo ambayo tumezijenga, ili barabara hizi zinapokuwa zinajengwa nchi iweze kujua kwamba barabara fulani imeweza kutoa mchango gani wa kiuchumi katika nchi yetu. Vinginevyo tutajikuta wakati mwingine tumejenga barabara ya mamilioni mengi ya fedha kumbe kwa *interest* ambayo si uchumi wa nchi bali kwa *interest* ya mtu au kikundi cha watu!

Mheshimiwa Spika, la pili ni kuhusu barabara za Mikoa. Barabara za Mikoa kiukweli Mheshimiwa Waziri amejitahidi sana kuzipangia mafungu ya fedha. Lakini kuna kitu kimoja ambacho mimi kinanipa shida, zile barabara tunazipelekea fedha kila mwaka, tunazifanyia *periodic maintenance*, *spot improvement* sijui ni nini.

Lakini kila mvua inaponyesha barabara zile zinapata adha kubwa sana, ni kama tumeweka fedha zikasombwa. Ningemuomba Mheshimiwa Waziri ahakikishe kwamba ndugu zetu hawa wa *TANROAD* ambao wako Mikoani wanajitahidi sana. Lakini ili kuzilinda zile barabara zifanyiwe *drainage* na ziwe na makalvati, sehemu nyingi barabara hizi zinatengenezwa hazina *drainage*, wanakuja wanaburuza buldoza wakishapita kama ni kipindi cha mvua mwezi mmoja tu wananchi ni kama hawakuwa na barabara wanajiuliza maswali mengi sana. Serikali imetumia milioni labda 90 au 200 lakini baada ya muda mfupi fedha zote zimesombwa na zimepelekwa baharini.

Nakuomba Mheshimiwa Waziri kwa ujasiri wako na umakini wako hili ukaliangalie, mahali unapoweka fedha ya Serikali kwa barabara vile vile uhakikishe unailinda sawasawa na mtu aliyeweka fedha katika *self*. Tunapopeleka shilingi milioni 200 katika barabara ya Mkoa ni kwa sababu umekwenda kuwekeza zile fedha ziweze kuwasaidia wananchi.

Lakini kama barabara ile imetengenezwa baada ya muda mfupi barabara ile tena haipo wananchi wanajiuliza maswali mengi sana. Pamoja na hilo, barabara hizi za Mikoa sehemu nyingi ni za udongo, sijui sera ya Wizara ni ipi kwamba barabara ya Mkoa iwe ya changarawe ama ya udongo. Kule kwangu barabara nilizonazo zote ni za udongo ukiangalia barabara ya Halmashauri ambayo kwa kiwango chake ingekuwa na kiwango cha chini na ukiangalia barabara ya Mkoa utaona kama hazina tofauti, zote ni za udongo. Sasa tungeomba barabara hizi za Mkoa hadhi yake iwe kubwa kidogo ili hizi barabara wananchi waone zina mkono wa Serikali kuu zisionekane kama zile za Halmashauri.



Mheshimiwa Spika, lingine kuhusu barabara zetu kule Same, niliongelee kidogo. Barabara za Mkoa kiukweli tuna barabara moja ya kutoka Same kwenda Mkomazi kupitia Kisiwani na Gonja. Barabara ile imekuwa na hali mbaya sana kwa miaka mingi Wananchi wanapata adha na mara nyingi wakati wa mvua haipitiki kabisa. Mheshimiwa amejitahidi kuifanyia matengenezo ya mara kwa mara na kila mara imetumia fedha nyingi sana.

Nakumbuka katika mwaka wa fedha uliopita alitoa karibu shilingi milioni 70, lakini zile fedha hazikuweza kufanya chochote ile barabara bado ina hali mbaya mpaka nikafikiri kwa nini Wizara isifikirie kuijenga vizuri kwa vipande vipande (*peace work*), na sehemu nyingine ikafanya matengenezo ya kawaida na hatimaye wakaweza kuwa na barabara ya changarawe nzuri.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa tunategemea Mbuga ya Mkomazi Umba ambayo inachukua sehemu ya Wilaya ya Mwanga, Same na Lushoto na Korogwe, mbuga ile kuwa Hifadhi ya Taifa. Hivi sasa kuna watalii wengi wanaingia katika ile mbuga.

Lakini mara nyingi wanakwamishwa na barabara, sasa watalii wanajenga uchumi wa nchi wanatuongezea pato la Taifa, ni kwa nini barabara ile inakuwa ni kikwazo kwa watalii kule Same, Korogwe, Lushoto na Mwanga. Hizo ni wilaya karibu nne ambayo ni Mkoa mzima, kwa hiyo ningemwomba Mheshimiwa Waziri anapoitengea fedha hii barabara ajue ni barabara ambayo iko katika eneo la uchumi, eneo la kupatia Taifa letu ongezeko la pato la Taifa. Kwa hiyo, ninamwomba sana barabara hii pesa aliyoitengea safari hii ni kidogo mno na Mheshimiwa Rais alipotembelea Same nakumbuka aliwaahidi wananchi wa Same kwamba, kwa sababu wamechimba barabara asilimia 90 kwa mikono yao wenyewe bila msaada wa Serikali na ninashukuru hili kalisema Mheshimiwa Anne Kilango kwamba Serikali itafikiria kuongeza fungu la barabara kule Same kwa wananchi wa milimani.

Sasa leo nikiangalia katika kitabu hiki sioni tofauti ya mwaka huu wa fedha uliopita na mwaka huu wa fedha. Ni kama ndugu yangu John Magufuli na ujasiri wake anarudufisha yale yale ya mwaka jana, kwamba kama iko tofauti ni kidogo sana. Mimi ningependa nifahamu Rais aliahidi ujenzi wa barabara ile ya kutoka pale Makanya mpaka Same amepeleka fedha nashukuru sana, naishukuru Wizara yako.

Lakini ongezeko la kuchangia barabara zote za Same hakuna tofauti ya mwaka wa fedha unakwisha na huu unaoanza. Ningekuomba sana Mheshimiwa Waziri ukaliangalie hii ni ahadi Rais aliitoa na kipindi chake kinakwisha huyu Baba kafanya kazi kubwa sana ya kujenga uchumi wetu na hakuna sababu gani akaondoka huku watu wengine wakilalama kwamba tuliahidiwa hiki hatukupata. Pamoja na kwamba Serikali iko pale pale, lakini tungeomba ahadi zake zile ambazo amewapa wananchi tuweze kuzikamilisha.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ya barabara za Mikoa niweze kuongelea suala la nyumba za Serikali. Mimi sina mgogoro wa nyumba za Serikali zikiuzwa, sawasawa na mtu ambaye ana ng'ombe yake anaamua kuiuza huwezi

ukamuuliza kwa nini unaiuza. Lakini vile vile lazima ukaangalie anauza ng'ombe huyu kwa sababu wameongezeka ama ng'ombe ni yule yule mmoja?

Sasa kama ng'ombe ni yule yule mmoja halafu unauza mimi inanipa shida, sina mgogoro kabisa na uuzaji wa nyumba za Serikali. Lakini mimi nafikiri hatukufanya maandalizi mazuri, tunauza nyumba huku tunawapangishia watu nyumba hii maana yake nini? Tena kwa mamilioni ya fedha. (*Makofi*)

Tulisema kuna nyumba ambazo ziko katika maeneo *prime* na nyumba za viongozi kama vile Mawaziri, Makatibu Wakuu, Majaji *Osterbay*, Msasani zile zingebaki za viongozi lakini zote hizi zimeuzwa. Hatukufanya maandalizi ya kuwa na nyumba zingine kama hizi, tumekuwa kama mtu ambaye ana mifugo yake halafu anaamua kuuza yote kwa mfano uleulewa ng'ombe niliokuwa naongea. Wakija wanya atawaweka wapi? Na zizi hana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi inanipa shida sana, sasa viongozi hao wanaokuja inabidi wapangishiwe nyumba. Kule Same Mkurugenzi wangu imebidi apangishiwe nyumba, kwanza alikaa hotelini baadaye wakamtafutia nyumba ya kupanga kwa sababu nyumba iliyokuwepo ameuziwa Mkurugenzi aliyekuwepo na ameondoka.

Sasa Mheshimiwa Waziri hili ukaliangalie hatukufanya maandalizi, kama hatukufanya maandalizi sasa haya mapungufu yaliyotokea tunayakabili vipi? Kitabu chako hiki hakituelezi mapungufu yaliyopo. Mimi ningependa Serikali ambayo imefanya mema tunaipongeza sana na hongereni sana. Lakini mapungufu yanapokuwepo vile vile tuyakabili, hatuwezi kuongelea mazuri siku zote na mabaya lazima tuyaongelee ndio maana wanadamu tunaishi na tunakufa. Kwa hiyo ningekuomba sana Mheshimiwa hili la nyumba ukaliangalie kwamba hivi sasa watu wanalipiwa mafedha mengi kwenye mahoteli na ni fedha ya Serikali. Vinginevyo utakuwa unafanya mambo mazuri lakini ndani ya vicious *circle*.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni jinsi nyumba hizi zilivyouzwa, kiubaguzi baguzi nani wanauziwa? Mimi ni Mkurugenzi wa *STAMICO* kuna nyumba za *STAMICO* zinauzwa na nikaomba na mimi niuziwe, nikaambiwa wewe hapana kwa sababu wewe mwanasiasa, wewe ni Mbunge ukiwa mwanasiasa wewe ni dhambi?

Sasa tunataka kujua nani wanauziwa hizi nyumba? Kunakuwa na vikwazo vingi sana. Watendaji wale wameuziwa nyumba sisi ambao ni Wakurugenzi wa ile Bodi tumeambiwa nyumba hapana zimerudishwa Serikalini, zimerudishwa kwa Mheshimiwa John Magufuli. Sasa Mheshimiwa John Magufuli mimi sielewi kabisa hii nyumba nimenyimwa nyimwaje na wengine wamepata pataje? Ningependa kufahamu leo zinapatikanaje, zinakosekanaje? Na Wabunge wote wafahamu ili pale ambapo zipo tukaziombe na sisi tuuziwe.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa ni kuhusu walimu. Hawa wafanyakazi wengine wote wanauziwa nyumba, hivi walimu siyo wafanyakazi? Za kwao haziuzwi kwa sababu gani? Hivi za kwao si za Serikali hazikuchakaa? Na wao hawajengewi nyumba? Na kama wanajengewa nyumba mpya na wao wauziwe na kama kuna taratibu

zingine zitafutwe ili nao wajisikie kwamba hizi nyumba za Serikali zinapouzwa kwa wafanyakazi nao wana sehemu yao ndani ya Serikali yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ningomba sana kwa sababu Serikali yetu ni ya uwazi na ukweli (*transparent*), tuweze kupata majibu na kufahamu haya mapungufu tutayakabili vipi?

Baada ya hayo nichukue nafasi ya mwisho kumpongeza Mheshimiwa Ndugu yangu John Magufuli na Naibu wake na Katibu wake Mkuu na watendaji wote wa Wizara ya Ujenzi kwa kazi nzuri wanayofanya na mimi naunga hoja yake mkono asilimia mia moja, lakini tupate majibu. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. KILONTSI M.M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii. Naomba na mimi niungane na wenzangu kutoa rambirambi kwa familia ya Marehemu Margareth J. Bwana aliyetutoka hivi karibuni. Ninamwomba Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi Amina.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba na mimi kutoa mchango wangu juu ya hotuba hii na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi kwa kazi nzuri ambayo amekuwa anaifanya toka ameingia Serikalini mwaka wa 1995 na mwaka wa 2000 akachaguliwa kuishika Wizara hiyo.

Mimi nampongeza sana, maana wengi tumekuwa tunaona jitihada zake za kufanya kazi katika Wizara hii. Nampongeza sana Mheshimiwa John Magufuli, nampongeza sana mzee wangu Hamza na ninawapongeza viongozi wote wakubwa wa Wizara ile ikiwa pamoja na Katibu Mkuu, hongereni sana kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi leo katika nchi hii mtandao mzima wa barabara uko *defined*? Mimi labda niseme kwamba ndani ya Chama kinachoongoza Serikali hii, sisi tumekuwa watu wa kujikosa pale tunapofanya makosa. Waheshimiwa Wabunge ambao tumekuwa tunazungumza humu ndani, nia yetu ni njema tu *because we all have a stake in the development of this country*. Kwa sababu hiyo, ni lazima tuzungumzie yale maneno muhimu na ya maana zaidi yanayoweza kutuletea maendeleo au kuharakisha maendeleo ya Taifa letu. Kwa hiyo, hakuna mtu anayezungumza habari ya barabara au habari ya kitu kingine humu ndani ambaye nia yake ni mbaya, nia ni kuendeleza, nia ni kuleta ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ninaomba jambo hili lieleweke kwa sababu wengine wamekuwa wanafikiri kwamba kuna Mbunge anakuja humu ndani na anazungumza kumlenga Waziri fulani. La hash! Wote tunapenda maendeleo ya Taifa hili na kwa

sababu tunapenda maendeleo ya Taifa hili ni vema tuyazungumzie yale yaliyo ya maana kwa Watanzania waliotuleta humu ndani ambao ni wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, humu ndani tumekuwa tunapigia kelele sana barabara za Magharibi. Ukijenga barabara miezi sita zimeharibika. Mvua zinazonyesha Magharibi tukubali ni nyingi kuliko sehemu nyingine yoyote. Kwa hiyo, barabara inakuwa *washed away*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, barabara ya Nyakanazi - Kigoma ilijengwa kwa zaidi ya shilingi bilioni sita lakini baada ya miezi sita ilikuwa inahitaji matengenezo tena kwa sababu ilikuwa imeshaharibika, madaraja mengine yameporomoka kwa sababu ya mafuruko. Kwa hiyo barabara ile imekuwa bado ni barabara ya matatizo na barabara nyingine ndani ya Mkoa huo.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia *generally* ukitoka Mkoa wa Kigoma ukaja Mkoa wa Rukwa ukaja Mkoa wa Tabora bado utaratibu wa maendeleo ya barabara ni mdogo sana na haukidhi matarajio ya wananchi toka walipoichagua Serikali ya Awamu ya Tatu mwaka 1995. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, labda nianze, Rais anapotoa ahadi mahali fulani na ile ahadi isitekelezwe, wananchi wanavunjika moyo. Mwaka 1995 wakati Rais wetu, mpendwa wetu Rais Mkapa alipokuja Kasulu alisema maneno yafuatayo. “Ninawaahidini Waheshimiwa wananchi nitakapokuwa nimechukua madaraka, mkisikia umeme unawaka Masasi na Kasulu umeme utawaka.” Watu wakapiga Makofi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, alipotembea Mkoa mzima akasema “Nawaahidini wananchi....

(*Hapa umeme ulikatika*)

**WABUNGE FULANI:** Kumekucha. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. KILONTSI M. M. MPOROGOMYI:** “Ninaahidi barabara yenu toka Kigoma – Tabora, nitahakikisha inajengwa”. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo hii barabara ile tunawekewa vipesa vya *spot improvement* na vingine vingine, tunashukuru hata kwa hilo. Maana binadamu ni anayeshukuru, tunashukuru hata kwa hiyo inayowekwa. Lakini ni vizuri barabara kama ile ambayo ingeweza ku-*stimulate production* katika Mkoa wa Kigoma na Mikoa mingine ingejengwa kisha wananchi wakaitumia kusafirisha mazao yao kutoka katika ule Mkoa. Hakuna anayebisha kwamba Mkoa wa Kigoma *is a very productive region* na kwamba kama sisi tungepatiwa barabara, tukaunganishwa na Mikoa ya Shinyanga na Kagera, tukaunganishwa na Mkoa wa Sumbawanga na Mkoa wa Tabora, watu wetu wangepanya biashara ya kusafirisha mazao yao ambayo hayana soko katika Mkoa wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninayasema haya kwa uhakika kabisa kwa sababu najua Rais alitamka. Sasa tunapokwenda sisi kule tunaulizwa, au ninyi Wabunge hamfuatili maana Rais akitamka jambo lake lazima litekelezwe itakuwaje mtu asitekeleze, nani yuko juu ya Rais tena asitekeleze agizo la Rais? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, siyasemi haya kwa ubaya bali nayasema kwa sababu yanazungumzwa kule Kigoma na si vizuri tukayaficha na yanazungumzwa sehemu nyingine lakini ukiangalia mtandao mzima wa barabara hiyo ya kutoka Tunduma – Sumbawanga – Mpanda – Uvinza – Kigoma halafu kwenda na hiyo ya Nyakanazi ambayo sasa imepewa ni *corridor* moja, tunashukuru kwamba ipo mikakati inayoendelea lakini tunaomba mikakati hiyo iendelee kweli. Watu wa Mkoa wa Kigoma wapate angalau barabara moja ya lami wajisikie kwamba na wao sasa wanaishi katika uhuru. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mwandiga – Manyovu, mwaka jana tuliambiwa mmetengewa shilingi milioni 400 zitajenga barabara ya Otasile ambayo itakuwa ni ya mfano. Tumekuwa tunasubiri, watu wanauliza sasa mbona haijajengwa, hatuioni zile shilingi milioni 400 sijui ziliende wapi. Barabara hii hadi leo ukitaka kusafiri, Waziri ameipita, barabara ile ni mbaya sana na *three quarters of the year*, barabara ile haipitiki. Leo watu wachache sana wanaoweza kupita katika barabara ile maana lazima uhakikishe gari yako ni nzima kweli.

Mheshimiwa Spika, humu katikati tunapozungumzia haya madaraja ya Munginya ambayo naona yametengewa pesa tunashukuru, mengi yamekatikatika au mengi unapita kwa tahadhari kubwa sana na ukiandesha kama *Fuso, you risk* kudumbukia ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa naona tumetengewa shilingi milioni 800, sijui hizo zitamaliza hiyo barabara au sijui hizo zitatengeneza udongo ule ule ambao unakuwa *washed away* mvua ikinyesha. Mimi naomba tufike mahali tutekeleze basi yale tunayoahidi, yakikamilika twende mbele.

Mheshimiwa Spika, kwenye barabara ya Kisili – Buhigwe kiko kijiji kimoja kinaitwa Nyamihanga. Nyamihanga sio Burundi ni nchini Tanzania. Nyamihanga wanapita kwenye mto mmoja mkubwa, watoto wao walikuwa hawasomi, kiongozi wanayemjua ni Mporogomyi hakuna kiongozi mwingine aliyewahi kufika pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, watoto wao lazima wavuke maji waende kusoma, ule mto ukifurika hamna kwenda kusoma. Wagonjwa lazima watoke kule waende Kigoma vijijini ndio kuna hospitali karibu na prisons kubwa ya Kwitanga.

Mheshimiwa Spika, nimezungumza na ma-*engineer*, mimi nina imani ma-*engineer* hawaendi kwenye Mkoa kukaa tu, wanaenda kwenye Mkoa kuangalia *infrastructure* iliyopo na jinsi wananchi wanavyoweza kuhudumiwa. Nimewaambia tafuteni au elezeni kwamba tunahitaji daraja hapa, mchunguze na watu waliokufa katika daraja lile, watu wamekufa kwenye mto ule. Nimeomba tujengewe daraja lile wale watu

angalau wasafiri kwa amani. Mimi mwenyewe ninapokwenda kule inabidi nivue viatu, suruali nikunje mpaka, sijui nisemeje? (*Kicheko*)

**MBUNGE FULANI:** Wawe wanavaa bukta. (*Kicheko*)

**MHE. KILONTSI M. M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Spika, nina imani Mheshimiwa Waziri, *you will be kind enough so as to allocate money* ili tujengewe daraja pale kuwasaidia wale Watanzania wenzako nao wafaidike na matunda ya uhuru wa nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kitu kingine, tuliomba barabara za ulinzi na usalama katika Mkoa huu wa Kigoma *and it is serious*. Ukitoka Kasulu unakwenda mpakani kupitia Muyama kule, unakwenda mpakani kupitia Jimbo la Magayane kule Buyungu au Jimbo la Mheshimiwa Ntagazwa kule Muhambwe, barabara ni mbaya sana, tukaomba hizi barabara zitengenezwe na tukaorodhesha, tukapeleka Wizarani. Tukaambiwa tutajibiwa lakini mpaka leo hatujasikia kitu wala sikuisikia katika mpango. Lakini Majimbo ya Kasulu Magharibi, Kasulu Mashariki, Buyungu na Muhambwe tunahitaji barabara za ulinzi na usalama *and that is a risk area* huwezi kupaacha hivi hivi! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hii *central corridor* ambayo inazungumzwa *has been so significant in the development of this country requires* kwamba sisi tunakuwa *focused*. Ie tunazungumza humu ndani hatutaniitani habari ya *economics of geography, it is so important and so crucial to the development of this country. Central corridor* iwe *properly defined*. Kama inakuwa Dodoma – Kigoma via Tabora, Kigoma ndio iwe *headquarter* za hiyo ili iweze ku-*tap* biashara za Rwanda, Burundi, Congo, Zambia tuweze kufanya biashara namna hiyo. *To be focused*, vinginevyo tunakwenda kwenda tu kwa Mungu nijalie, *we do a conglomeration of things which won't develop this country*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *quality* ya barabara zetu *is so bad* kwamba hata barabara za lami miezi sita *they are washed away*, lakini unaambiwa wamepata *clean certificate from where?*(*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Fedha.

**MHE. KILONTSI M. M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Spika, nasema hivi, sera ya nchi hii ya kubinafsisha na kutoa mali toka Serikalini, *requires* kwamba sisi sasa tusifanye biashara ya kujenga nyumba. *We don't need* hizi nyumba zinazojengwa na Serikali baada ya kubadilisha sera. Huwezi kujenga nyumba kama hizi zilizojengwa Dodoma kama watu ni manamba. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hili lazima tuseme. Si vizuri kuendelea kuanza kukodisha nyumba hapa, hii ni Serikali ifanye kazi ya Kiserikali ya kutengeneza sera na kusimamia mambo. *This is the policy* ambayo tunaizungumzia hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, watu wanapoizungumza wala hakuna anayemchukia Magufuli. Magufuli nakupongeza sana *you are so enthusiastic, you would like to see things developed but we are saying that the policy of this Government has completely changed, we now need a complete change in the outlook of doing things.* (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kama sera imebadilika tusijenge nyumba tukitaka wapeni hela hao wanaochaguliwa kwenye nafasi hizo wajenge nyumba zao, hata Wabunge msipewe nyumba, mzikatae mpewe pesa mjenge nyumba zenu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tusije humu ndani tukaanza kuomba nyumba, *no*, sio sera ya Serikali. *That is what he should be asking for.* (Makofi)

**WABUNGE FULANI:** *Yes.*

**MHE. KILONTSI M. M. MPOROGOMYI:** *We need a situation, we need a Government that is so focused, kwamba tunajua tunakokwenda vizuri zaidi sio katika hali ambayo ni ya kuchanganyikiwa kidogo, hapana. Kama mipango iwe defined, kama unasema unataka sijui Mtwara Corridor weka Mtwara Corridor tekeleza vizuri. Kama unasema Western Corridor weka Western Corridor focus na nchi nyingine kisha utajenga mipango madhubuti maana utakuwa na cha kufuata na utakwenda vizuri then utasimamia utumiaji wa fedha zile then you will have proper use of your finances and you can exercise control.*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. (Makofi)

**MHE. LYDIA T. BOMA:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Magufuli kwa taarifa yake pamoja na Naibu Waziri kwa kipindi chote tulichokuwa naye, kwa miaka mitano amekuwa akijitahidi kujibu maswali vizuri. Nimpongeze Katibu Mkuu na wafanyakazi wote kwa jitihada wanazozifanya katika kuweka hali nzuri ya Serikali kupitia ujenzi wa barabara. Nawatakia kila la kheri na waendeleo na taratibu hizo.

Mheshimiwa Spika, pia niwapongeze, Wizara imekuwa ikipanga ziara kwenda Mikoani. Mimi kama Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu, ni mmoja ambaye nilikuwa nakwenda, napenda niwashukuru kwa jinsi vijana wao waliokuwa wanawatuma hata wale wa kutoka Wizarani walivyokuwa makini katika kutuelekeza shughuli na tumeona mambo mengi. Isipokuwa ninalotaka kushauri katika ziara ni mambo mawili madogo tu kwamba wafanye ufuatiliaji wenyewe wa karibu kila mara kwa sababu makandarasi wetu wengine sio waaminifu wanajisahau. Pili, ni kwamba ratiba inapopangwa basi wahakikishe inatekelezwa kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, niungane na wenzangu kutoa pole kwa familia ya Mheshimiwa Margareth Bwana ambaye ametuacha hivi karibuni. Ninaomba Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi, amin.

Mheshimiwa Spika, ninataka kuzungumzia kuhusu barabara kwa sababu barabara ndio miundombinu ambayo Mtwara tunaikosa. Haya nimekuwa nikiongea wakati wote, inawezekana Wizara inaweza ikasema leo labda ana jambo jipya, kama ni barabara si alishaongea lakini kwa sababu barabara hazijawa katika hali ile ninayoitaka nalazimika kuzungumzia tena na tena katika siku zangu za uhai mpaka Bunge hili linapovunjika. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Sawasawa!

**MHE. LYDIA T. BOMA:** Mheshimiwa Spika, barabara ya kwanza ni ile ya kutoka Mtwara – Tandahimba – Nanyamba – Newala – Masasi na barabara kutoka Newala – Kitangari – Mtama. Barabara hii ni ya Mkoa. Katika barabara hizi mbili hali yake sio nzuri. Majibu ya humu ndani Bungeni Naibu amekuwa akinijibu tutafanya matengenezo madogo madogo, mimi nakataa. Ninayo sababu ya kukataa kwa sababu ile barabara ni ya Mkoa na wananchi wake ndio barabara wanayoitegemea kwa kusafirisha mazao, wagonjwa na ni barabara ambayo iko katikakati ya miji yote miwili kwa maana ya Makao Makuu ya Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la kuniambia kwamba tayari mna barabara ya *Mtwara Corridor*, nimesema na sasa narudia, nasema hivi unakotoka huko iliko barabara hii ambayo ni mbaya na mazao na mgonjwa uipite ile eti uifuate ya *Mtwara Corridor* ambayo wameweka pembezoni, sio kweli. Hatuwezi kwenda huko kusafirisha mazao barabara yake ni hii ambayo naizungumzia ambayo yenyewe bado haijajaliwa na Serikali ilisema itaweka lami barabara zile za Mikoa, Mkoa wa Mtwara tunahitaji lami tena ikiwezekana haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti hii bado nimeona taratibu ni zile zile. Je, ndani ya Tanzania hatujaona Mikoa ambayo tayari yote ina barabara za lami? Je, katika ndani ya Tanzania barabara nyingine za lami si ziko katika Makao Makuu ya Tarafa mpaka kwenye Kata? Kwa hiyo bado nina sababu ya kuililia barabara hii iwekwe lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niipongeze Wizara ya Ujenzi kwa jinsi ilivyosimamia barabara ya Kibiti – Lindi na ikahakikisha daraja lile linaisha na sisi wenyewe ni mashahidi kama Wajumbe wa Kamati kuona Daraja la Mkapa lilivyotengenezwa vizuri. Yote hii isingeweza kufanyika kama sio usimamizi mzuri wa Mheshimiwa Magufuli pamoja na timu yake lakini bado barabara hii ina utata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utata unatokana na sehemu zile korofi. Sehemu korofi zinamnyima uhuru mwananchi wa kutoka Mkoa wa Mtwara kuja Dar es Salaam wakati wa masika, hawezi kusafiri kwa wakati wake. Sehemu korofi tatizo ni nini? Labda Waziri atakaposimama aniambie. Je, ni wale makandarasi ndio wanafanya ukorofi wa kutengeneza barabara au je tatizo ni nini, ni fedha?



Mheshimiwa Spika, kama ni fedha hatuna njia nyingine ya kutafuta fedha? Kama ni makandarasi, kwa nini tusiwabadilisha tukawaweka wengine ili watekeleze azma ile tuliyokusudia kwamba barabara ile zitapita *taxi* kutoka Mwanza – Nangurukuru mpaka Mtwara? Sasa hivi hatuwezi kupita kwa *taxi* kwa sababu barabara ile bado haijakamilika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wananchi wamekuwa wanateseka, wanalala pale wiki mbili, tatu, wengine wanatoka wakiwa wagonjwa mahututi na ijapokuwa ninajua haipendezi lakini katika kushindwa nifanye na wananchi wa Mtwara wananipenda niliuliza je, Serikali imetenga fedha za kuwalipa wale fidia? Nadhani hili japokuwa litakuwa sio rahisi lakini mkae mfikirie sasa kwa sababu anateseka ambaye hausiki anayehusika huyo anawajibishwa vipi ili wananchi wale wasafiri kwa raha na wafike makao makuu kwa mujibu wa ratiba yao sawa na Mikoa mingine wanavyosafiri toka asubuhi kufika na kurudi makwao. Hilo nadhani Magufuli kwa usikivu wako umenisikia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Rais Mkapa. Rais Mkapa hatuna cha kumlipa Mungu mwenyewe atamlipa. Amefanya mambo mengi sana katika nchi hii. Ninalotaka kusema la karibuni ni ule msamaha wa madeni wa nchi 18 miongoni mwa ikiwemo Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninachosema zile za msamaha muangalie ikiwezekana basi mega kidogo mzipeleke kwenye barabara hizi ambazo zinazungumzwa ziwekwe lami. Tuna mambo mengi kwa mfano ujenzi wa shule, nini lakini hilo nalo linawezekana kwa kuangalia hali ya mazingira ya Mkoa ule kwamba unakosa miundombinu, tangu uhuru umepatikana mpaka leo bado mambo ni magumu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu *Mtwara Corridor*, nimeuliza swali la nyongeza leo ambalo kidogo limekuwa gumu kwa Serikali lakini sina jinsi ya kusema ni hivyo kwamba bado mimi binafsi nimeona mipango yake inasuasua. Ukiacha hii leo mipango ipo ambayo Mheshimiwa Waziri amesimama akanijibu lakini nataka niulize saini ya mkataba wa ujenzi au wa usimamizi wa maendeleo ya *Mtwara Corridor*...

(*Hapa umeme ulikatika*)

**WABUNGE FULANI:** Washa!

**MHE. LYDIA T. BOMA:** *Okay.*

Mheshimiwa Spika, tangu *Mtwara Corridor* mkataba ule umetiwa saini katika nchi zote mbili ni miaka mingi? Inawezekana mpaka sasa hivi kwa haraka haraka ni karibu miaka 40. Kwa hiyo, ninaposema kwamba *Mtwara Corridor* haiendi kwa uhakika, nina maana hiyo. Ninataka Serikali inielewe. Je, tatizo ni nini?

Mheshimiwa Spika, tuna barabara imekuwa ikizungumzwa kutoka Mtwara – *Mbamba Bay*. Imeshafanyiwa usanifu tayari na kila kitu tayari bado ujenzi haujaanza ni

kutokana na fedha nchi za nje hazipo au ile mikataba bado tunategemea nchi za nje? Kwa nini sasa Serikali isiamue kuanza kutengeneza ile barabara kwa fedha zetu sisi wenyewe kwa sababu bado tunazo barabara zingine ambazo Serikali imeanza au tunayo mipango mingine imeanza kutokana na fedha za ndani!

Sasa kwa nini hii barabara bado imesimama na hatuanzi na tunavyochelewa kuanza ndivyo tunavyochelewa na maendeleo yetu na ndivyo tunavyobaki sisi humu ndani inabidi tulalamike au bado hamuoni kuna umuhimu wa kufanya hivyo? Lakini tukisema, mimi nina ushahidi nimewahi kuambiwa kwamba Mkoa wa Mtwara mnapenda kulalamika. Nataka nikanushe hilo sio kulalamika tunaeleza ili haki itendeke. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika historia ya nchi hii hasa Mkoa wa Mtwara, nataka niwaeleze wananchi ambao pengine hawajui katika miaka ya huko nyuma kulikuwa na vita dhidi ya Tanzania na Msumbiji. Wananchi wa Mtwara ndio walioteseka. Kipindi kile tumepata matatizo sana kwa sababu ilikuwa lazima tuishi kwenye mahandaki, watu wengine wamekufa, watoto na wazazi wao wameteseka sana halafu tumekuwa na matatizo mengi tu.

Kipindi hicho Mkoa wa Mtwara ilikuwa kama wameweka barabara yaani sisi tuzuie vita tu kule tuendeleo na vita haikuvuka kuja Dar es Salaam wala Kaskazini. Kwa maana hiyo, hiyo ni moja ya sababu ambayo ametufanya sisi tumechelewa kuwa na maendeleo.

Serikali isingeweza kuja kule kuleta barabara, simu, maji, umeme, lakini ilikuwa inaleta kuanzia Dar es Salaam kwenda huko majuu huko Kaskazini, wapi, wapi kwa sababu kule hakupitiki kuna vita. Sasa leo mimi mwenyewe nimewahi kusikia mtu anasema hao wamechelewa wenyewe, wamazubazubaa, hivi kweli tumezuba?

**WABUNGE FULANI:** Eeeh. (*Makofi*)

**MHE. LYDIA T. BOMA:** Hivi Serikali inatungaliaje, inatushukuru vipi, inatupa pole vipi kutokana na mateso yale tuliyoyapata sisi ikiwa mpaka sasa hivi barabara zake hazipitiki? Ninapozungumzia kuhusu barabara nina maana hiyo nyingine kwamba hebu angalieni hawa walishapata shida.

Mheshimiwa Spika, katika Tanzania hii Mkoa mingine ikipigana kidogo tu barabara ikitetereka kidogo tayari Serikali inakimbia kwenda kutengeneza je na hizi barabara za Mkoa Mtwara? Tuna barabara ile ya mpakani ambayo ilikuwa inaweza kutoka mpaka kwenda Mbambabay tumeizungumzia mara nyingi kwamba itengenezwe mpaka sasa hivi bado haijatengenezwa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hilo nashauri Serikali iangalie jinsi gani wananchi hawa walivyokuwa wanateseka na jinsi gani leo Mbunge anapolalamika

anataka maendeleo yake angalau muone kwa sababu bado watu wengine walikuwa wanastarehe lakini sisi tuko kwenye mahandaki kwa kipindi chote kile. (*Makofi*)

**WABUNGE FULANI:** Naam!

**MHE. LYDIA T. BOMA:** Mheshimiwa Spika, katika kupitia taarifa, nataka niwapongeze kitengo cha wanawake. Nataka niseme kwamba wanawake katika nchi hii ya Tanzania ni wengi na ndio wazalishaji wa mazao mbalimbali na wanaleta pato kubwa kwa nchi hii na hao hao ndio wapiga kura wetu walio wengi na ni waaminifu, watiifu hasa wale wa kutoka Mkoa wa Mtwara. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, sasa wanasema Kampuni tatu zitaanzishwa Kilimanjaro. Mimi nauliza je, baada ya huko Mtwara mtakuja lini kwa sababu nataka hiyo Kampuni ije haraka sana iwezekanavyo Mtwara na ikiwezekana tunapomaliza Bunge hili la bajeti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, halafu niwapongeze pia mmesema kutakuwa na semina, hizo semina ninaomba nishirikishwe. Hilo ni ombi. Tangu nimeanza kuzungumza sijaleta ombi sasa hivi naleta ombi kwamba nishirikishwe katika semina hiyo kwa sababu mimi ninapata shida sana ndani ya Mkoa wangu katika vikundi karibu 220 vilivyopo ndani ya Mkoa ule ukianzia na kila Wilaya wanabangua korosho na wanafanya shughuli ndogo ndogo za kusuka vikapu au mikeka.

Wameniliza kuhusu uanzishaji wa shughuli za barabara maana wanasikia katika redio lakini leo kama nitashirikishwa kwenye semina hata kama Bunge hili sitakuwepo, ninaahidi nitajihidi kuzunguka kwa kujitolea kuwaelimisha wale wananchi wa Mkoa wa Mtwara hasa akina mama ili waweze kujikomboa kimaendeleo kutokana na hali ya kiuchumi. Kwa hiyo, sijui ni lini hizo semina lakini nimesoma katika taarifa hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumzia hayo machache...

**MBUNGE FULANI:** Makubwa.

**MHE. LYDIA T. BOMA:** Ninaendelea tena kumpongeza Waziri kwa kazi nzuri na wenzangu walikuwa wanasema aende ngazi ya juu, lakini mimi napenda aende ngazi ya juu je, atakapokwenda ngazi ya juu barabara atamwachia nani hasa hizi za Mtwara bado. Kwa hiyo ningepomba aendelee kubaki au labda atamfute mtu amrithishe na mkabidhi kuhakikisha zile barabara za Mtwara wanaweka lami haraka iwezekanavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, ninaomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

**MHE. SULEIMAN A. SADIQ:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nami naomba nianze kwa kusema naunga mkono hoja mia kwa mia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nami naomba niungane na wenzangu kwa msiba mkubwa uliotokea katika familia ya Mheshimiwa Margareth Bwana. Kwa kweli tulipokea taarifa hizo kwa majonzi makubwa lakini na sisi tunasema mwenzetu katangulia sisi tuko nyuma, tunachoomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi, amin.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Katibu Mkuu na wataalam wote wa Wizara ya Ujenzi kwa kazi kubwa wanayofanya katika suala zima la barabara na katika suala zima la kutengeneza hotuba hii ambayo kila mmoja wetu ameifurahia.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba nianze na barabara za mkoa. Barabara za mkoa sisi kama Wabunge tunaingia moja kwa moja kwenye vikao vya Bodi za Barabara za Mikoa, kule kwenye Bodi za barabara huwa tunaelezea matatizo ya barabara zetu, ni jinsi gani barabara zile zinahitaji matengenezo lakini taarifa tunazopewa ni kwamba sasa wenzetu wanapeleka Wizarani kwa kupata baraka na bajeti.

Mheshimiwa Spika, lakini ukija hapa kila mwaka unakuta mambo kwa kweli yanasuasua kwenye barabara za mikoa na mimi ningependa nipate taarifa kamili ya Mheshimiwa Waziri ni vigezo gani vinavyotumika katika kugawa fedha katika mkoa mmoja. Barabara moja ya mkoa inapata fedha nyingi barabara nyingine inapata fedha kidogo lakini barabara moja inapata fedha kila mwaka, mwaka huu wamepata 70, mwaka ujao 100, mwaka mwingine 150, ile nyingine kila mwaka inadumaa mimi naomba nitaje kabisa na barabara zenyewe na hali halisi.

Katika ukurasa wa 144 katika hotuba ya Waziri hapa tumezungumzia barabara za mikoa lakini kuna barabara ya mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mvomero – Ndole – Kibati. Hii barabara ni ya mkoa ina urefu wa kilomita 80, miaka mitano haikupata fedha, mwaka jana baada ya kumwomba Mheshimiwa Waziri akatusaidia tukapata milioni 40, mwaka huu tena nishukuru kwa hicho kidogo kilichotengwa cha milioni 40. Lakini wenzetu wa barabara zingine katika Wilaya zetu hizi hizi kila mwaka wanaongezewa, barabara ya Dutumi – Kolelo mwaka jana walipata 60 mwaka huu wameongezewa imekuwa 90. Barabara ya Dakawa – Bwakila mwaka jana walipata 50 mwaka huu wamepata 80, barabara ya Morogoro – Kisasi mwaka jana walipata 70 mwaka huu wamepata 100.

Sasa Mheshimiwa Waziri hii barabara ya Ndole ni mbaya kwelikweli na miaka mitano nyuma haikupata hata shilingi, mwaka jana kwa huruma yako ukatutengea milioni 40, mwaka huu tena 40 tunatengeneza kilomita nne katika kilomita 80 na mwaka jana

Mheshimiwa Waziri ulinipa ushirikiano na uliahidi ungetembelea barabara hii kwa kweli ni barabara inayounganisha kata mbili, kata zenye kilimo cha mazao ya biashara na chakula ni kata ambazo ziko pembezoni mwa Mkoa wa Morogoro ambazo zinaunganisha Mkoa ya Morogoro na Mkoa ya Tanga. Sasa Mheshimiwa Waziri pamoja na kazi nzuri lakini bado nikuombe kwa heshima na taadhima barabara hii uangalie. Ninazo barabara nyingi lakini barabara hii imesahauliwa kabisa na uliniahidi ukasema ukipata nafasi utatembelea. Mimi nikuombe bado kipindi kipo ukijaaliwa hata kesho twende ili ukashuhudie uone hali halisi ikoje.

Mimi langu ni hilo Mheshimiwa Waziri katika hili.

Mheshimiwa Spika, Lakini la pili nizungumzie barabara ambayo kuna kauli ya Serikali kupitia katika Bunge hili, barabara ya kutoka Handeni – Mziha – Magole. Mheshimiwa Waziri ulipokuja kufungua barabara na Mheshimiwa Rais pale Morogoro nilikuuliza kuhusu barabara hii ulinipa majibu mazuri sana, ukaniunganisha na Katibu Mkuu wako. Mwaka jana barabara hii ilitengewa fedha milioni 250 kwa ajili ya upimaji.

Mheshimiwa Spika, Lakini katika kikao hiki na katika hotuba yako hii hatujapata kauli yoyote ila nina matumaini niliposoma hotuba yako ukurasa wa 138 barabara hii imezungumziwa na ukurasa wa 128 tena imezungumziwa tena kwamba kuna fedha lakini tungependa tupate kauli ambayo na sisi tukawaeleze wananchi wetu. Kauli ambayo ipo sasa hivi ni kwamba barabara hii ipo katika mpango wa Serikali na mwaka jana fedha zimetengwa na mwaka huu fedha zimetengwa.

Mheshimiwa Spika, Lakini Mheshimiwa Waziri ajue barabara hii haitasaidia tu eneo moja, ni barabara itakayounganisha Bandari ya Tanga kupitia Handeni – Mziha kuunganisha Dumila hatimaye kuunganisha *Central Corridor* ambayo ndiyo barabara iliyokuwa ikipitika zamani na kwa sasa hivi kwa hali iliyopo na msongamano mkubwa kwa barabara ya Segera – Chalinze kwa kweli na sisi tunaoba barabara hii iwekwe katika mpango wa kitaifa ambao nina uhakika upo. Maelezo mengine zaidi Waziri anayafahamu hapa nafikiri sina sababu ya kueleza mengi lakini ningeomba nipate kauli yake katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, barabara nyingine ni ya kwenda Chuo Kikuu cha Mzumbe, inaitwa Sangasanga Mzumbe. Vyuho vikuu vyote katika nchi yetu vinabarabara ya lami, hii barabara mwaka jana ilitengewa milioni 250 tukaambiwa kazi ya upimaji ingeanza. Mwaka huu naona tena imetengewa fedha, nimetumwa na Uongozi wa Chuo Kikuu cha Mzumbe waliahidiwa kwamba kazi itaanza Julai Mosi mwaka huu. Ninaomba ahadi hiyo itekelezwe kwa vitendo na mipango yote ambayo imeandaliwa naomba basi iende kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nizungumzie masuala ya Barabara za Taifa. Kwanza nianze na daraja la Ruvu, hali ya daraja la Ruvu ni mbaya sisi watu wa Morogoro tunasafiri kila siku kuelekea Dar es salaam. Daraja lenyewe na ndani ya Daraja ile lami iliyopo imeanza kuchimbika na hali ile inatishia, sasa ningeomba kwa sababu ziko fedha zimetengwa basi kama mipango ipo ianze mapema tuliokoe daraja lile. Lile daraja kwa kweli lina hali mbaya, sisi wengine haichukui hata wili tunapita kwenye

daraja lile, ni daraja ambalo tunalitegemea kiuchumi katika Taifa letu. Mheshimiwa Waziri pamoja na kazi nzuri unayoifanya ninaomba na hili ulitolee maelezo ya kina ili sisi tujue nini kinachoendelea.

Mheshimiwa Spika, lingine naomba nizungumzie upande wa kazi kubwa inayofanywa na Wizara katika eneo la mizani. Tuna mzani unaounganisha Kibaha kazi ni nzuri, pale Morogoro eneo la Mikese wamejenga mzani, sawa. Lakini kuna eneo limesahaulika na eneo hilo sasa hivi ndiyo Wabunge wengi wanalalamika kwamba hiikazi ya barabara inaonekana kidogo siyo nzuri. Eneo ambalo limesahaulika ni Morogoro – Dodoma, sasa hivi eneo hili linahitajika mzani wa haraka ili kuiokoa barabara hii na kuiweka katika kiwango ambacho kitakuwa ni barabara ya kudumu. Kuna kazi kubwa sana inafanyika katika barabara hii. Ili barabara hii iwe ni ya kudumu suala la mzani linahitaji kupewa kipaumbele na ikiwezekana kauli itolewe katika Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri amefanya kazi kubwa sana ile mizani ya Mikese kwa kweli ilikuwa hakuna sababu kwa kipindi hiki. Kipindi hiki ilikuwa ni mizani moja katikati ya Dodoma – Morogoro ingesaidia, sasa hivi magari mengi yanaleta shehena kubwa hapa Dodoma kwa ajili ya kusafirisha kupeleka kwenye mikoa ya Kanda ya Ziwa na lipo tatizo kubwa sasa si vyema kulielezea lakini nafikiri wenzangu watakuwa wamenielewa vizuri sana.

Lingine ni barabara za Halmashauri. Ubora wa kazi katika barabara za Halmashauri ni duni kwelikweli. Halmashauri zinapata fedha nyingi kupitia TAMISEMI, lakini kazi zinazofanyika za barabara ndani ya Halmashauri yetu kwa kweli hairidhishi, Wizara kama Wizara inahitajika ikae na TAMISEMI tutoe ushauri na ikiwezekana jukumu hili tuwape wenzetu wa *TANROAD* aidha kusimamia au kushauri au kufuatilia. Barabara za vijijini zina hali mbaya lakini mimi nitoe mfano wa Halmashauri yetu ya Morogoro, Halmashauri yetu ya Morogoro tumeshasimamisha pale Wahandisi zaidi ya mara tatu, kila Mhandisi anayekuja ni tatizo, kila Mhandisi anayekuja ni tatizo. Sasa nimuombe sana huyu Askari wa Miamvuli kwa sababu amekaa pale na Naibu Waziri, na Naibu Waziri tuko pamoja kwenye hii Halmashauri atajua ukweli wa tatizo. Mimi ningeshauri Halmashauri za Wilaya zinapopata Fedha za Mfuko wa Barabara basi ni vyema sasa Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi tukarekebisha mtandao wa barabara hizi kwa kufuatilia hatua kwa hatua.

Tatizo la kwanza lililopo ni kwamba fedha zinazokwenda ni chache kwa hiyo hata utaratibu wa matengenezo unakuwa ni utaratibu wa ubabaishaji.

Tatizo la pili, kiwango cha kazi, hakuna mtu anayekwenda kukagua zaidi ya Mhandisi wa Wilaya. Sasa mimi ningeomba *TANROAD* kwa sababu wanafanya kazi nzuri na *TANROAD* Morogoro wamejitahidi kweli kweli wanafanya kazi nzuri na sisi kama Wabunge mimi upande wangu nina imani kubwa na *TANROAD* hususani Morogoro wamefanya kazi nzuri na mimi naomba ikiwezekana suala hili waachiwe *TANROAD*.

Mheshimiwa Spika, la mwisho. Sasa hivi barabara nyingi katika nchi yetu zimetengenezwa na nyingine zinaendela kutengenezwa na jambo ambalo linaonekana hata uongezeko wa magari umekuwa kwa kiasi kikubwa, msongamano umekuwa mkubwa katika Jiji la Dar es Salaam hususani saa za asubuhi kutoka Ubungo kuelekea katikati ya Jiji. Hili suala nafikiri limeshazungumzwa na juzi nimeona Naibu Waziri amejibu swali sasa naomba kupitia bajeti hii Mheshimiwa Waziri aweze kulieleza Bunge hili ni mipango gani inafanywa na Wizara katika kuangalia msongamano katika barabara zote za Jiji la Dar es Salaam nyakati za asubuhi na nyakati za jioni, wao kama Wizara wana Ma- *engineer*, wana wataalam wazuri sana wenzetu wa Kenya wanasifia Wizara yetu ya Ujenzi inafanya kazi kubwa sasa ni vema tukaliangalia Jiji la Dar es Salam katika sura ya kukua kwa uchumi na kukua kwa Jili letu.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kumuomba Waziri kwamba nimeagizwa na wananchi wa Jimbo la Sumve kwamba kuna kwamba kuna Barabara ya Ngudu – Malya nayo imesahauliwa muda mrefu kama inawezekana tupate maelezo ya barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. LUCAS L. SELELI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika hotuba ya Wizara ya Ujenzi. Lakini kabla ya hapo napenda kutoa salaamu za rambirambi kwa mwenzetu aliyetangulia mbele ya haki Mheshimiwa Margareth Bwana Mbunge wa Viti Maalum, Rukwa ni lazima tufarijiane kwamba sisi wote njia yetu ni hiyo hiyo. Bwana alitoa na Bwana ametwaa Jina lake libarikiwe. Amin.

Mheshimiwa Spika, Lakini la pili kabla sijasahau kwa kweli nianze kwa kuwapongeza wenzetu wa Wizara ya Ujenzi kwa kazi nzuri ambayo wameifanya na inaonekana na wananchi wanaiona lakini kwa kweli mnyonge mnyongeni haki yake mpeni. Kwa hiyo katika hilo napenda kuwapongeza Wizara ya Ujenzi wenyewe, Makatibu, Makamishna, Wakurugenzi wakiongozwa na Waziri pamoja na Naibu wake vilevile wenzetu wa *TANROAD* kwa kazi nzuri ambayo wameifanya ya kuiweka nchi iweze kuonekana kama inavyoonekana sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, hapo hapo katika pongezi nilikuwa napenda nitoe salaam zangu za shukrani kutoka kwa wananchi wa Jimbo langu la Nzega, Wilaya ya Nzega pia na Mkoa wa Tabora. Sisi katika ramani ya lami hatukuwemo kabisa tangu Dunia hii iumbwe lakini kwa kazi nzuri ambayo imefanywa pamoja na kuwa barabara za lami huwa hazipiti mjini sisi wananchi wa Nzega tunayo haki ya kufurahia kwa sababu pamoja na kwamba lami inapita *truck road highway* mbali na mji lakini leo hii lami imeingia Nzega Mjiji. Kwa hiyo, ni jambo la kushukuru sana kwa kazi nzuri ambayo imefanywa na Wizara hii.

Kasoro yake moja tu kwa sababu kila kitu huwa kina kasoro. Kasoro yake moja tu pale kwenye kona pale unapopita *highway* na kona ya kuingia mjini tumeipa jina la Magufuli. Magari yanaanguka sana pale na kwa hali hiyo nilikuwa napenda ifanyiwe marekebisho ili pawe na mzunguko na kwa kweli kwa heshima ambayo imefanyika kwa kazi nzuri chini ya Mheshimiwa Magufuli, mzunguko huo tumekubaliana uitwe Mzunguko wa Magufuli kwa hali hiyo nakuomba kabla hujakabidhi na kufungua hiyo barabara basi parekebishwe ili paweze kuwa pazuri pa kufanana na jinsi ambavyo kazi nzuri imefanywa ya Nzega - Shelui, Nzega – Tinde mpaka Shinyanga, Nzega – Tinde mpaka Isaka ambayo inafanywa na Makandarasi wa *GRAYNICA* na inatia moyo kweli.

Hapo hapo kwa niaba ya wananchi wa Nzega, mkoa ya Tabora na Shinyanga na Mwanza nilikuwa napenda ile kazi ambayo ilifanywa Mwanza mpaka Shinyanga na yenywe ianze kuangaliwa upya. Ile barabara sehemu za kabla ya kwenda Hungumalwa pameharibika sana hata baada ya Hungumalwa pameharibika sana kwa kweli hiyo kazi ingeweza kuangaliwa upya na nimeangalia katika hotuba yake hakuelezea tayari Mkandarasi ameshapatikana au kuna hatua gani za kuchukua kurekebisha aina hiyo. Lengo letu kwa kweli ni kutoka Nzega kwenda Mwanza mara moja na kurudi Nzega, unatoka Mwanza unakuja Nzega unakwenda Kahama bila matatizo kama katika maeneo mengine inavyofanyika.

Mheshimiwa Spika, Lakini vilevile katika hiyo hiyo pongezi nimpongeze kwa kazi nzuri ambayo tayari wameshatangaza barabara ya kutoka Shelui kwenda Singida na hasa pale Mlimani. Pamoja na kwamba itapita pembeni ya Mlima lakini nilikuwa napenda kwa sasa kwa sababu kazi bado paweze kufanyiwa matengenezo ili magari yaweze kuwahi kwa sababu pale mlimani Sekenke kuna uharibifu mno wa barabara. Nimeangalia katika vitabu vyake sikuona na nikakumbuka kwamba barabara inapokuwa chini ya Mkandarasi inakuwa chini ya matengenezo ya Mkandarasi lakini pale ni eneo gumu sana ambalo ningepomba Serikali yenyewe iweze kuingilia kati ili paweze kupitika kwa urahisi. Huo ulikuwa ni utangulizi tu kwa kazi ambayo wenzetu wameifanya. Kazi nzuri ambazo zinafanyika na Wizara hii zingekuwa nzuri zaidi iwapo Wizara hii ingeweza kutekeleza kama ambavyo imetenga kanda mbalimbali kwa kufuata jiografia. Zipo kanda ambazo zinaonekana kwenye maelezo yake ya kitabuni, Kanda za Mashariki, Kanda za Kaskazini, Kanda za Kati na kadhalika. Lakini mimi nilikuwa nataka kusemea Kanda hii ya Magharibi maana yake wamesema Kanda ya Kati katika mpango wao inapitia Nzega - Isaka – Shinyanga mpaka Mwanza na kuendelea.

Niseme Kanda hii ya Magharibi. Kanda ya Magharibi nikichukulia barabara kutoka Itigi kwenda Tabora, kwenda mpaka Kigoma. Na kanda ya Kati nikichukulia barabara ya kutoka Nzega, Tabora, Ipole kwenda mpaka Mpanda, Kanda hiyo hiyo nikichukulia kutoka Ipole kwenda Mbeya, hii barabara katika Maelezo ya Mheshimiwa Waziri bado imesahaulika kabisa. Amezungumzia usanifu na upembuzi katika barabara ya Itigi kwenda Kigoma peke yale na bado hakuelezea usanifu huo utamalizika lini, atakuwa tayari lini kutengeneza barabara iwe katika kiwango cha lami kwa kweli kwa jinsi ambavyo kazi ilivyofanyika katika maeneo mengine hapa kwenye Kanda hii ya Magharibi bado.

Mheshimiwa Spika, hii kanda ni muhimu mno, muhimu sana. Kama barabara hii itatengenezwa barabara ni kichocheo kikubwa sana katika kuibua uchumi na uchumi



katika maeneo hayo ya Magharibi kwa Mikoa ya Tabora, Mbeya, Sumbawanga na Kigoma ni jambo ambalo lipo na wala siyo suala la kufanyia usanifu wala upembuzi yakinifu, ni kitu kipo. Mbona Mheshimiwa Waziri katika maeneo mengine unatengeneza barabara bila kufanya usanifu na upembuzi yakinifu?

Leo tu katika mikoa hiyo ya Magharibi, mikoa ambayo siku zote mlikuwa mnatuita *sleeping giant* kwa kutucheleweshwa ninyi wenyewe leo mpaka ufanye upembuzi yakinifu, mbona maeneo mengime unafanya bila upembuzi yakinifu?

Mheshimiwa Spika, Ndugu yangu Mheshimiwa Waziri ningepomba hebu aonee imani maeneo haya ya Magharibi. Ni maeneo ambayo kwa kweli ukiangalia katika nyanja zote yameachwa nyuma hakuna barabara, hakuna umeme, hakuna maji ya uhakika.

Lakini ukiangalia kwa uzalishaji, angalia uzalishaji wa mazao kama Tumbaku, tumbaku Tanzania ni asilimia 75 mpaka 80 inatoka mikoa ya magharibi. Angalia uzalishaji wa pamba, mazao ya kilimo watu wa Sumbawanga wanakosa maeneo ya kuuza mazao yao kwa sababu hakuna barabara za uhakika.

Angalia Mkoa wa Kigoma ambao mimi ningedhani mkoa wa Kigoma baada ya bandari ya Dar es Salaam ukiachilia mbali bandari za Tanga na Mtwara, baada ya Bandari ya Dar es Salaam ingeweza kuwa ni kiungo kikubwa sana kwa kufanya biashara na nchi za jirani kwa kutumia Bandari ya Ujiji Kigoma. Lakini huwezi ukafanya biashara, huwezi kufanya biashara ya kiuchumi kama hauna barabara.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi nilikuwa nadhani jambo hili Mheshimiwa Waziri na Wizara yake na Wataalam wote pamoja na sifa ambazo anazipata hebu tuzingatie katika kuangalia uchumi wa kijiografia lakini vilevile uchumi wa kuweza kuteka nyara biashara katika maeneo ambayo yanatuzunguka.

Hatuwezi kungumzia uchumi kama hatuwezi kuwa na mpango wa kuteka nyara maeneo ambayo yanatuzunguka ya nchi nyingine za jirani, pale Kigoma unaweza ukafika Burundi, Rwanda, Congo na bado unaweza kufanya biashara na Zambia, kwa hali hiyo tunaweza kuibua uchumi na kuondoa umaskini katika maeneo yote ya Mikoa ya Magharibi mikoa ambayo inaweza kufanya biashara na nchi nyingine za Magharibi. Kuna wakulima wazuri sana ambao wanakosa soko kwa sababu soko linategemeana humuhumu ndani kwa ndani.

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa naomba barabara hizi ziwekewe kipaumbele na ziweze kujengwa kwa kweli kwa kiwango cha lami. Tunashukuru Serikali tulianza kujenga barabara ya kutoka Tabora kuja Itigi kwa pesa zetu za mkoa lakini tunashukuru Serikali ilitupa nguvu ikatusaidia angalau inaweza kupitika sasa hivi kwa 80% mpaka 90% kwa uhakika mwaka mzima.

Lakini barabara hizi za udongo, mimi huwa nawaambia watu wa Wizara ya Ujenzi kwamba Wizara yao ni ya barabara za udongo maana kila unapotaja unazungumza barabara za udongo wakisema sana ni barabara ni barabara za changarawe. Hizi barabara za udongo kweli ni rahisi kuzitengeneza ni rahisi sana kutengeneza, lakini vilevile ni rahisi sana kuharibika.

Hebu tuwe na mtazamo wa kuweka barabara za lami ambazo ni za uhakika pamoja na kwamba ni gharama kubwa lakini zinachukua muda mrefu na zinakuwa na uhakika zaidi wa kudumu kwa maisha ya kudumu na kufanya kazi nzuri, yakipita tu magari makubwa barabara zile zinaharibika, ikinyesha tu mvua barabara hizo zinaharibika haraka sana.

Kwa hali hiyo Mheshimiwa Waziri mimi nilikuwa napenda hii uweze kuitilima mkazo hasa barabara kutoka Itigi – Tabora kwenda Kigoma kutoka Nzega – Tabora kwenda Mbeya na Sumbawanga na hususan Daraja la Malagarasi.

Nashukuru kwa heshima ambayo Mheshimiwa Rais wetu Rais Mkapa amepata kwa kufungua daraja la Rufiji ambalo sasa hivi ni daraja la Mkapa, mimi ningetoa wazo kwamba awamu ijayo ya nne na ninaamini itakuwa ya Chama Cha Mapinduzi ambayo mgombea wetu Rais mtarajiwa Jakaya Kikwete mimi ningeomba katika kazi ya kwanza atakayoifanya ya madaraja basi daraja la Malagarasi liwe daraja la Kikwete, tukishindwa kutaja Kikwete basi tuliite daraja la JK.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataka kuunganisha na barabara hizi za vijijini. Kukiwa na barabara kubwa za lami za uhakika kama ambavyo juhudi zinafanywa na Serikali huwezi ukawa na barabara ambazo zina faida ya maana kama hauna barabara hizi za vijijini.

Mheshimiwa Waziri mara zote tukizungumzia barabara za Halmashauri anatuambia nendeni mkakae na Halmashauri zenu, mkazungumze na Halmashauri zenu kunzungumzia juu ya barabara za vijijini, Halmashauri zenyewe ndizo hizo hazina pesa sasa leo akijibu swali la nyongeza amesema toka mwaka 2001 Serikali ilikuwa inakaa kupitia mapitio kubadilisha sheria lakini ni kitu ambacho kingewezekana tu kama kweli wangukuwa makini kwa kuangalia kwamba barabara kuu haiwezi kuwa barabara yenye maana kama huna barabara ndogo zinazolisha barabara kuu.

Mimi ningependa kutoa mapendekezo kwamba katika mwaka huu au miaka ijayo ya fedha tuweze kuwekeza katika barabara za vijijini na hasa zile barabara zinazohudumiwa na Halmashauri zetu za Wilaya ambazo mara nyingi zinakuwa na pesa kidogo haziwezi kuzihudumia kwa uhakika.

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano. Ukiwa Tabora kuna barabara inaitwa Tabora – Mambali – Itobo, hiyo ni barabara kuu ya Mkoa, lakini barabara hiyo kuu ya mkoa imeishia Itobo tu wakati barabara hiyo hiyo inaendelea kutoka Itobo kwenda Mwangoye,

Mwaluzwilo kwenda Choma ambayo ni Wilaya nyingine ya Igunga. Wao *TANROAD* wanahudumia kutoka Tabora wanaishia Itobo wakati barabara hiyo inaendelea hadi Choma sasa mimi ningedhani kwa kujua ile ramani kwamba barabara hii inaendelea ingeweza kwenda moja kwa moja hadi Choma kwa kutumika kwa fedha za mkoa.

Mheshimiwa Spika, Mfano mwingine ni barabara ya kutoka Nzega kupitia Itobo kwenda Kahama pale Kagongo ile barabara iko kwenye barabara kuu lakini imekuwa hiyo barabara inayumbishwa kweli inahamishwa kila mwaka. Mara nyingine inapelekwa Shinyanga mara nyingine inapelekwa Tabora mara nyingine inapelekwa Halmashauri ya Nzega.

Sasa hebu tuwe na uhakika wa kitu cha kufanya unazungumzia barabara unatoka Nzega unakwenda Itobo leo unaambiwa kwamba hii barabara iko Mkoa wa Shinyanga. Kweli tuna nia ya kutengeneza barabara kuu ziwe nzuri, barabara ziwe za lami lakini bila kutengeneza barabara hizi za vijijini bado tutakuwa na mahangaiko kwa kuwezesha mazao, wananchi, mifugo na bidhaa mbalimbli kufikia barabara kuu zikafanyika kwa uzuri sana.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kutoa angalizo moja. Tumesema Dodoma ni Makao Mkuu ya nchi lakini kwa jinsi ambavyo nimeangalia inavyoelekea mimi ningomba tutamke waziwazi kwamba hapa Dodoma hapawezekani na Ndugu zetu wa Dodoma wangetusamehe katika hilo hapawezekani, mpende msipende hapawezekani.

Angalia *vote* ambayo imewekwa kuendeleza Makao Makuu, imewekwa jumla ya shilingi milioni 500 kuendeleza Makao Makuu, imewekwa shilingi milioni 500 tu kama kweli tungekuwa na nia ya kuhamia Dodoma tusingeweka chini ya hapo, tungeweka zaidi lakini kwa sababu haiwezekani basi tukubaliane kwamba haya mambo yameshindikana na kwa uwezo wetu hatuwezi.

Mheshimiwa Spika, ni kengele ya kwanza au ya pili?

**WABUNGE FULANI:** Hiyo ni kengele ya pili.

**MHE. LUCAS L. SELELI:** Mheshimiwa Spika, kwa haya machache nakushukuru. (*Kicheko*)

**MHE. MOHEMED A. ABDULAZIZ:** Mheshimiwa Spika, naomba na mimi nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, naomba na mimi niungane na wenzangu kutoa pole kwa familia ya Marehemu Margareth Bwana (Mbunge) ambaye ametutoka hivi karibuni. Kifo cha Margareth Bwana kimetia pengo kubwa katika Bunge letu lakini zaidi ni kwamba sisi tunaokaa upande huu kushoto kwako tunahofu zaidi kwa sababu katika Wabunge sita

waliokufa watano wametokea upande huu sasa kidogo inatupa wasiwasi kidogo, huenda mwakani tukirudi wengine tukahama upande huu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kuwashukuru Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri nimpongeze yeye Mheshimiwa Magufuli, Mheshimiwa Mwenegoha Naibu Waziri, Katibu Mkuu, *Engineer* Kijazi kwa kazi nzuri waliyoifanya kuandaa hotuba hii lakini siyo tu kwa kuandaa hotuba lakini vilevile kwa kazi nzuri ambayo Wizara inafanya kwa kipindi hiki cha miaka 10 ya awamu ya tatu.

Kwa maana hiyo basi naomba vilevile kumshukuru Mheshimiwa Mama Anna ambaye naye alikuwa Waziri katika Wizara hii katika kipindi cha miaka mitano ya kwanza ya utawala wa awamu ya tatu kwa sababu miradi mingi ni ile mipango endelevu ambayo pengine na yeye alishirikia kuianza kule nyuma.

Mheshimiwa Spika, naomba mimi nizungumzie katika maeneo machache tu nikianza na barabara ya Kibiti Lindi. Naomba nishukuru sana Wizara kwa kazi nzuri inayofanya katika ujenzi wa barabara ya Kibiti Lindi. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu naomba nishukuru Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi kwa hatua mbalimbali walizochukua kwa ujenzi wa barabara hii, tunawashukuru sana. Barabara haijakamilika lakini jitihada za kazi zinaonekana zinavyofanyika.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kuna maeneo machache ningomba niyazungumzie katika barabara hiyo. La kwanza ni eneo la Dar es Salaam - Kibiti. Eneo hili limefanyiwa matengenezo kwa muda mrefu sana sasa lakini *speed* yao ni ndogo sana, naiomba Wizara itupunguzie kero ile kwa sababu kero kutoka Kibiti mpaka pale Kimanzichana ambayo sasa hivi barabara imefika ni kero kubwa sana tunaomba Serikali iongeze jitihada ili eneo lile likabadilike mapema.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni kutoka Kivukoni mpaka Somanga. Katika miradi inayoendelea sasa hivi ni miradi ya Mingoyo, Mbwemkulu na Nangulukuru na eneo la Nangulukuru mpaka Somanga tayari limekamilika. Isipokuwa Somanga mpaka darajani ni eneo korofi ambalo bado hatujui mjenzi ni nani na itajengwa lini, nilikuwa naomba labda Mheshimiwa Waziri anijulishe mipango iliyopo ya Wizara katika eneo kutoka kivukoni pale Daraja la Mkaa mpaka Somanga ikoje na lini itatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusu wajibu wa wakandarasi wakati wa ujenzi wa barabara. Mwaka huu mwanzoni wasafiri wengi sana walikwama barabarani katika eneo kati ya Mbwemkuru na Nangurukuru na kuna baadhi ya wakati wakandarasi wanaojenga eneo lile walionekana kama vile wao hawahusiki sana na ubovu ule.

Naomba niwashukuru sana watendaji wa *TANROADS* Mkoa wa Lindi akina *Engineer* Chacha, kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuwaokoa wananchi ambao kwa kweli walipata shida kubwa pale njiani baada ya barabara kuwa mbaya katika eneo ambalo barabara imechepushwa ili kuruhusu ujenzi katika barabara ya zamani. Kwa hiyo, naomba Wizara iwakumbushe wakandarasi wao kwamba inapotokea vile, wao wana

wajibu mkubwa wa kuwasaidia wasafiri wanaokwama katika barabara wanazozitengeneza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu *speed* ya wakandarasi hasa katika eneo la Nangurukuru mpaka Mingoyo. Nianze kupongeza kwanza kazi ya madaraja, Kampuni iliyopewa ujenzi kutoka Lindi mpaka Mbwemkuru inafanya kazi nzuri sana kwa upande wa madaraja, ni mazuri na yanapendeza kuyaangalia na tunaamini ni imara vile vile, lakini *speed* ya ujenzi wa barabara ni ndogo, watu inawatia wasiwasi. Nilikuwa naomba Wizara kupitia kwa msimamizi nadhani ni *Engineer* Muyungu, ajaribu kuwasukuma zaidi wale wakandarasi wetu ili *speed* ya kazi yao iwe kubwa zaidi kuwajengea wananchi imani zaidi.

Mheshimiwa Spika, Awamu ya Tatu inamaliza muda wake katika miezi michache ijayo na kwa vyovyote vile kazi itakuwa haijamalizika. Bahati mbaya sina uwezo mkubwa, lakini mimi ningeomba waliopo waendele, watumilishie ile kazi, wasije kuja wanya wakasema hii habari sisi tumesahau, hatuijui. Tunaomba hawa wanaokuja wawakumbuke hawa waliopo ili na sisi tuweze kupata barabara nzuri kutoka Dar es Salaam mpaka Lindi-Mingoyo na baadaye Mtwara.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri na wataalam wake waendele kuwapitia wale wakandarasi na kuwatia nguvu ili waweze kufanya kazi kwa *speed* kubwa zaidi kuliko ilivyo sasa. Sielewi tatizo ni nini, sijui ni pesa au ni utendaji wao tu, nadhani Wizara inajua vizuri zaidi, ni vyema itusaidie katika eneo hili ili iweze kuwatoa wananchi mashaka.

Mheshimiwa Spika, vile vile katika mradi huo huo naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri, pale Lindi zipo nyumba zimejengwa pale Rasibura na nyingine zipo Mitwero pale kambi ya ujenzi wa wakandarasi. Nataka kujua zile nyumba kama Wizara ina hati ya viwanja vile au imeanza kuhakikisha kwamba inapata hati ya viwanja vile. Nadhani Mheshimiwa Waziri ananielewa ninapouliza hivyo. Nisingependa kuzungumza kwa kirefu zaidi, nina imani Mheshimiwa Waziri ananielewa kwamba tunaomba tuwe na hakika kama zile nyumba ni mali ya Wizara ya Ujenzi. Sasa je, mpaka sasa hivi wamechukua hatua gani ya kuhakikisha kwamba zile nyumba zinakuwa ni mali ya Wizara ya Ujenzi?

Mheshimiwa Spika, nilitaka kuzungumzia kuhusu suala la mizani. Mimi naunga mkono ujenzi wa mizani katika barabara zetu ili kuzitunza barabara zetu, lakini nina tatizo moja kuhusu mizani iliyopo Kibaha. Tatizo langu si kwamba utendaji ni mbovu, hapana, isipokuwa tatizo langu ni kuhusu magari ya mafuta, haya ya petroli yanayopimwa katika mizani ya Kibaha.

Mheshimiwa Spika, mafuta kwa kawaida hupakiwa sehemu moja kama ni *depot* yanapakiwa *depot* na sidhani kama kuna uwezekano wa kupakia mafuta mengine njiani. Mafuta ni kitu cha hatari, huweza yakaua watu na hata kusababisha hasara kubwa. Mimi nilidhani si busara kuweka magari ya mafuta pale kwenye *depot* ya mizani ya Kibaha. Kama inawezekana, nadhani Wizara ingefanya utaratibu wa kuweka mizani kule Dar es

Salaam kwenye *depot*, gari ikipakia ipimwe ikitoka pale iende moja kwa moja bila kupitia mizani mingine kwa sababu sidhani kama mtu anaweza kupakia mafuta sehemu nyingine njiani kwa sababu naogopa pale Kibaha ipo siku inaweza kutokea bahati mbaya, ukatokea moto mkubwa na tukashindwa kuudhibiti kwa sababu mafuta ni kitu cha hatari sana kuweka sehemu ambayo watu wake si waangalifu, huyu anavuta sigara, huyu anachoma korosho na mwingine anafanya hivi.

Mheshimiwa Spika, kusema ukweli inaweza kutokea hatari, kwa hiyo, naomba Wizara ifanye utaratibu wa kupima magari yale kule Dar es Salaam, vinginevyo basi ijenge mizani peke yake pembeni ambayo itakuwa inashughulika na mafuta peke yake na usalama mkubwa wa kudhibiti moto katika maeneo ya magari hayo yanapoegeywa. Huo ulikuwa ni ushauri wangu katika suala la mizani ya Kibaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nizungumzie suala la rushwa. Kwa muda mrefu wa nyuma maeneo mbalimbali ya Wizara ya Ujenzi yalikuwa yanatuhumiwa kwa rushwa. Lakini naomba nipongeze maeneo mawili ya Wizara ambayo yalikuwa yanatajwa tajwa, *TANROADS* na *CRB* (Bodi ya Wakandarasi). Maeneo haya kwa kweli yamefanya kazi nzuri sana na malalamiko dhidi ya rushwa katika maeneo haya mawili yamepungua sana. Naomba sana niwapongeze watendaji wote wa *CRB* na *TANROADS* katika Makao Makuu na hata katika Mikoa ya nchi yetu. Kwa kweli kwa kiasi kikubwa sana wameweza kupunguza malalamiko ya rushwa ambayo kwa kweli yalikuwa mengi, lakini sasa hivi inaonekana wamefanya kazi yao nzuri. Kwa hiyo, nadhani wanastahili pongezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia naomba nizungumzie barabara za Mikoa. Katika Mkoa wa Lindi zipo barabara ambazo kama zitakwenda vizuri, naamini tutapiga hatua kubwa ya maendeleo. Barabara ya kwanza, ni barabara ya kutoka Ngongo-Ng'apa-Lutamba-Milola-Mandawa na kuanzia Nanganga-Ruangwa-Mandawa. Kama barabara hii itatengenezwa vizuri ina nafasi kubwa ya kutuletea maendeleo ya haraka katika Mkoa wetu wa Lindi kwa sababu ni eneo ambalo wananchi wa Mkoa wa Lindi hasa Lindi Mjini wanalitegemea sana kwa chakula na mazao mengine ya biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani Wizara ingefanya jitihada kuipa umuhimu barabara hii ya Ngongo-Rutaba-Milola-Mandawa-Ruangwa mpaka Nanganga kwa mzunguko wake. Barabara ya Masasi-Nachingwea na barabara ya Nangurukuru mpaka Liwale ambayo kwa kweli ni kiungo kizuri sana kwa wananchi wa Liwale kuja Dar es Salaam na maeneo ya Wilaya ya Kilwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi yake aliyofanya, amefanya kazi nzuri, zipo lawama, ni wajibu kupata lawama kwa sababu hii ni kazi ya watu na hana uwezo wa kumridhisha kila mmoja, lakini kwa ujumla amefanya kazi nzuri. Mimi namshukuru sana na kwa niaba ya wananchi wangu tunakushukuru sana kwa kazi nzuri aliyofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kumalizia kwa kusema naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Spika, napenda nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nichangie hoja hii ya Waziri wa Ujenzi ambayo ipo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza katika mchango wangu ningependa niipongeze sana Serikali nzima kwa mipango mizuri ya ujenzi wa barabara. Kwa kweli nchi yetu ilikuwa na barabara chache sana ukilinganisha ukubwa wa nchi na urefu wa barabara za lami, labda tulikuwa watu wa mwisho mwisho katika Bara la Afrika na ukiangalia urefu wa barabara na wingi wa watu labda tulikuwa wa mwisho mwisho katika Bara la Afrika. Lakini sivyo tena. Katika kipindi hiki cha miaka kumi yote, haya yamebadilika na kazi kubwa imefanywa katika kupima barabara, kuzitengenezea na kuweka mipango ya kupatia fedha na kuanza kuzijenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli ni jambo la kushukuru sana na ni jambo la kupongeza sana Serikali kwa kazi kubwa ambayo imefanyika. Tulikuwa tunatafuta wawekezaji kila mahali na ilikuwa vigumu sana kupata wawekezaji wengi maana ni nchi isiyokuwa na barabara. Lakini haya yote yamebadilika na kwa kweli unapongeza picha ile kubwa, ni vizuri pia kupongeza picha ile ndogo kwa sababu isingekuwa kazi nzuri sana iliyofanywa na Wizara ya Ujenzi, tafsiri yote hii isingeweza kutokea. Hivyo, tunapenda sana tuwapongeze na msichoke kupongezwa, maana ukifanya kazi nzuri wahenga wanasema ukimpongeza mgema uwapongeze na wanywaji. *(Kicheko)*

Napenda kumpongeza sana Mheshimiwa John Pombe Magufuli na tumpongeze sana Mheshimiwa Hamza Mwenegoha na kupitia kwa Katibu Mkuu tuwapongeze sana wataalam wa Wizara ya Ujenzi na wataalam wa *TANROADS* kwa kazi nzuri sana ambazo wamefanya na kutufanya tusimame kifua mbele na tuweze kujivunia nchi yetu. Hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa ziada kabisa ningependa niwapongeze vijana wetu wa *TANROADS* Kilimanjaro, wamefanya kazi nzuri sana katika kipindi hiki cha miaka mitano ambacho mimi nimekuwa Mbunge wa Jimbo la Mwanga. Baada ya kuangalia picha kubwa, maana sasa unaweza kufikiria uwezekano katika kipindi kifupi tu cha miaka mitatu au minne ijayo kwamba unaweza kuondoka na gari ndogo kuanzia Mtwara ukaenda Bukoba bila wasiwasi. Ukiangalia ramani ya kwanza, hii iliyowekwa hapo na ukatoka Bukoba usipitie Kenya, ukarudi ukaenda Arusha, ukaenda Tanga ukarudi Dar es Salaam na Mtwara. Hili ni jambo la kushukuru sana na kuwapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie Wilaya yangu ya Mwanga. Ni vyema nikarudi pale maana kazi kubwa ya nchi imefanywa. Katika Wilaya ya Mwanga, sisi tunazo barabara za Taifa, hizi za *TANROADS*, kilometa 121. Kati ya hizi kilometa 50 ni barabara ya lami ambayo ingepita tu hata kama watu wa Mwanga tusingekubali ingepita tu kutoka Same kwenda Moshi. Sasa ukiondoa hizo kilometa 50, basi sisi tumebaki kilometa 71 za barabara za *TANROADS* ni kidogo sana. Wote mnajua kwamba wananchi wa Mwanga ni majasiri sana katika kutengeneza barabara. Mwalimu na wazee wetu kama Mheshimiwa Rashid Kawawa, walipotembelea kule walisema wananchi wa Mwanga ni Wachina wa Tanzania, maana wametengeneza barabara kweli kweli. Kwa

mikono yao wenyewe, bila kungoja Mheshimiwa John Magufuli aje kule. Lakini barabara hizi walizotengeneza wenyewe, hawa Wachina wa Tanzania hawana uwezo wa kujenga madaraja yanayostahiki na hawana uwezo wa kuweka makalvati yale makubwa makubwa na kufanya upembuzi huu unaosemwa hapa kila siku na *realignments*.

Sasa barabara hizi tungependa ukizingatia kwamba Mfuko wa Barabara unatoa fedha kidogo sana kwenye barabara za Halmashauri. Basi barabara zetu zinazoshughulikiwa na Mkoa ziongezeke, kilometa sabini na moja ni kidogo sana. Tumetoa mapendekezo kwamba zaidi ya barabara hizi ambazo zipo kilometa sabini na moja basi barabara ya kutoka Kikweni kwenda kwenye hospitali ya Wilaya iwe ni barabara ya Mkoa. Kwa sababu ina sababu kubwa kabisa kwamba kama mtu anatakiwa kupelekwa kutoka kwenye maeneo mengine ya Wilaya kwenda kwenye hospitali ya Wilaya basi kuwe na barabara ya kuaminika ili aweze kufikishwa huko. Zipo barabara kutoka Lembeni mpaka Kilomeni; Kifula-Masumbeni mpaka Butu, Mwaniko-Vuchama tunaomba barabara hizi zihudumiwe na Mkoa.

Mheshimiwa Spika, barabara zingine ambazo niliomba tangu mwaka 2001 kwamba zifikiriwe na zipandishwe daraja kutoka barabara za Wilaya ziwe barabara za Mkoa. Sasa leo asubuhi rafiki yangu Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, alikuwa anajibu hapa kwamba zipo kwenye sheria hiyo inayoletwa ya *Highway Ordinance*. Sheria hii imechukua muda mrefu sana. Imechukua muda mrefu kweli kweli na tulitegemea ingekuja mwaka 2002 haikuja, 2003 haikuja. Sasa hizi barabara ni muhimu sana katika kubadilisha hali ya barabara katika Jimbo la Mwanga. Kama unajitolea kufanya vitu kwa uhakika basi na Serikali ikupe msaada kuku-*pat on the back* kwamba wewe unafanya vizuri, kwa hiyo, tunakusaidia. Tusaidieni!

Mheshimiwa Spika, la pili ambalo ningependa kusema ni barabara ya Mjini Mwanga ambayo inaitwa *Mwanga by pass*. Katika barabara hii tungependa mabasi na magari ya kutoa huduma yapitie katikati ya Mji wa Mwanga badala ya kupita kando kama hivi sasa na kama alivyosema Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, hapa asubuhi labda hata nyumba zote zitaondoka kutokana na bomoa bomoa.

Kwa hiyo, tumepanga kwamba magari yote yapitie katikati ya Mji. Sasa ili iwezekane, tulikuwa tumeomba Wizara itupatie *Bailey bridges* mbili na Mheshimiwa John Magufuli, alikuwa ametuahidi kwamba *Bailey bridges* hizo zitapatikana mapema iwezekanavyo kwa kuwa barabara za lami ambazo zilikuwa zinatumia barabara hizo zitakuwa zinaondoa daraja hizo na kutengeneza madaraja mengine kama alivyokuwa anayataja hapa Mheshimiwa Mohammed Abdulaziz. Sasa kwa bahati mbaya, bado yale madaraja hayajafika na nilikuwa nakumbusha kwamba Mheshimiwa John Magufuli, kwa kuwa wewe ni mchapakazi mkubwa, basi haya madaraja yafike kule Mwanga kabla mambo hayajabadilika kule kwenye uchaguzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili, lilikuwa linahusu maombi yetu ya barabara ya kutoka Mwanga Mjini kwenda Milimani katika eneo la Kishegheni au *Mwanga Escarpment* ambalo kwa kweli linahitaji fedha nyingi sana za *maintenance* kila mwaka, kwa sababu ya mwinuko na kwa sababu ya hali yake mbaya ya mawe na kwamba wakati umefika



sasa eneo hili la *Mwanga Escarpment* lipatiwe hii lami ya majaribio ya *Otta Seal* ili liweze kutengemaa na magari yaweze kupanda kutoka tambarare na kwenda mlimani bila uharibifu mkubwa wa magari kama unavyotokea sasa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ningependa niongee kidogo kuhusu wakandarasi wa barabara. Kama ambavyo Wabunge wenzangu wameeleza hapa, kumekuwa na usimamizi mkubwa na mzuri kwa ngazi ya Wizara na ngazi ya *TANROADS*, lakini ujenzi wa barabara hata ule wa Wilayani bado ujenzi ni jukumu la Wizara hii. Hata kama ni kupitia Wizara zingine. Makandarasi wanaochukua ukandarasi wa kujenga barabara katika Halmashauri zetu wanafanya kazi mbaya sana. Fedha nyingi zinatumiwa lakini barabara hazitengenezwi vizuri na usimamizi katika Halmashauri ni mbovu sana.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli kwa hili tungependa sana Wizara yako na hasa Bodi ya Kusimamia Wakandarasi iende mpaka kwenye Wilaya ikawaangalie wakandarasi wa kule ambao kwa kweli wanafanya kazi mbaya sana. Kwa kuwa Madiwani hawamo kwenye Kamati za kuteua wakandarasi na kusimamia kwao kunakuwa kugumu sana na kwa hiyo, watendaji wa Halmashauri na wakandarasi hawa wanafanya kazi mbovu sana. Wakati mwingine hata baada ya kufanya kazi mbovu ya barabara hawawalipi wanavijiji wanaowaajiri katika kazi ya uchimbaji. Kwa hiyo, unakuwa na watu wengi sana wanakuja kudai Halmashauri walipwe na wakandarasi ambao wameshaondoka kwenye barabara. Kwa hiyo, tunapenda kuomba usimamizi mzuri na kama wakandarasi hawa hawafanyi kazi nzuri basi wadhibitwe kama wakandarasi wanaofanya kazi chini ya Wizara na chini ya *TANROADS*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine, tunaomba sana *labour based road maintenance* ipewe uzito tangu sasa. Kwa sababu wananchi wanaweza kutengeneza barabara zao na hasa wakipewa *incentive* ya fedha za Mfuko wa Barabara, watafanya vizuri sana na barabara zitakuwa nzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nilikuwa napenda niongee kidogo kuhusu sera ya nyumba na hasa sera ya nyumba kulingana na wafanyakazi wa Serikali na watu ambao wanakuja kuwekeza. Kwa upande wa wafanyakazi wa Serikali mimi sina tatizo kabisa na kuuza nyumba za Serikali kuwauzia wafanyakazi na tungependa kuwashauri wakishauziwa basi wazitengeneze nyumba hizo ili ziwe na sura nzuri na wasiwe na wasiwasi wowote. Lakini kutengwe nyumba ambazo haziuzwi kwa ajili ya watendaji wakuu wa Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pili, watu wanaokuja kuwekeza hapa nchini ni vizuri wapewe maeneo ya kujenga ofisi na viwanda, lakini wasipewe viwanja vya kujenga nyumba. Viwanja vya kujenga nyumba wapewe Watanzania, wapewe na mikopo ili wajenge nyumba, hawa watu wanaowekeza viwanda wakodishe. Watanzania watapata nini kama mjenga kiwanda anajenga kiwanda halafu anajenga na nyumba ya kukaa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitawapa mfano wa Mji Mkuu wa Kenya, Mji Mkuu wa Nairobi una zaidi ya nyumba 4,000 ambazo zinalipiwa kodi ya dola 1,500 kila mwezi na

utaona kila mwezi nyumba hizi peke yake zinaingiza zaidi ya dola milioni sita na Dar es Salaam lazima tubadilishe iwe hivyo. Wananchi wajenge nyumba na tuwawezeshe wajenge nyumba, halafu wawakodishe hawa watu ambao wanakuja, *expatriates* na wawekezaji ili basi kuwe na *spill over* ya mapato ambayo yanayoondoka kutoka kwa wawekezaji na wafadhili yanakwenda kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, mimi nimefurahishwa sana na bajeti hii na naiunga mkono mia kwa mia. (*Makofi*)

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. PAUL E. Ntwina:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kwa kumpongeza sana Waziri Mheshimiwa John Magufuli, pamoja na Naibu Waziri, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Katibu Mkuu wa Wizara hii Ndugu Kijazi, pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii imeyafanya mazuri sana katika jimbo la Songwe. Hivi sasa *graders* na vijiko vya kutengeneza barabara zinaendelea kutengeneza barabara ya Galula-Namkikwe. Nategemea bila shaka makandarasi wanaoendelea sasa hivi wataitengeneza katika hali ya juu sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na barabara hii barabara ya Mbalizi-Galula-Mkwajuni-Saza-Makongorosi. Yale maeneo mabaya yamechongwa vizuri ingawa bado kama nilivyosema kwenye hotuba yangu kwa Waziri wa Mipango na Fedha tunahitaji sasa lami ili kuoanisha ile barabara ya Mbeya-Chunya na Makongorosi kwenda Itigi.

Mheshimiwa Spika, huwezi kukwepa hili kwa sababu Makongorosi, ni pacha ya barabara ya Mbalizi-Makongorosi, watendaji wako wanajua hili vizuri. Huwezi kuzungumzia barabara hizi bila kuongelea zote mbili. Hapo zamani mabasi toka Arusha yaitwayo *Oman Bus* yalikuwa yakipita pamoja na yale ya *Railways*. Sasa hivi licha ya ujenzi wenu, mabasi bado hayaendi kwa kutumia barabara ile, barabara bado ni mbovu kwa maana inatengenezwa kwa kima cha udongo kila mwaka, mvua zikija zinavuruga haipo tena.

Mheshimiwa Spika, katika barabara ya Galula-Namkukwe lipo daraja la Mto Songwe limejengwa miaka ya 1970 ambalo ndiyo kiwango kikubwa sana. Daraja hili huenda likavunjika wakati wowote ule. Naomba kujua Serikali itafanya nini kususuru daraja hili la Mto Galula? Inawezekana watendaji wa Wizara hii hawalioni zaidi ya sisi wananchi tunaolitumia. Naomba majibu kujua hatma ya daraja hili la barabara ya Galula-Namkukwe.

Mheshimiwa Spika, naishukuru sana Wizara kwa kutambua na kuanza kujenga barabara ya Saza-Kininga-Kapalala. Katika barabara ile yapo maeneo korofi ya udongo mweusi na udongo mwekundu. Naomba maeneo yale yajengwe vizuri sana tena kwa kiwango cha changarawe.

Mheshimiwa Spika, lipo ombi maalum ya kufungua eneo la mbele la Kapalala kwenda Kijiji cha mbele cha Gua ambako ni mpaka wa mbuga za Lukwati na lipo eneo la barabara la zamani enzi ya mkoloni kwenda Mpanda-Sikonge na Tabora. Kwa nini Serikali haioni umuhimu wa kufungua eneo hili ili wananchi wafaidike na urahisi wa barabara hii?

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa John Magufuli, hebu ajaribu walau kuikemea barabara hii ili iwe mkombozi wa watu wa eneo hili.

Mwisho bado lengo na nia na maombi ya barabara ya Mbalizi-Galula-Mkwajuni-Saza-Makongorosi iwekwe lami katika msimu ujao wa bajeti kwani itasaidia kukuza uchumi wa nchi hii na hasa wananchi wa eneo hili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kukupongeza wewe Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na wafanyakazi wote wa Wizara ya Ujenzi kwa kazi nzuri mliyoifanya kwa kipindi cha miaka mitano. Wizara yako chini ya uongozi wako wa kimapinduzi imeweza kutekeleza Ilani ya CCM ya Uchaguzi ya mwaka 2000 kwa asilimia 90%. Hongera sana.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa jimbo la Rorya, Wilaya ya Tarime ni mashahidi hai kuhusu utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi kuhusu Wizara yako. Kwa kipindi cha miaka 40, wananchi wa jimbo la Rorya walikuwa wanateseka sana kuhusu usafiri wa barabara, kuanzia mwaka 2002 chini ya uongozi wako thabiti barabara za jimbo la Rorya zenye urefu wa kilometa 258 zimetengenezwa na zinapitika wakati wote kwa mwaka. Naomba upokee shukrani za wananchi wa Jimbo la Rorya. Naomba ufikishie wasaidizi wako shukrani hizi.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru pia Mheshimiwa Waziri kwa hatua zake za kimapinduzi kuhusu kivuko cha Kinesi. Nimesoma katika kiambatanisho B kitabu chako cha Hotuba ukurasa 142, *Project Code 4188 Procurement of Musoma-Kinesi Ferry* ununuzi umepangwa katika mwaka wa fedha 2006/2007. Kwa kuwa gati ya Kinesi ujenzi umekamilika mwaka 2002 na wananchi wanapata shida sana, naomba wakati tunangojea ununuzi wa kivuko kipya, jitihada zifanyike kwa kipindi cha mwaka 2005/2006 kupata kivuko cha muda.

Kuhusu ukarabati na ukarafati wa barabara zinazohudumiwa na *TANROADS* Mkoa, naomba barabara hizi zinazoendelea kuhudumiwa hasa wakati huu ambapo CCM itatetea sera Ilani ya Uchaguzi wa mwaka 2000.

Ombi la pili kuhusu ukarabati na ujenzi wa barabara za Jimbo la Rorya ni ukamilishaji wa ujenzi wa barabara ya Nyamagongo-Masongo-Bubombi-Kirongwe hadi Mpakani kwa Obadia Kenya urefu wa kilometa 17 kutoka barabara ya Mkoa. Barabara hii ndiyo ilikuwa barabara kuu iliyokuwa inatumika wakati wa Utawala wa Ujerumani. Barabara hii ni muhimu sana hasa ikizingatiwa kuwa inatumika na Kata tano, nilikuletea

maombi maalum pamoja *BQ*. Naomba sana unilinde kwa kuwa hata Waziri mwenzako Raila ameanza kutengeneza barabara kwa upande wake kuunganisha upande wa Rorya. Naomba sana utukamilishie ndogo ya wananchi wa Jimbo la Rorya ya miaka 70.

Ombi la tatu, barabara ya Utegi (Mikai)-Shirati kilometa 45 inayohudumiwa na *TANROADS* imetengenezwa hadi Ikome tu. Imecha kutaja Shirati-Bandari ya Sota kwa kutokuelewa kuwa unapozungumzia Shirati unazungumzia Bandari ndogo ya Sota. Bandari hii imefanyiwa ukarabati mkubwa na kufunguliwa mwaka 2004. Meli kutoka Kenya na Uganda zinatia nanga, tatizo ni kuwa *TANROADS* haikuingiza kipande cha barabara kutoka Mkoma hadi Bandari ya Sota. Kamati ya Bunge katika hotuba yao wameomba sehemu hii ya barabara kilometa 9 ihudumiwe. Naomba sana sehemu hii ya barabara ya Utegi (Mikai-Mkoma-Shirati Sota iingizwe kwa mradi wa *TANROADS*.

Nakushukuru sana, nakuombea Mungu na Naibu Waziri uwajalie katika kinyang'anyiro cha ubunge mtashinda na naunga mkono hoja.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri John Magufuli, Naibu Waziri Mheshimiwa Hamza Mwenegoha na Katibu Mkuu Ndugu Kijazi, kwa kazi nzuri sana waifanyayo Wizarani. Wananchi wa Kongwa wanashukuru sana, ila wameniomba nifikishe kilio kifuatacho:-

Mheshimiwa Spika, barabara zifuatazo ziangaliwe kipekee ikiwezekana kwa mradi wa *HIPC*.

Kwanza Kongwa- Sagara - Suguta, haipitiki hivi sasa pamoja na matengenezo madogo madogo panahitajika kalvati kwenye kichanga cha Ibwaga na madaraja kati ya Sagara-Ijalia na Iduo.

Pili, barabara ya Kongwa J4 hadi Hogoro J4 kilometa 8 haijawahi kuguswa kwa matengenezo yoyote *for years!* Tuikumbuke jamani.

Mheshimiwa Spika, tatu, Kongwa J4 - Mwapwa-Suguto-Mlali-Pandambili, hii ipewe fedha nyingi za kutosha, ni barabara muhimu inayopita katika maeneo ya kilimo kikubwa cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, ninayo maombi zaidi lakini hayo matatu yatosha kwa leo na naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naunga mkono hoja hii na natoa pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na wataalamu wote wa Wizara na Wakala wa *TANROADS*.

Mheshimiwa Spika, katika mchango wangu nitajielekeza kwenye maeneo ya barabara tu. Ningependa kupata maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi suala zima kuhusu utaratibu na upana wa *Road Reserve Area* ya barabara kutoka Ubungo-Mlandizi-Chalinze-Morogoro. Kwa sasa *Road Reserve Area* imepanuliwa kutoka mita 70 mpaka mita 100. Kwa kufanya kitendo hichi Serikali imewafanya

wananchi wabomolewe nyumba zao na wengine nyumba zao au majengo yao yametiliwa alama za X maana yake mali hizi zinaweza zikabomolewa wakati wowote. Tatizo hili limewakumba wananchi wengi wa *Kimara Stop Over*, Temboni, Mbezi Luis, Korogwe, Kiluvya na kadhalika.

Tafadhali, Mheshimiwa Waziri nakuomba utoe maelezo kama kweli kuna ulazima wa kuwa na *Road Reserve Area* pana kwa kiasi cha mita 100 zilizowekwa sasa badala ya mita 70.

Mheshimiwa Spika, barabara kutoka Kiomboi Bomani-Kisiriri-Kidaru-Ibaga-Kidarafa, barabara hii ya Wilaya ya Iramba, sasa inahudumiwa na Halmashauri, lakini hali yake Mlimani sasa hivi haipitikia kabisa hasa sehemu ya Mlimani. Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Singida mwaka juzi ilipendekeza kuwa Serikali Kuu ichukue majukumu ya kuihudumia kwa sababu Halmashauri ya Iramba haina uwezo kabisa kifedha kutengeneza barabara hii ambayo inaunganisha maeneo muhimu kwa kuzalisha mazao ya kilimo, mifugo na misitu. Tafadhali Mheshimiwa Waziri usikie kilio cha wananchi wa vijiji vya Kisiriri, Kidaru, Ndurumo, Tyegelo na Ndurumo kwani sasa wanajiona kama wametengwa kama wafungwa walioteswa Gereza la Kisiwani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara kutoka Shelui-Sekenke-Nkonkilangi-Nsunsu-Mingela-Doromoni- Megilango-Luona Kigaa-Kidaru, kupitia kwako namwomba Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi awape wananchi wa vijiji vilivyotajwa juu barabara inapopitia maelezo ya kuridhisha sababu zilizofanya Serikali iamue kuwa barabara kutoka Shelui kupitia Kijiji cha Mgongo mpaka daraja kwenye Kijiji cha Sekenke Machimboni (kilometa 15) kuwa ni barabara ya Mkoa (*TANROADS*) na sehemu ya barabara inayoendelea kutoka Kijiji cha Sekenke Machimboni (Darajani) kuendelea vijiji vya Nkonkilangi mpaka Doromoni-Luono-Kidaru kuwa ni chini ya huduma ya Halmashauri ya Wilaya (takribani kilometa 40).

Mheshimiwa Spika, kusema kweli Halmashauri haina uwezo kuhudumia barabara hii ipasavyo. Katika sehemu ya barabara hii kunahitajika kujengwa madaraja/*ma-drifts* mengi madogo na makubwa kwenye mito mingi na makorongo makubwa kwa madogo kutoka milima ya Sekenke inayokinga Bonde lote la Shelui/Wembere kuanzia Kata ya Urughu mpaka Kata ya Kidaru.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Bonde hili la Wembere/Shelui wanaomba Serikali iwasaidie kujenga madaraja/*ma-drifts* tu na wananchi wako tayari kuchangia nguvu zao kwa hali na mali kufyeka, kulima, kuchimba na kusawazisha maeneo yote ya njia ya barabara kwenye tambarare na mabonde ya wastani. Mheshimiwa Waziri, barabara hii inahudumia vijiji ambavyo ni maarufu sana kwa kilimo, madini, ufugaji, uvuvi katika Ziwa la Kitangiri, Utalii na Maliasili nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, barabara hii wakati wa msimu wa mvua (miezi 4) haipitiki kabisa na magari ya aina yeyote hata mikokoteni inayovutwa na ng'ombe/punda na baiskeli inakuwa vigumu kupitisha chochote na hata wagonjwa hawawezi kupelekwa kupata huduma za Hospitali Kiomboi au Kituo cha Afya kilichopo Kijiji cha Mgongo.

Mheshimiwa Waziri, tunaomba uonyeshe huruma zako, wananchi wa vijiji hivi katika Bonde la Wembere/Shelui wanakuomba uone umuhimu kuwa barabara hii ichukuliwe na Serikali Kuu (*TANROADS*- Mkoa wa Singida).

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri John Magufuli na pia kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Iramba Magharibi natoa pongezi nyingi kwa kazi nzuri ya kuendeleza sekta ya barabara.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba ya kina na kwa namna alivyoiwasilisha. Napende pia kumpongeza Naibu Waziri na watendaji wote chini ya Katibu Mkuu. Ufanisi wa kazi zinafanyika unatokana na ushirikiano uliopo katika Wizara hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kupitia kwako nipongeze Serikali kwa utekelezaji mzuri wa Ilani ya Uchaguzi kuhusu mawasiliano ya barabara Mkoani Kagera. Barabara nyingi hata zile za vijijini ni nzuri sana na hupitika wakati wote mwaka mzima.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara ya lami Kyamyorwa-Bwanga ambao Mheshimiwa Rais ameweka jiwe la msingi hapo tarehe 21 Juni, ni wa kupongeza sana. Barabara hiyo ni muhimu kwa vile itafupisha umbali wa safari za Bukoba-Mwanza na kadhalika lakini pia barabara hii itatoa huduma kwa wananchi tukizingatia kuwa inapita katika eneo la uzalishaji wa mazao ya chakula kwa wingi na pia biashara hivyo italeta hamasa kwa uzalishaji zaidi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo naomba kujua ni lini barabara ya Katoma-Kanyigo itatengenezwa ili ipitike wakati wote kwa kutengeneza eneo la Kajai. Eneo hili ni bonde kubwa lenye maji mengi na kuna vidaraja vingi, wakati wa mvua nyingi pamoja kama ilivyotokea mwaka huu na kusababisha Kanyigo kuonekana kama (Ulaya) kwa vile ilikuwa ni lazima kuzunguka Bugandika. Eneo hili limekuwa ni kero. Napenda kuiomba Serikali ilianganalie eneo hili yaelekea panahitajika kuinua tuta kubwa na kuweka madaraja imara zaidi. Tuzingatie kuwa hii ni barabara ya ulinzi.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kuwaombea Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, Mungu awasaidie wapite bila kupingwa katika Uchaguzi Oktoba, 30. Kwa vile sikusema hapo mwanzoni, nitoe salaam za rambirambi kwa familia ya Mheshimiwa Margaret Bwana, kwa kifo kilichotokea ghafla, Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi. *Amin.*

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nikupongeze wewe Mheshimiwa Spika, kwa kuweza kuliongoza Bunge hili kwa uwezo na uadilifu mkubwa katika kipindi cha miaka hii mitano. Mwenyezi Mungu akujaalie na akupe afya njema.

Mheshimiwa Spika, naomba pia niwapongeze Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara, Wakurugenzi na watumishi wote wa Wizara hii ya Ujenzi na Kitengo cha *TANROADS* na *RFB* kwa kazi kubwa wanayoifanya ya

kuhakikisha nchi yetu inakuwa na mawasiliano mazuri ya barabara. Mwenyezi Mungu pia awajaalie kila la kheri hapa duniani na hata huko akhera.

Mheshimiwa Spika, naomba nirudie tu kwa kumwomba Mheshimiwa Waziri ombi letu la kupatiwa vifaa vya ujenzi vya barabara kwa kutumia njia yoyote ile ili mradi tufanikishe kupata vifaa hivyo, sababu tuweze kulipunguzia Taifa mzigo wa kupoteza fedha nyingi kwa kutoa hela kwa wakandarasi wanaotoka nje ya Wilaya na wanakuja mikono mitupu na hatimaye hawatengenezi vizuri, pesa za walalahoi au wananchi zinapotea bure na mwishowe huja lawama kubwa kwa viongozi wa Serikali na Serikali kwa ujumla. Natumaini Mheshimiwa Waziri safari hii utatoa tamko rasmi la kupatiwa vifaa hivyo. Ahsante!

Mheshimiwa Spika, thamani ya vifaa hivyo ni Dola za Kimarekani 230,000 lakini tukapata shilingi milioni 200 tu, mambo mazuri.

Mheshimiwa Spika, pili, naomba kwa masikitiko makubwa sana kuleta malalamiko yangu kupitia kwako na Mwenyekiti au Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Wakandarasi juu ya Kampuni moja ya Ujenzi inayoitwa *TANHOPE LTD.* ambayo ilipata *tender* ya kuja kutengeneza barabara ya Mkoa wa Pwani iliyopo Mafia.

Mheshimiwa Spika, alipokuja kule Mafia alikuja na vifaa vibovu na hatimaye kushindwa kutengeneza barabara hiyo na kusimamishwa. Lakini alipokuwa Mafia alikuwa anakodisha magari, anakopa *oil* na mafuta ya *diesel* na vitu vingi ambavyo mpaka anasimamishwa mkandarasi huyo anayelitwa Kileo ndiye aliyekuja Mafia kama mmoja wa Wakurugenzi wa Kampuni ya *TANHOPE* alikuwa amekopa vifaa hivyo na vikafikia thamani ya shilingi 3,746,300/=.

Mheshimiwa Spika, naomba nikuhakikishie hao wanaoidai Kampuni ya *TANHOPE* ni kama ifuatavyo, Ndugu Mwalim Esaya Surera, alikuwa anadai jumla ya shilingi 410,000/=, alizolipwa ni shilingi 205,000/= na anadai shilingi 205,000/= hazijalipwa.

Mheshimiwa Spika, mdai wa pili ni Ndugu Abdallah Jabey alikuwa anadai jumla shilingi 1,476,300/=, alizolipwa ni shilingi 738,150/= na anadai 738,150/=, mdai wa tatu ni Ndugu Hassan Makunda, alikuwa anadai jumla shilingi 1,585,000/=, alizolipwa ni shilingi 792,500/= na bado anadai shilingi 792,500/= na mdai wa mwisho ni Ndugu Rashid Abdallah alikuwa anadai jumla shilingi 275,000/=, alizolipwa ni shilingi 137,500/= na bado anadai shilingi 137,500/=.

Mheshimiwa Spika, hizo pesa zilizolipwa zililipwa baada ya mvutano mkubwa na kusaidiwa na ndugu zetu wa *TANROADS* Mkoa wa Pwani baada ya kubakia na kuzuia pesa zake za *retention* kwa ujenzi wa barabara hiyo aliyoiboronga Mafia ndio tukazipata.

Sasa hivi pesa zilizobaki anadaiwa na hao wananchi ni shilingi 1,873,150/= hadi leo ni karibu au zaidi ya miezi nane kila nikimkumbusha sasa anakuwa mkali na hataki

kulipa. Hivyo naomba sana Mheshimiwa Waziri unisaidie hizo pesa za hao wananchi zilipwe haraka kabla hata ya mwisho wa Bunge hili ili zisije kuwa sumu kwangu.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba niunge mkono hoja hii asilimia mia kwa mia. Ahsante sana.

**MHE. BASIL P. MRAMBA:** Mheshimiwa Waziri, hongera kwa hotuba nzuri na *debate* poa.

Mheshimiwa Spika, nilimweleza Naibu Waziri matatizo ya barabara yangu. Norway wanachelewesha idhini ili tutiliane sahihi (Norway - Tanzania) ya *framework* ya ufadhili.

Mheshimiwa Spika, baadae wanasubiri taarifa ya *TANROADS* sharti la Uarabu limetukwamisha. Wako *flexible* wakipata taarifa ya *TANROADS*. Wale Wachina wanaendelea vizuri kukwangua njia ili waumbe. Kesho nitampigia Waziri au Balozi wa Norway nikipata habari ninazo subiri. Jiwe la msingi ni muhimu *mid July*. *RC* pia amemsihi Rais.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa John Magufuli na Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, ambao ni Waziri na Naibu Waziri wake, kazi nzuri wanayoifanya nchini. Pia pongezi kwa Katibu Mkuu Ndugu Kijazi na watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, natoa pole kwa ndugu, jamaa na wapiga kura wa Kilombero na Rukwa kwa kuwapoteza Wabunge wao mahari. Naomba Mungu awajalie raha ya milele. *Amin*.

Mheshimiwa Spika, nataka kuchangia machache kuhusu Wizara hii. Kwanza nataka kuungana na ushauri wa Kamati ya Miundombinu kuhusu ujenzi wa nyumba za watumishi wa Serikali. Mpango ni mzuri lakini eneo kati ya nyumba na nyumba ni dogo hivyo kutoa sura ya nyumba kuwa kama makambi. Hivyo ni vyema kujenga nyumba kwa nafasi kubwa ili wakazi waweze kupanda maua na mchicha kidogo.

Mheshimiwa Spika, pili, katika ukurasa 21, Wizara imetoa maelezo kuwa imeandaa mwongozo unaoonyesha jinsi wawekezaji binafsi watakvoweza kutengeneza barabara na madaraja kwa miradi iliyoainishwa. Tatizo langu ni kwamba endapo wawekezaji binafsi hawatajitokeza je, Serikali ina mpango gani mbadala? Naomba ufafanuzi wa hili kwa vile barabara na madaraja yaliyoainishwa (miradi) ni muhimu sana kwa kufufua uchumi wa sehemu husika.

Mheshimiwa Spika, napongeza Serikali kwa kushughulikia mtandao wa barabara za kuunganisha mikoa lakini ifike wakati wa kuunganisha barabara zilizo nyeti kati ya Wilaya na Wilaya kutegemeana na umuhimu wa maeneo husika. Katika hili naomba kuungana na Waheshimiwa Wabunge waliozungumzia barabara ya kutoka Mtwara,



Nanyamba, Tandahimba, Newala, Masasi mpaka Nachingwea kwa kiwango kinachostahili hasa cha lami.

Mheshimiwa Spika, barabara hii inapita kwenye maeneo ambayo huzalisha korosho, karanga na ufuta ambayo wananchi ndiyo mazao yao ya biashara na huwawezesha kuhudumia familia zao. Pia inatia faraja kuwa angalau kuna hatua nzuri iliyofikiwa katika maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Mtwara, Mnazi Mmoja, Masasi, Songea-*Mbamba Bay* kwa kiwango cha lami kwani naamini uchumi wa sehemu hizi sasa utachangamka kwa vile itakuwa rahisi kufikisha mazao yao kwenye masoko hali ya mbali.

Mheshimiwa Spika, ukombozi wa kiuchumi mwingine kwa upande wa ukanda wa maendeleo wa Mtwara unatarajiwa baada ya kumalizika kwa daraja la Umoja kati ya Tanzania na Msumbiji ambalo Wizara/Serikali imetoa taarifa kuwa ujenzi utanza katika mwaka huu wa bajeti 2005/2006. Pongezi nyingi kwa Serikali ya awamu ya tatu chini ya uongozi wa Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa.

Mheshimiwa Spika, zaidi nashauri kuwa makandarasi wanaolegalega katika kumaliza kazi zao kwa wakati basi watathminiwe upya ili kama kazi zinawashinda watafutwe wengine kwa sababu ucheleweshaji wa kazi hatimaye gharama za vifaa vya ujenzi vinapanda na kusababisha kuhitajika fedha nyingi za ziada.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. JOHN L. MWAKIPESILE:** Mheshimiwa Spika, naomba nitoe mchango wangu mfupi kwa maandishi. Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi ni nzuri sana na inatoa matumaini makubwa kwa Watanzania wote. Natoe pongezi kubwa sana kwa Waziri Mheshimiwa John Magufuli. Uwezo wake mkubwa na umakini wake katika kufuatilia kazi za ujenzi nchini kote ni mfano mzuri wa kuigwa. Vile vile nampongeza Naibu Waziri wa Ujenzi kwa kazi nzuri na usikivu wake kwa matatizo ya Wabunge.

Mheshimiwa Spika, ningependa nimkumbushe Mheshimiwa Waziri kwamba Wilaya yangu ya Kyela ni Wilaya iliyo tambarare. Kyela ni moja ya Wilaya inayopata mvua kwa wingi kila mwaka. Kwa mwezi wa Aprili na Mei Wilaya hupata mafuriko makubwa ambayo yanaharibu sana barabara zote za Mkoa.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuchukua nafasi hii, kwa niaba ya wananchi wote wa Wilaya ya Kyela, kumshukuru sana Mheshimiwa John Magufuli, kwa uwezo wake mkubwa wa kusikiliza maombi yangu ya kutengeneza barabara mbili muhimu kwa uchumi wa Wilaya ya Kyela. Barabara mbili hizi ni barabara ya Ibande - *Itungi Port* na barabara ya Kikusya-Ipinda-*Matema Beach*.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 125 wa kitabu cha hotuba ya Waziri, kimbatanisho na 4 (2) barabara ya Ibanda-*Itungi Port* imetengewa shilingi 60,000,000/= kwa kutengeneza kilometa 1.5. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kuikamilisha ahadi yake aliyotoa akiwa Naibu Waziri kwamba barabara hii

ingetengenezwa kwa kiwango cha lami awamu kwa awamu. Kipande kilichobaki hadi kufikia lango la *Itungi Port* ni kilometa 3 ½ shilingi 60,000,000/= zilitengwa hazitoshi. Ninamwomba Waziri aongeze ili tumalize barabara hii.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana Mheshimiwa Waziri alisikia kilio changu akanipa shilingi 100,000,000/=. Barabara ya Kikusya-Ipinda-*Matema Beach* ni barabara muhimu sana kwa uchumi na mawasiliano katika Wilaya ya Kyela. Ninaishukuru sana Wizara na *TANROADS* kwa kutengeneza sehemu korifi za barabara. Bado kuna sehemu korofi ambazo hazijakamilika hasa kati ya Kikusya na Ipinda. Mwaka jana, ingawa barabara hii haikutajwa na kutengewa fedha katika bajeti lakini Waziri alisikia kilio changu nikichangia hotuba yake na akanipa shilingi 40,000,000/ =.

Mheshimiwa Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri aniahidi tena shilingi 50,000,000/= ili *TANROADS* watengeneze barabara hii kwani mwezi wa Aprili mwaka huu mafuriko yaliharibu sana barabara hii. Barabara hii ni uhai wa Wilaya! Barabara hii ni uhai wangu !! Naomba Waziri alione suala hili kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Waziri wa Ujenzi. Ahsante sana.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa naomba nichukue nafasi hii kutoa rambirambi zangu kwa kifo cha Mheshimiwa Margareth James Bwana, aliyefariki dunia tarehe 23 Juni, 2005. Rambirambi hizi ziwafikie wazazi wake, kaka zake, watoto wake, ndugu zake, marafiki zake, wapiga kura wake wa Mkoa wa Rukwa na wananchi kwa ujumla. Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa pongezi kwa Mheshimiwa John Pombe Magufuli, Waziri wa Ujenzi, ndugu yangu Mheshimiwa Hamza Abdallah Mwenegoha, Naibu Waziri wa Ujenzi, Katibu Mkuu na watendaji wote walioshiriki katika kuandaa bajeti hii nzuri yenye mwelekeo mkubwa wa kuinua uchumi wa nchi na kuondoa kero ya usafiri kwa Watanzania wote kwa ujumla. Mungu awape uzima na washinde tena katika majimbo yao, waje waendeleze kusimamia bajeti hii waliyoandaa.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitashukuru Serikali kwa juhudi kubwa iliyofanyika katika kutengeneza barabara nchi nzima, hususan ujenzi wa barabara za Mkoa wa Singida yaani Dodoma hadi Manyoni, Manyoni hadi Singida Mjini na Singida Mjini hadi Shelui ambao tayari ziliishapata makandarasi.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kuwa makandarasi waliopewa barabara za Dodoma hadi Manyoni na Manyoni hadi Singida zinatengenezwa pole pole sana. Hivyo wananchi wanapata wasiwasi kuwa hawatamaliza kwa muda waliopangiwa hasa barabara ya Manyoni hadi Singida Mjini. Naomba ushauri uliotolewa na Kamati ya Miundombinu ufuatiliwe.

Mheshimiwa Spika, vile vile nipongeze Serikali kwa ujenzi wa barabara ya lami toka Dar es Salaam hadi Morogoro hasa kwa kuweka *milestones* pembeni mwa barabara

ambayo yanasaidia sana abiria pamoja na madereva kufahamu safari yake ina umbali kiasi gani.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iweke hayo *milestones* barabara zote hata barabara za mikoa mfano Dodoma hadi Singida kupitia Kwamtoro na barabara Singida kwenda Kiomboi kupitia Ndago na nyingine zote.

Mheshimiwa Spika, nashukuru Serikali sasa inaweka pia mipaka ya upana wa barabara ili kuwasaidia wananchi kufahamu wanatakiwa ujenge umbali gani toka barabarani ili waondokane na bomoa bomoa kila ujenzi wa barabara unapoanza.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali kwa ujenzi wa nyumba nyingi za kutosha kwa ajili ya watendaji wa Serikali kwa kila Mkoa. Naiomba Serikali ujenzi huu wa nyumba za Serikali sasa uelekezwe Wilayani kwani huko pia wapo watendaji wanahitaji kuthaminiwa ama kuwekewa mazingira mazuri ya kazi.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa kuwauzia watendaji nyumba, lakini nina wasiwasi kuwa nyumba hizo wataonufaika ni watendaji wa ngazi ya juu tu. Watumishi wa kawaida mfano walimu, wauguzi, makarani na kadhalika hawatanufaika na nyumba hizo maana bei ni za juu sana.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali sasa iweke mkakati wa kujenga nyumba za watumishi wa chini na kati ili nao wafaidi matunda ya Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, upitishaji au uswagaji wa mifugo kama ng'ombe, barabarani huharibu barabara. Naomba adhabu kali au faini kubwa kwa anayepitisha ng'ombe barabarani ili barabara zetu zidumu.

Mheshimiwa Spika, nitumie pia fursa hii kumpongeza Meneja wa *TANROADS* na watendaji wote wa *TANROADS* kwa kazi nzuri wanayofanya katika kutengeneza barabara za Mkoa wa Singida. Kwa kweli barabara za Mkoa wa Singida zinapitika kote na maeneo korofu hukarabatiwa mara yanapojitokeza.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kuwatambua watendaji hao kwa kazi zao nzuri na wengine wa maeneo mengine kama wapo.

Mheshimiwa Spika, sipendi niwe mchoyo wa fadhila, kwani bajeti hii haikuacha kutenga fedha kwa ajili ya barabara za Mkoa wa Singida. Naipongeza sana Serikali kwa kutenga fedha kwa ajili ya barabara ya Manyoni, Itigi hadi Tabora na barabara ya Singida Mjini hadi Minjingu (Arusha).

Mheshimiwa Spika, naiomba sana Serikali iwape makandarasi wenye vifaa na uwezo ili ziweze kumalizika kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Spika, napenda sasa nimalizie mchango wangu kwa kuunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia kwa mia na niwatakie utekelezaji mwema.

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kabisa kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Mwanza Mjini, kutoa rambirambi kwa kifo cha Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Margareth Bwana. Mungu aiweke pema roho yake. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, pili, naomba kuchangia kwenye Wizara ya Ujenzi. Ni lazima kwa kweli nimpongeze Waziri wa Ujenzi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wote kwenye Wizara ya Ujenzi kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuandaa hotuba hii ambayo imekuwa wazi na nzuri. Mimi nimeifurahia sana.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa kazi ya ujenzi wa barabara nchi nzima inaonekana ingawa kazi bado kubwa kutokana na ukubwa wa nchi yetu. Lakini matumaini kila mmoja wetu anayo kwamba hatimaye kila barabara itajengwa kwa kiwango cha kuridhisha. Kutokana na hatua iliyofikiwa naomba nipongeze Wizara ya Ujenzi na pia *TANROADS* kwa kazi nzuri hiyo. Nawatakia heri sana wote.

Kwa kuanzia naipongeze sana Serikali ya CCM kwa kazi nzuri ya ujenzi wa barabara za Jijini Mwanza. Ujenzi wa barabara hizi umetuletea maendeleo makubwa, ustaarabu na zimepamba Jiji la Mwanza. Kwa sasa kwa juhudi za Halmashauri yetu tumeanza kufunga taa za barabarani kwenye baadhi ya mitaa.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hapo ninayo hoja kwamba kwa Waziri wa Ujenzi kutimiza ahadi yake kwetu wana Mwanza kwa kuchangia shilingi bilioni moja ili tuongeze barabara zaidi zilizojengwa kwa kiwango cha lami. Hoja yangu ni kuipongeza Wizara ya Ujenzi zaidi.

Mheshimiwa Spika, tunalo tatizo la barabara nyingi Jijini Mwanza ambazo zinahitaji kujengwa kwa kiwango cha lami. Kwa wastani, ujenzi wa barabara ya lami hugharimu shilingi milioni 250 kwa kilometa moja. Halmashauri ya Jiji la Mwanza pato lake kwa mwaka ni shilingi bilioni 7.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Halmashauri hii peke yake kwa kiwango kikubwa haina uwezo wa kujenga barabara za Mwanza ninazozizungumzia. Tunayo barabara ya Pamba-Lumumba-Karuta, Kilimahewa-Isamilo Sanga-Igogo, Bugarika-Kitangiri-Makaburini hadi Kabuhoro na kadhalika zinahitaji kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naiomba Wizara ya Ujenzi itufikirie zaidi kwenye ujenzi wa barabara hizi isiachie Halmashauri ya Jiji la Mwanza.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara ya Ujenzi kama inayoshughulikia barabara za Jijini Dar es Salaam ifanye hivyo hivyo kwa Jiji la Mwanza. Wizara ya Ujenzi ipange utaratibu wa kujenga barabara za Jiji la Mwanza au yenyewe au kwa kushirikiana na Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, mwisho naiomba Wizara ya Ujenzi iongeze bidii kushughulikia barabara ya Kisesa hadi Usagara. Naomba sana ujenzi wa barabara hii ufanywe kwa haraka kutokana na umuhimu wa barabara hii.

Mheshimiwa Spika, ninayo imani Mheshimiwa Waziri atanipa majibu kwenye hoja zangu hizi. Baada ya kueleza haya naunga mkono hoja ya Wizara hii.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Waziri wa Ujenzi kwa kazi nzuri ya ujenzi wa barabara nchini. Pia, Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa ushirikiano wao katika ujenzi wa barabara nchini.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kazi nzuri iliyofanyika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuzungumzia barabara ya Ilula - Magogo na baadaye hadi Mwanza. Barabara hii ilishajengwa, lakini cha ajabu inafumuka sehemu mbalimbali hali ambayo kama haitafanyiwa matengenezo italigharimu Taifa pesa nyingi. Hivyo, naomba kujua Serikali ina mkakati gani wa haraka kuepusha balaa hilo.

Mheshimiwa Spika, ujenzi na ubora wa shughuli nzima ya barabara ni pamoja na kuwa na Mfuko wa Barabara ambao umeisaidia sana. Lakini katika hotuba ya Waziri wa Fedha alifuta baadhi ya vyanzo vya mapato vya mfuko huo kama vile leseni za magari makubwa. Je, Wizara imejiandaaje kuziba pengo hilo ili mazuri yanayotendwa na mfuko yaendelee?

Mheshimiwa Spika, barabara ya Fulo-Nyambiti kupitia Sumve, Koromije-Kanyerere ni mbovu sana hasa eneo la Kanyerere darajani hadi Kanyerere madukani, ni urefu wa kilometa tano hadi saba. Je, Waziri amefikia wapi katika ahadi yake kwa Askofu Mayala ya kutengeneza barabara hiyo?

Mheshimiwa Spika, wananchi na wagonjwa hali zao ni hatari hasa wakati wa mvua. Naiomba Serikali ifikirie suala hili ili eneo la Kanyerere litengenezwe.

Mheshimiwa Spika, upembuzi yakinifu wa barabara ya Usagara - Kisesa kupitia Fela umekamilika na kama nilivyosema katika swali langu la nyongeza, maafa yanatokea kati ya Fela na Bujingwa wananchi wanashindwa kupita eneo la daraja la Fela ambalo ni bovu kwa kufuata mahitaji yao muhimu kama vile hospitali na kadhalika. Ombi langu kwa Serikali ni kwamba, tunaomba iweze kuweka madaraja yanayoweza kuhamishika ili kusaidia jamii isiendelee kupoteza maisha wakati umma unaendelea kusubiri ujenzi wa barabara mzuri ambayo itakuwa ya kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kuiomba Serikali iendelee kutunza au kuendelea kuhudumia barabara zilizotengenezwa ili zidumu. Mfano ni kazi nzuri iliyofanyika Mwanangwa - Misasi - hadi Salawe, kwani sasa hivi ujenzi wa mradi wa

maji toka Ihelele hadi Kahama na Shinyanga unaharibu barabara hiyo. Hivyo, ni wajibu wa Serikali kuona kazi hiyo inaboreshwa.

Mheshimiwa Spika, narudia kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na Katibu Mkuu pamoja na timu yao yote kwa kazi nzuri wanayofanya. Pamoja na pongezi hizi, napenda kupata ufafanuzi ufuatao.

Kwanza, kwa vile Serikali yetu imekwisha kufanya upembuzi yakinifu au utafiti wa awali kwa kutumia fedha zetu za ndani ya Serikali sasa inaweza kueleza kama mfadhili amepatikana wa kuunganisha barabara ya Makuyuni - Lalago au sasa Njiapanda (Karatu) Lalago katika mkoa wa Shinyanga. Je, baada ya utafiti wa awali au upembuzi yakinifu barabara hiyo itagharimu kiasi gani na mfadhili aliyeonyesha nia ya kujenga barabara hiyo ni nani?

Pili, kwa vile *RCC* ya Mkoa wa Arusha ilipendekeza Wizarani barabara ya Njiapanda - Mangola - Matala katika Wilaya ya Karatu ipandishwe daraja kuwa barabara ya mkoa, je, utaratibu huo sasa utanza lini? Ni kwa sababu zipi za msingi zinazofanya maamuzi haya yachukue muda mrefu kutekelezwa?

Kwa vile Mheshimiwa Rais/Waziri wa Ujenzi siku ya tarehe 14 Aprili, 2005 aliahidi kutoa shilingi 100,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa daraja la Baray, je, katika kifungu cha Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2005/2006 *Vote 47* fedha hizo zinaonekana wapi? Mheshimiwa Waziri anaweza kutuhakikishia kama haziko kwenye vote hii, kuwa fedha hizo zitapatikana ili darja hilo muhimu liweze kujengwa? Na je, kazi sasa itanza lini?

Mheshimiwa Spika, natanguliza shukrani zangu za dhati.

**MHE. PROF. HENRY R. MGOMBELO:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kutoa rambirambi kwa familia na ndugu wa Marehemu Mheshimiwa Abu Kiwanga na Mheshimiwa Margareth Bwana. Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, Wizarani ya Ujenzi ni muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu. Naipongeza sana Serikali kwa juhudi madhubuti za kujenga barabara za nchi hii.

Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza suala la ujenzi wa barabara, kwa vile fedha zetu hazitoshelezi, nashauri Wizarani ya Ujenzi ije na mpango wa ujenzi wa barabara zote muhimu nchini. Barabara hizo ni zile zinazokwenda bandarini (kwenye maziwa na bahari ya Hindi) na nchi jirani. Ni dhahiri kuwa mpango huo utaonyesha kuwa fedha nyingi zitahitajika. Katika kutafuta pesa za miradi nashauri tutumie pia ule utaratibu wa *Build Operate Transfer, (BOT)* kwa baadhi ya barabara muhimu. Utaratibu huu ni mzuri sana maana unaiondolea mzigo Serikali katika kujenga na kuzihudumia barabara.

Mheshimiwa Spika, naomba niendeele kuiomba Serikali izikumbuke barabara zitakazoufungua Mkoa wa Tabora. Barabara hizo ni ile ya Manyoni - Itigi - Kigwe - Tabora; Tabora - Urambo - Kigoma; Nzega - Tabora, Tabora - Sikonge - Mbeya na Tabora - Sikonge - Mpanda - Sumbawanga. Barabara hizi ni muhimu sana kwa maendeleo ya Mkoa wa Tabora. Naomba Serikali itueleze ni lini barabara hizi zitajengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, naipongeze Bodi ya Usajili wa Makandarasi (*CRB*) kwa kazi nzuri wanayoifanya. Kwa vile nchi yetu ni kubwa sana, naiomba Serikali iwawezeshe *CRB* ili waweze kukagua utendaji kazi wa makandarasi wote wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba pia Serikali iwasimamie kwa ukaribu sana makandarasi wa barabara ili ahadi ya Serikali kwamba hivi karibuni tutaweza kuendesha gari dogo kutoka Mtwara hadi Mwanza iweze kukamilika mapema iwezekanavyo. Pia, matatizo yanayopelekea ucheleweshaji huo yatatuliwe mapema.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara ya Ujenzi ijenge uzio kwenye nyumba mpya inazozijenga ili zisionekane kama makambi. Kwa nyumba zinazojengwa hapa Dodoma karibu na Redio Mwangaza, nashauri mabati yapakwe rangi ili yaweze kutoa mandhali nzuri.

Mheshimiwa Spika, vile vile, ugawaji wa nyumba za Serikali uwe wa uwazi zaidi na kasoro zilizojitokeza zishughulikiwe mapema.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. PROF. PIUS P. MBAWALA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Hata hivyo, ninayo yafuatayo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kuhusu barabara ya Mtwara -Pachani - Lusewa hadi Magazini na Likusenguse.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa msaada wa fedha za kujenga madaraja na njia hii hadi sasa imefika Likusenguse, lakini kumetokea mmomonyoko katika barabara hii. Mmomonyoko huo unatokana na mvua kati ya Mtwara Pachani na Lusewa Kijijini, nyasi hazijafyekwa kati ya Mtwara - Pachani hadi Lusewa hivyo barabara ni nyembamba mno, changarawe hazijawekwa kati ya Mto Makong'otela na Kijijini Likusenguse.

Mheshimiwa Spika, vibarua wa Kampuni ya Legele hawajalipwa mishahara yao kwa kazi waliyofanya kati ya Kijiji cha Magazini na Likusenguse tangu Januari, 2005 hadi sasa.

Mheshimiwa Spika, je, ni lini barabara hiyo itaendelezwa kati ya Likusenguse hadi Sasawala darajani ambako sasa wananchi wamehamia toka Wilayani Tunduru?

Mheshimiwa Spika, kwa nini upana wa barabara kati ya Magazini na Likusenguse ni nyembamba sana kuliko ile barabara inayotoka Magazini kuja Ligunga Kijijini?

Mheshimiwa Spika, pili, ni kuhusu barabara na daraja kati ya Kijijini Kitanda - Namtumbo - Daraja Ilondo hadi Kijijini Kilosa kwa Mpepo. Barabara hii ni kiungo muhimu sana kati ya Mkoa wa Ruvuma (Lumecha hadi Kitanda) na Kilosa kwa Mpepo hadi Kijiji cha Lupilo Mkoani Morogoro (Wilaya ya Ulanga). Barabara ya Lumecha hadi Kitanda tayari ni barabara ya Mkoa (Ruvuma). Aidha, barabara kati ya Lupilo hadi Kilosa kwa Mpepo ni barabara ya Mkoa (Morogoro).

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni kupata fedha za ujenzi kujenga Daraja la Ilondo, ili kusudi kuunga Mikoa hii miwili. (Ruvuma na Morogoro). *TANROADS* wanakamilisha kufanya *design* na gharama yake inakisiwa kuwa shilingi bilioni 306. Hii haihusu ujengaji tuta la barabara ambalo *Selous Conservation Programme* watagharimia kati ya barabara ya Kitanda hadi Ilondo Darajani. Tafadhali tupewe hizo shilingi milioni 306 katika bajeti ya mwaka 2005/2006. Tayari ujenzi Ruvuma wanapata shilingi milioni 60 za kufanyia *design* inayokamilishwa sasa.

Mheshimiwa Spika, faida ya barabara hii kupitia Mto Ilondo ni kuunganisha Mikoa ya kati ya Mkoa wa Ruvuma (Wilaya ya Namtumbo) na Mkoa wa Morogoro (Wilaya ya Ulanga). Hadi sasa Halmashauri ya Namtumbo na Halmashauri ya Ulanga tumekuwa na mikutano ya pamoja na njia hii ni muhimu tangu mwaka 2002. Mimi ni Makamu Mwenyekiti na Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa (Mbunge) ni Mwenyekiti (toka Halmashauri ya Ulanga).

Mheshimiwa Spika, barabara hii itarahisisha utalii na hifadhi ya Selous, watalii hao wakitokea *Mikumi National Park*.

Pia barabara hii itarahisisha usafiri kati ya Namtumbo na Songea hadi *Mikumi National Road* kwa kupitia Ifakara, pia barabara itapunguza gharama za kusafirisha mazao ya chakula na biashara (mbao) badala ya kupitia kwanza Njombe na Iringa hadi Mikumi ambako ni mzunguko mrefu usiokuwa na faida.

Mheshimiwa Spika, barabara hii itaendeleza barabara ya *TANZAM Corridor* kutoka Ifakara hadi Songea kupitia Lupilo - Kitanda na Lumecha.

Mheshimiwa Spika, kufunguliwa kwa barabara ya Kitanda - Lupilo kutairahisisha Wizara ya Kilimo na Chakula kuendeleza kilimo cha *irrigation* kati ya Kijiji cha Kitanda na Mto Ilondo hivyo kuzalisha nijiunge katika hekta 6,000. Kwa kufanya hivyo tutakuwa tumetekeleza mpango wa MKUKUTA katika Wilaya ya Namtumbo.

Aidha, ng'ambo ya Mto Ilondo yapo mabonde mazuri ya kilimo cha *irrigation* ambayo Halmashauri ya Ulanga inasubiri kuyaendeleza.

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.



Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Wizara hii hasa kwa ujenzi wa barabara ya lami Mwanza - Dodoma ambayo tangu tumejitawala ilikuwa ndoto. Kazi inaendelea vizuri sana na watu wote wanapongeza sana umahiri wa Wizara hii kwa utekelezaji wa miradi yake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu fedha za *road toll* kuwa haziruhusiwi kujenga madaraja, naomba Wizara hii itutafutie fedha za kujenga madaraja ya Ndala na Mshikamano kwa gharama ya shilingi milioni 250. Hii itasaidia kuunganisha baadhi ya Kata za Ndala, Ngokolo (Mshikamano) na Mji wa Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, nawatakia kheri kwa utekelezaji wa malengo waliyojiwekea.

Mheshimiwa Spika, Mola awabariki watendaji wote wa Wizara ya Ujenzi.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, tafadhali sana tena sana.

Mheshimiwa Spika, napenda kumwambia Mheshimiwa Waziri kwamba, mimi na Marehemu Mheshimiwa Abu Kiwanga tuliomba baada ya kushauriwa na wewe mwenyewe kwa maandishi *extension* ya *Regional Road* kati ya Taweta - Lupembe ili kuhudumia Mikoa ya Ruvuma, Iringa na Morogoro. Tayari Njombe - Lupembe na Mlimba - Taweta ni *Regional Roads*. Mtaalam wake Mfugale anajua kwa undani suala hili tumefikia wapi katika ombi letu.

Mheshimiwa Spika, pili, barabara ya Njombe (Kibena) - Lupembe ni *Regional Road*. Haina fedha kwa miaka miwili sasa. Ilikuwa chini ya mradi wa *RUSM* na fedha za wahisani zilitolewa isipokuwa fedha za ndani. Barabara hii imechakaa kutokana na kukosa fedha, pamoja na kupitiwa na magari mengi ya chai na mbao. Tafadhali itengewe fedha mwaka huu.

**MHE. PROF. JUMA A. KAPUYA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wake na Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi kwa hotuba yao nzuri ambayo imetupatia matumaini ya kuwa na barabara ya lami sisi wananchi wa Kaliua. Pia, naomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kutupatia shilingi milioni 50 za kukarabati barabara ya Kaliua - Uyowa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na shukrani hizi naomba tuongezewe shilingi milioni 100 ili tuifikishe barabara hii hadi kwenye barabara iendayo Rwanda kwa kupitia Kahama. Tukifanikiwa, barabara hii itakuwa ni moja ya barabara muhimu za Mikoa ya Tabora na Shinyanga kwa kuunganisha wananchi wake wa Mikoa hii miwili na pia itakuwa ni mhimili muhimu wa kufufua na kuimarisha uchumi wa maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. SHAMSA S. MWANGUNGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza natoa pongezi kwa Waziri, Mheshimiwa John Magufuli na Naibu Waziri wake Mheshimiwa

Hamza Mwenegoha kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara ya Ujenzi. Ni Wizara ya uhakika na isiyotetereka kwa ajili ya uongozi wao mzuri.

Mheshimiwa Spika, pili, naipongeza bajeti hii ni nzuri na iliyotilia maanani maeneo mengi ya muhimu. Naunga mkono bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, tatu, napenda kuchangia kama ifuatavyo kuhusu barabara za Mkoa wa Dar es Salaam na hususan barabara zinazounganisha maeneo ya *Mbezi Beach*, Kunduchi, Tegeta hadi Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, usafiri wa kutoka katikati ya jiji kwenda maeneo haya niliyoyataja ni kero na usumbufu mkubwa kwa ajili ya msongamano usiopungua na usioepukika. Ni muda mrefu wasafiri wa aina zote aidha, magari binafsi au mabasi wanasota kwenye barabara hii hadi kufika makwao au kwenda kazini.

Mheshimiwa Spika, barabara zitumikazo ni mbili tu ikiwamo ya Ali Hassan Mwinyi na ile ya *Old Bagamoyo Road*. Barabara hizi hazitoshi kwani ni nyembamba za mstari mmoja tu. Kwa hali hiyo, foleni inakuwa ndefu na fujo nyingi zinakuwemo na mara nyingi wanasababisha ajali na kusitisha kabisa magari kupita. Wananchi wa maeneo hayo wamechoshwa na kero hiyo. Kwa hali hiyo nauliza yafuatayo: -

Je, hakuna uwezekano wa kupanua barabara hizi mbili ziwe njia za mistari miwili badala ya moja?

Mheshimiwa Spika, ni lini madaraja mawili yaliyoko kwenye *Old Bagamoyo Road* yatajengwa kiuhakika kwa kuyapanua na kuyajenga kwa udhibiti badala ya sasa ambapo daraja la Mlalakuwa limejengwa kwa mabati na ni jembamba na lina uwezo wa kupitisha gari moja, moja tu?

Je, kuna uwezekano gani wa kuanzisha *Commuter Trains* kama nchi za Ulaya ambapo hiyo ni njia mojawapo ya kutatua kero ya msongamano wa abiria. Je, Wizara iko tayari kujenga reli?

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nachukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji na wafanyakazi wote wa Wizara ya Ujenzi kwa hotuba hii nzuri ya Mheshimiwa Waziri, hotuba ambayo iko wazi na inayogusa sehemu zote za ujenzi zilizopo katika Wizara hii ya Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, pia nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri iliyojaa usimamizi imara wa shughuli na kazi za Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, ni jambo lililo wazi kuwa Wizara hii inafanya kazi zake kwa ufanisi mkubwa katika maeneo yote hususan ya barabara na kadhalika. Kwa kweli ujenzi wa barabara zinazojengwa hivi sasa hapa nchini katika Mikoa na Wilaya mbalimbali inadhihirisha ufanisi mkubwa wa kiutendaji wa Wizara hii na kwa Serikali yetu ya

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa Chama chetu cha Mapinduzi ambacho ndicho kilichoweka Ilani yake ya Uchaguzi ya mwaka 2000 ambayo hivi sasa inatekelezwa na Serikali yetu kupitia Wizara zake ikiwa ni pamoja na Wizara hii ya Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri inadhihirisha uimara wa Serikali yetu ya CCM katika kujenga misingi mikuu ya maendeleo ya nchi yetu na kwa wananchi wote wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni muhimu sana na yenye kuthibitisha ujenzi ulio thabiti wa maendeleo ya Taifa letu hili la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama imetembelea karibu mipaka yetu ya nchi isipokuwa mpaka wa Ruvuma. Tumeshuhudia ukubwa wa nchi yetu, pia tumeona urefu wa barabara zetu kutoka Wilaya moja kwenda nyingine na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli kutokana na ukubwa wa nchi yetu bado tunayo kazi kubwa ya kulijenga Taifa letu. Tuongeze umoja na mshikamano ili tuweze kuyafikia malengo yetu tunayopanga kwa maendeleo sahihi ya nchi yetu na watu wake wote.

Mheshimiwa Spika, pia tunaipongeza Wizara ya Ujenzi kwa uamuzi wake wa kujenga nyumba za viongozi mbalimbali wa Serikali hapa nchini. Naomba juhudi hizi ziendelezwe vizuri na kwa haraka sana ili kuondoa tatizo hili la nyumba za kukaa viongozi wa watumishi mbalimbali wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, pia naipongeza Wizara ya Ujenzi kwa kuweka wataalam wazalendo kutoka Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kujenga nyumba hizi za viongozi wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, pia katika mchango wangu huu nitazungumzia ujenzi wa barabara yetu ya Mkoani Pemba. Barabara hii ambayo ilifunguliwa rasmi na Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Amani Abeid Karume, siku ya tarehe 08 Januari, 2005 iligharimu shilingi bilioni 6.4.

Mheshimiwa Spika, nikinukuu hotuba ya Mheshimiwa Rais Amani Abeid Karume, aliyoitoa siku hiyo ya ufunguzi wa barabara hiyo alisema kuwa: “Wakati wa kampeni mwaka 2000 Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa aliwaambia wananchi waliohudhuria mkutano huo kuwa tatizo la barabara hii lipo mikononi mwetu. Aliwahakikishia wananchi na kuwaambia watupigie kura Chama cha Mapinduzi kitajengwa barabara hii.”

Mheshimiwa Spika, ni kweli barabara hii imejengwa kwa kiwango cha lami na tayari imefunguliwa rasmi na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar tarehe 08 Januari, 2005.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa, Chama cha Mapinduzi pamoja na Serikali zetu zote mbili yaani Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ujenzi wa barabara hii ambayo ilikuwa katika hali mbaya sana kwa miaka mingi.

Mheshimiwa Spika, pia naiomba Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuongeza misaada kujenga barabara za Pemba na Zanzibar kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nataka kuchangia katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi ni kuangalia tena ombi langu ambalo nilishampelekea mnamo mwaka 2001 na kwa kweli alilipokea vizuri na kujaribu kulitolea maelekezo mazuri, lakini huyo aliyeelekezwa ndiye aliyenikwamisha kutofanikiwa.

Mheshimiwa Spika, ombi langu lilikuwa ni juu ya barabara zangu za Vitongoji zenye urefu wa kilometa 24 tu.

Mheshimiwa Spika, barabara hizi ni ile iliyoanzia Vitongoji - Vikutani kupitia Vitongoji Uwandani/Ole - Kianga, barabara iliyoanzia Vitongoji - Mzambarau Mboko/Vikunguni/Wawi Matrekta na barabara iliyoanzia Uwanja wa Mpira Gombani/Ng'ambwa/Ole.

Mheshimiwa Spika, mbali ya kuwa barabara hizi zitajenga sura na msingi mizuri ya kimaendeleo katika eneo letu la Vitongoji, barabara hizi ni muhimu kiusalama katika kisiwa chetu cha Pemba.

Mheshimiwa Spika, barabara hizi pia ni kiungo muhimu sana kati ya Wilaya yetu ya Chake Chake na Wilaya ya Wete na pia Mkoa wetu wa Kusini Pemba na Kaskazini Pemba.

Mheshimiwa Spika, pia natoa shukrani na pongezi nyingi kwa Kamati ya Miundombinu ya Bunge kwa kufanya ziara katika Kisiwa cha Pemba tarehe 03 Juni, 2005 na kutembelea baadhi ya maeneo katika Kisiwa hiki cha Pemba.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali yetu ya Muungano kutoa fedha na misaada mingi na itakayoweza kujengwa kwa kiwango cha juu gati yetu na Mkoani Pemba na pia ninaomba tujengewe gati yetu ya Weshi, Pemba.

Mheshimiwa Spika, narudia kumpongeza Mheshimiwa Waziri na naunga hoja mkono kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tatu kwa mafanikio makubwa ya maendeleo katika uchumi, huduma za uchumi ikiwemo barabara, madaraja na umeme, pamoja na huduma za jamii ikiwemo elimu, afya na huduma nyingine. Mafanikio haya yametokana na mshikamano wa Serikali nzima iliyotayarisha mipango na mikakati bora ya utekelezaji wa Sera sahihi ya Chama Tawala CCM.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Mbinga Magharibi nampongeza Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, Makamu wa Rais Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Fredrick Tluway Sumaye, Waheshimiwa Mawaziri, Manaibu Waziri na watendaji wote wa Serikali kwa maendeleo yaliyopatikana katika kipindi cha Awamu ya Tatu.

Mhesheshimiwa Spika, vile vile nitumie nafasi hii kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wataalam na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri ya matengenezo ya barabara, madaraja na ununuzi wa vivuko. Matengenezo ya barabara pamoja na madaraja yaliyofanyika na yanayoendelea kufanyika pia yatakayofanyika nchi nzima, Kaskazini, Kusini, Mashariki na Magharibi. Matokeo haya mazuri yaliyopatikana ni mipango mizuri ya maendeleo ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, kwa yale yaliyofanyika mwaka 2004/2005 na yote yatakayofanyika katika mwaka 2005/2006. Kwa niaba yangu mwenyewe naunga mkono kwa asilimia mia moja hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo yafuatayo ni maombi yetu tunaomba yapewe uzito unaostahili kwa utekelezaji.

Kwanza, barabara ya Chiwindi hadi Lituhi imetengenezwa sehemu sehemu kama ifuatavyo, kutoka Nangombo hadi Ng'ombo ilitengenezwa mwaka 2002/2003 na mwaka 2004/2005 na 2005/2006 Wizara imetenga shilingi milioni 170. Fedha hizi naamini zitatosha kutengeneza sehemu iliyobaki hadi mpakani na sehemu ya kutoka *Mbamba Bay* hadi Lituhi.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya *Mbamba Bay* hadi Liuli imetengenezwa mwaka 2002/2002, mwaka 2004/2005 na 2005/2006 Wizara imetenga shilingi milioni 148. Fedha hizi zitatumika kutengeneza kutoka Liuli hadi Liundi Kata ya Ngumbo.

Kutokana na hali hii barabara ya *Mbamba Bay* hadi Lituhi zitabaki kilometa 20 kufika mwisho wa barabara yaani Lituhi. Tunaomba sana Wizara ifanye kila liwezekanalo ili kilometa 20 zilizobaki zitengenezwe kabla ya kipindi hiki cha Awamu ya Tatu kuisha. Kama maombi haya yatakamilika, basi itasaidia sana kukamilisha ahadi ya Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa aliyowaahidi wananchi wakati wa ziara yake Wilaya ya Mbinga.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kitai hadi Lituhi matengenezo yamekamilika lakini bado madaraja nane kutengenezwa. Tunaomba madaraja hayo yatengenezwe.

Naishukuru Wizara kwa kutenga fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara ya Kigonsera hadi Mbaha. Kata ya Mbaha iko kisiwani haifikiki, hivyo hali hii inaathiri sana maendeleo ya uchumi na ya kijamii. Kama mradi huu utakamilika utaleta mapinduzi makubwa ya maendeleo katika Kata ya Mbaha.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mbinga hadi Ngumbo kwa mwaka 2005/2006 itafanyiwa matengenezo. Tunaomba sana mpango huu ukamilike kama mlivyopanga.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naishukuru Wizara kwa kutenga shilingi milioni 500 kutoka Mfuko wa Barabara kwa ajili ya kununulia kivuko kipya chenye uwezo wa kubeba tani 50 kitakachopelekwa Mto Ruhulu. Mradi huu ukikamilika utapunguza kero za watu wa Mbinga na Ludewa.

Mheshimiwa Spika, naipongeza na kuishukuru tena Serikali ya Awamu ya Tatu kwa kufanikisha matengenezo ya barabara, madaraja na kwa ununuzi wa vivuko.

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI:** Mheshimiwa Spika, kabla ya yote naomba nitoe salaam za rambirambi kwa ndugu, jamaa na hasa akinamama wa Mkoa wa Rukwa kwa kifo cha Mbunge Mheshimiwa Margareth Bwana, Mungu ailaze pema roho ya marehemu. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa John Pombe Magufuli, Waziri wa Ujenzi, Naibu wake, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha na watendaji wa Wizara hii kwa mambo mawili yafuatayo: -

Kwanza, usimamizi madhubuti wa ujenzi kwa kuwa umekamilika tayari na sasa Makandarasi wanaweka alama muhimu za baraka wana Nzega na Igunga tunawashukuru sana.

Pili, tunaishukuru Wizara ya Ujenzi na Serikali kwa ujumla kwa kuwaunga mkono Wakuu wa Mikoa ya Tabora na Singida kwa mradi waliobuni na kuanza kuutekeleza tena fedha zilizochangwa na Halmashauri zetu. Mradi wa barabara ya kuunga Manyoni na Tabora kupitia Itigi - Igalula hadi Tabora Mjini. Wizara imeanza kutoa fedha. Tunaomba tu fikra za kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami hadi Kigoma zianze kuzingatiwa.

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni kwamba Tabora ni Makao Makuu ya Mkoa usioundwa na Mji mwingine wowote wa Mkoa. Tabora - Mbeya hatuungani, Tabora - Singida hatuungani, Tabora - Shinyanga hatuungani. Tunaomba mawazo ya kutoa kifungoni Mji huu mkongwe wa Mikoa inayouzunguka.

Mheshimiwa Spika, ndani ya Mkoa wenyewe kuna baraka ambazo zinapoteza umuhimu wake sababu magari yanazikwepa japo ni fupi sababu tu zimetelekezwa *TANROAD*. Barabara ya Nzega - Kahama kupigia Igusule imeachwa, magari yanazunguka kupitia Tinde. Je, unaona mzunguko huo?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri ya Wizara, nashauri yafuatayo: -

Kwanza, Wizara itekeleze ahadi yake ya kujenga barabara za ulinzi na usalama mipakani. Kwa Jimbo la Buyungu, barabara hiyo ni Bitale - Katanga - Gwanumpu - Bukiliro - Kasongati - Kiga - Kasuga - Nyakayenzi - Muhange mpakani Burundi na Muhange - Kabare - Rumashi - Nyabibuye hadi Murusagamba.

Pili, kwa kuwa asilimia 70 ya Wilaya ya Kibondo ni hifadhi ya Muyovozi na maeneo ya maji (*wetlands*), nashauri Serikali ikubali kujenga barabara nyingi za Wilaya hii chini ya *TANROADS* ili Wilaya ipate mgao wa kutosha kutoka mgao wa Taifa.

Tatu, tumekuwa tunasikia mipango mizuri ya barabara ya Kigoma - Nyakanazi kwa miaka kadhaa sasa, ni vyema kazi ianze ili watu tuone kuwa si ahadi tu, kwani imekuwa inawekwa kipaumbele miaka mingi bila kazi kuanza.

**MHE. CHARLES H. KAGONJI:** Mheshimiwa Spika, naomba unipatie fursa ndogo niwape pole sana familia , ndugu , marafiki na akinamama wa Mkoa wa Rukwa kwa kumpoteza mpendwa wao na Mbunge mwenzetu; Mheshimiwa Margareth Bwana, ambaye alifariki hivi majuzi. Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, katika mkutano huu huu niliuliza swali kuhusu barabara za Jimbo langu la Mlalo. Niliuzia barabara ya Mlalo - Lushoto, Malindi - Nkelei na Lukozi - Manolo - Mtae. Majibu ya Wizara yalikuwa mazuri ya kutosha na kwa kiwango fulani barabara hizi zinatengenezwa zile sehemu korofi mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo hoja yangu ni kwamba barabara hizi zilipata ajali mara mbili. Mara ya kwanza ni mwaka 1993 tulipopata mafuriko na maporomoko ambako barabara hizo katika Jimbo langu zilipoteza kiwango kikubwa cha changarawe.

Pili, mvua nyingi na za muda mrefu za *El-Nino* nazo ziliondoa sehemu kubwa ya changarawe kiasi kwamba sasa barabara hizo zinageuka kutoka za changarawe kurudi kuwa za udongo.

Mheshimiwa Spika, nasisitiza kwamba kama barabara hizi ambazo toka zamani za Mkoa kwa kiwango cha changarawe zifanyiwe kazi zisirudi kuwa za vumbi. Barabara hizi zinastahili kupewa kipaumbele cha kwanza kwa kurudishiwa changarawe kuliko kufikiria kuwekewa changarawe barabara mpya.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mkomazi - Mnazi hadi Mung'aro ni ya Mkoa pia ambayo tulikubaliana kuwa ya Mkoa miaka michache iliyopita. Barabara hii ambayo ina mpaka mrefu sana na nchi jirani pia ikiwa inapakana na Mbuga ya Wanyama ya Mkomazi/Umba ni muhimu sana kwa wakazi wa Tarafa ya Umba na pia kwamba ni barabara ya usalama. Naomba jitihada za kuitengeneza ziendelee.

Mheshimiwa Spika, katika barabara hiyo ya Mkomazi - Mnazi - Mng'ara, ndipo palipo na daraja la Mkundi ninaloomba lijengwe mara kwa mara. Daraja hili inaelekea

halina bahati sana ya kutengenezwa. Kila daraja hili linapochelewa kupewa fedha gharama ya ujenzi wake inazidi kuwa kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, naishukuru sana Wizara kwa kuanza kulitengea fedha daraja hili. Mwaka wa juzi lilitengewa shilingi 100,000,000/= mwaka wa jana shilingi 50,000,000/= tunaipongeza sana Wizara ya Ujenzi. Hata hivyo daraja hili linahitaji shilingi 300,000,000/= na mwaka huu bado sijaona kitu. Tafadhali sana Waziri John Magufuli tusaidie. Hivi zile fedha tulizopatiwa jumla ya shilingi 150,000,000/= ziko wapi kwa hivi sasa maana sioni kazi yeyote inavyofanyika pale. Ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. Nawapongeza viongozi na watendaji wa Wizara hii kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya katika utengenezaji wa barabara katika kila kona ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Wilaya ya Manyoni, tushukuru sana Wizara kwa mradi wa barabara ya lami kati ya Dodoma - Manyoni na ile ya Manyoni - Singida. Hata hivyo tunaomba Wizara itusaidie yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, barabara ya Manyoni - Heka - Ikasi (kilometa 122) - ukurasa wa 148, barabara hii sehemu haipitiki nyakati za masika na ni tatizo kubwa kabisa kibarabara katika Jimbo langu la Manyoni Mashariki. Ilani ya Uchaguzi ya CCM iliahidi kutengeneza barabara muhimu za vijijini kama hii, lakini bahati mbaya kabisa barabara hii iliachwa katika mpango wa matengenezo ya barabara zilizoharibiwa na *El-nino* (ADB - page 153). Katika kiambatisho namba 6 (page 148) barabara hii haikuwekewa fedha kwa mwaka 2005/2006. Maana yake ni kwamba kero hii itaendelea. Tunaomba sana barabara hii ipewe fedha na itengenezwe/ikarabatiwe ili iweze kupitika hata nyakati za masika. Barabara hii inahudumia Kata 5 zenye kilimo kikubwa, ambao asili na utengenezaji wa chumvi. Ni eneo muhimu kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya Dodoma - Manyoni - Singida, barabara hii inapofika eneo la Manyoni Mjini, kwa *design* ya sasa itapitia pembeni kidogo ya Mji. Ombi letu ni kwamba Wizara ifanye mipango ili mkandarasi aweke lami kipande cha barabara ya sasa inayopita katikati ya Mji wa Manyoni. Vile vile kipande cha barabara kutoka katikati ya Mji Manyoni kwenda kwenye stendi ya mabasi itakayokuwepo kwenye barabara mpya, nacho kiwekwe lami.

Mheshimiwa Spika, narudia tena kusema naunga mkono hoja hii.

**MHE. DR. MAUA A. DAFTARI:** Mheshimiwa Spika, ninalo wazo dogo la kuchangia nalo ni pale wahandisi wanapoamua kujenga madaraja basi kabla ya kujenga wawasiliane na wahandisi wa reli kwani maji yanaelekezwa katika reli na kuharibu reli sana katika baadhi ya maeneo. Naomba hili lifikiwiwe.

Mheshimiwa Spika, naona sasa ni wakati muafaka wa kufikiria ujenzi wa *highway* ili kupunguza *congestion* mijini badala ya kufunga barabara. Wataalam tunao.



Mheshimiwa Spika, napenda kuwapa hongera kwa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya. Ili barabara zidumu lazima reli ziboreshwe na kufanya kazi. Je, lini watatumegea *road fund* ili tuboresha bili zetu?

**MHE. HALIMENSHI K. R. MAYONGA:** Mheshimiwa Spika, barabara ya Mwandiga - Manyovu haina jibu sahihi na la ukweli tangu mwaka 1990 mpaka leo 2005.

Mheshimiwa Spika, ni sehemu ya kilometa 10 tu ambazo zimetengenezwa kati ya kilometa 52. Hizo barabara nyingine katika Mkoa wa Kigoma, barabara ya Mwandiga - Manyovu ndiyo ya wazalishaji wa kuu katika Mkoa wa Kigoma. Barabara hii inakwenda nchi jirani za Burundi, Rwanda na Kongo (*DRC*).

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2004, Wizara ilichokiahidi kwa barabara ya Mwandiga - Manyovu ni lami ya *water seal*. Mpaka sasa wimbo wa mwaka huu ni ukosefu wa fedha na ahadi ni hii hii. Naona barabara hii imetengenezwa kilometa 5 tu kwa changarawe (Mlima Kasagamba). Sehemu nyingine za barabara hii ni mbaya sana. Uongozi wa Mkoa unajua kama barabara hii ni mbaya. Nimeisemea tangu mwaka 1990,1995, 2000, 2005 bila mafanikio ya uhakika. Nasubiri jibu.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga hoja hii mkono kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza sana Mheshimiwa John Pombe Magufuli na Mheshimiwa Hamza Mwenegoha. Kazi imefanyika vizuri sana katika Mkoa wetu wa Iringa.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa Wizara hii kusikia kilio changu cha barabara ya Ilula - Kilolo cha kuitengea fedha kwa mwaka huu wa fedha. Mwenyezi Mungu awabariki Mheshimiwa John Magufuli na Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, waweze kurudi tena.

Mheshimiwa Spika, kwanza niwapongeze *TANROAD* Iringa kwani wamefanya kazi hii ya ujenzi wa barabara zetu za Iringa vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kwa kuwa wananchi wameanza kazi ya kuchimba barabara ya kuunganisha na Mkoa wa Iringa na Morogoro tayari wamechimba kilometa 16 na wameshaunganisha. Tungeomba Serikali itusaidie ili nayo pia ipewe hadhi ya Mkoa kwani inapita Iringa - Idete - (Muhanga - Mbingu) - Kilombero, hivyo chonde sana.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajibu hoja zetu, angalau mwisho aitaje hii barabara ya Ilula - Kilolo. Ahsante.

**MHE. MIZENGO K. P. PINDA:** Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali hatimaye kwa kuamua kukarabati barabara ya Mpanda - Inyonga - Kogo ili kupunguza

kero ya wananchi wa eneo hilo, hata hivyo Mkandarasi Badri anapunguza kasi ya ukarabati. Nashauri jukumu la kukarabati barabara hii apewe Bwana Mselem ambaye sasa anaitengeneza kama *sub-contractor*.

Mheshimiwa Spika, lini Serikali itatengeneza barabara na madaraja ya kati ya Sitalike na Kilimatinde. Barabara hii inahudumia Tarafa ya Mpimbwe yenye wakazi zaidi ya 75,000 wengi wao ni wakulima na wafugaji wakubwa.

**MHE. JUMA S. KIDUNDA:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze mchango wangu kwa kumpongeza sana Mheshimiwa John Magufuli, Naibu wake Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, pamoja na timu yote ya wataalam wa Wizara ya Ujenzi ikiongozwa na Katibu Mkuu makini sana Ndugu Kijazi.

Mheshimiwa Spika, tukiangalia kazi kubwa iliyofanywa na Wizara hii nashawishika kushauri kuwa timu hii ya wanasiasa na wataalam ibaki kama ilivyo katika awamu ya nne.

Mchango wangu unahusu maombi yanayoihusu Wilaya yangu mpya ya Kilindi kuhusiana na mtandao wa barabara zilizo chini ya usimamizi wa Mkoa.

Mheshimiwa Spika, sababu kubwa iliyoifanya Serikali ianzishe Wilaya ya Kilindi ni kuwa eneo hili halikuwa na mtandao mzuri wa barabara pamoja na kupakana na Mikoa minne na kuwa Kilindi ndicho kiungo cha Mkoa wa Tanga na Mikoa hiyo.

Mheshimiwa Spika, mtandao wa barabara ambao tumeupendekeza katika vikao vya Mkoa kuwa za Mkoa Wilayani Kilindi ni hizi zifuatazo:-

Kwanza, Handeni - Muungano - Kibirashi - Songe - Kwekivu - Kikunde hadi Gairo (Wilaya ya Kilosa ambako inaungana na lami ya Dodoma - Dar es Salaam, pili, Kwekivu - Lwande - Kimbe - Mziha, tatu, Kimbe - Misufini - Kwedikundi - Muungano, nne Kibirashi - *Manyara border* na tano, Mziha - Negero - Handeni.

Mheshimiwa Spika, barabara hizi zina sifa za kuwa za Mkoa kama tulivyozichuja katika vikao vya Kamati ya Maendeleo ya Mkoa. Aidha, barabara hizi zimekaa vyema kupokea mawasiliano na barabara ambazo zilikosa sifa za kuwa za Mkoa ambazo tulizibakiza kuwa Wilaya na ijiji.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nieleze kuwa bandari ya Tanga haitumiki ipasavyo kwa vile hakuna barabara fupi inayoiunganisha na bara. Napendekeza barabara ya Korogwe - Handeni - Songe ambako ni Makao Mkuu ya Wilaya - Kikunde hadi Gairo iwe Barabara Kuu inayoiunganisha bandari ya Tanga na barabara kuu inayokwenda na kutoka bara kupitia Gairo na Dodoma. Umbali wa kutoka Gairo kwenda Tanga na Gairo kwenda Dar es Salaam ni sawa. Hivyo mizigo ya kwenda bara inaweza kupitishiwa katika bandari ya Tanga.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa barabara niliyoitaja utaonekana endapo itaainishwa katika ramani. Barabara nyingine inayounganisha bandari ya Tanga na Mikoa ya bara ni ile inayopitia Kibaya hadi Singida kupitia Kibirashi (Kilindi) ambayo kwa sasa hutumika kwa shida kwa sababu ya kuwa na ubora mdogo.

Mheshimiwa Spika, naomba pia niombe Serikali iruhusu matumizi ya *Force Account* katika kutengeneza barabara kwa Wilaya ambazo ziko mbali na maeneo ya miji mikubwa ambako ndiko makandarasi na zana za kutengeneza barabara ziliko. Hoja hii ni muhimu kwa vile fedha zinazotolewa kwa Halmashauri ni chache na haziwavutii makandarasi wazuri kuomba.

Mheshimiwa Spika, wanaoomba ni wale dhaifu ambao wakipewa, hufanya kazi hafifu. Pamoja na ombi la matumizi ya *Force Account*, naomba Serikali ifikirie kuziwezesha Halmashauri za Wilaya zilizo mbali na miji mikubwa kupata mitambo ya kutengenezea barabara.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kuiunga mkono bajeti hii kazi nzuri inayoifanya iendelee.

**MHE. DR. PIUS Y. NG'WANDU:** Mheshimiwa Spika, barabara ya Ngorongoro - Lalago - Maswa - Bariadi - Ramadi - Musoma itakamilika lini? Mbona haionekani katika mipango? Kwa ujumla hongera sana. Nchi imeshuhudia mabadiliko makubwa sana katika kipindi hiki cha 2000- 2005.

**MHE. RAMADHAN H. KHALFAN:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani za dhati sana kwa Waziri wa Ujenzi Mheshimiwa John Magufuli, Mbunge, Naibu Waziri wa Ujenzi Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Mbunge. Katibu Mkuu Ndugu *Engineer* John Kijazi, wataalam wa Wizara ya Ujenzi na wengine wote waliochangia kwa njia moja au nyingine katika kukamilisha maandalizi ya hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kuiwasilisha vizuri sana hotuba yake hiyo ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, nimeipokea kwa furaha kubwa na naiunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, katika kitabu cha hotuba ya Waziri ukurasa wa 127 kiambatisho Na.4 (i) Wizara imetenga jumla ya shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa kilometa 2 za barabara za Mjini Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuelewa ufinyu wa Bajeti yetu Kitaifa na kwa niaba ya wakazi wa Mji wa Bagamoyo, napenda kuishukuru sana Serikali, Wizara ya Ujenzi na hasa Waziri wa Ujenzi. Kwa nia hii njema waliyoionyesha katika kuujenga Mji wetu wa kale wa Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuendelea kuishukuru Serikali na Wizara kwa kutenga jumla ya shilingi milioni 100 kwa ukarabati wa Daraja la zamani sana la Makofia

(shilingi milioni 60) na Daraja kuu la muda la Kigongoni Mto Ruvu (shilingi milioni 40). Ukurasa wa 135 kiambatanisho Na.4 (q).

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani za dhati sana kwa Wizara yetu na Serikali kwa ujumla kwa kuinua kiwango cha barabara ya Bagamoyo hadi Makofia (kilometa 6.4). Jumla ya fedha za kigeni shilingi 1,130.6 zilizotengwa kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha *Otta Seal* (ukurasa wa 145 Kiambatanisho Na.6) ni hatua ya kutia moyo sana.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalize kwa kuiomba Wizara na Serikali kwa ujumla kutilia maanani haja ya kuijenga barabara ya Bagamoyo hadi Msata, kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri ya kupata wakandarasi toka Nangulukulu - Mbwemkuru na toka Mbwemkuru kwenda Mingoyo, tuna tatizo kubwa ambalo ni alama za barabarani za wakandarasi. Alama zao ni ndogo na zinawekwa karibu na jambo linalotolewa tahadhari. Kwa mfano alama ya kona huwekwa ilipo kona, tena kona kali. Je, huyu ni mkandarasi anayejua anachofanya kwamba tuna uhaba wa mbaao na rangi?

Naomba Serikali ilianganalie hili kabla hatujasababisha ajali katika barabara hizi. Katika kila mradi kuna Afisa wa Wizara, je, haoni kasoro hizi? Naomba lifanyiwe kazi haraka.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili, napenda kutoa ushauri kwa Serikali kwamba twende na wakati. Serikali haina fedha za kutosha, lakini wawekezaji wapo. Tuone mfano wa Afrika ya Kusini, Msumbiji, Namibia na Botswana. Barabara zinajengwa kwa *public private partnership*. Wamepiga hatua katika ujenzi wa barabara, mwekezaji anajenga, anatoza na Serikali inapata kodi, Serikali haina haja ya kutenga bajeti ya kujenga barabara bali inasimamia ujenzi wa barabara bora. Tunahitaji uzalendo, huthubutu na maamuzi ya haraka. Njia moja kuu ya kuimarisha uchumi ni kufungua barabara kuwafikia wananchi, inawezekana tuthubutu. Naunga mkono hoja.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kupata nafasi ya kuchangia hoja.

Pili, napenda kutoa pole kwa kifo cha Mheshimiwa Margreth Bwana, Mbunge wa Viti Maalum.

Tatu, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake na timu nzima ya Wizara lakini nawapongeza sana wakala wa ujenzi wa barabara *TANROAD* mkoa wa Ruvuma kwa kazi zao nzuri wakiongozwa na Meneja wetu *Mr. Laizer* na timu yake yote tunawatakia kheri sana na utendaji mwema.

Mheshimiwa Spika, hoja za kufanyiwa ufafanuzi, Ujenzi wa Daraja la Mto Ruvuma kupitia Songea - *Mitomoni Road* kuunganisha na Lupilichi Msumbiji. Tunaipongeza Serikali kwa ujenzi wa daraja la umoja kupitia mkoa wa Mtwara.

Lakini kwa sababu za kiuchumi na kijamii, Mkoa wa Ruvuma umekuwa ukiomba sana Serikali ifanye mazungumzo na Msumbiji na hivyo tujenge daraja hata la chuma katika mto huo ili kuongeza tija za kibiashara na kuongeza mapato ya mkoa wa Ruvuma katika miaka ya 1990.

Mheshimiwa Nicodemus Banduka alishaweka jiwe la msingi mahali hapo ni kwa nini Serikali haioni umuhimu wa Daraja hilo! Wenzetu wa Msumbiji na hasa mkoa wa Lichinga wameshachonga barabara nzuri mpaka hapo mtoni. Katika vikao vya mkoa mara zote tumekuwa tukitamani uwepo wa daraja hilo mfano ukurasa 17 wa kitabu cha Bajeti cha mkoa wa Ruvuma katika kuzungumzia sekta ya biashara na uchumi daraja hilo limepewa kipaumbele sana.

Lakini hata hivyo tunamshukuru sana Waziri wa Ujenzi wakati akijibu swala la nyongeza Na. 147 la tarehe 27 Juni, 2005 lililoulizwa na Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mheshimiwa Waziri aliliambia Bunge kuwa daraja hilo sasa limetengewa fedha, naomba nimshukuru sana. Lakini hata hivyo majibu haya ya swali la nyongeza hayamo katika mpango wowote wa Bajeti yake ya maendeleo, tungeomba tupatiwe maelezo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo hayo yote ziko sababu nyingi za kimsingi za kujenga hoja ya umuhimu wa daraja hilo ingawa majibu ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuhusu daraja hilo yanawataka Wanaruvuma ndio wajenge hoja za ujenzi wa daraja hilo. Tunashangaa sijui sasa kila aina ya maendeleo ni lazima wanaohitaji wajenge hoja. Sasa na huko kunako jengwa hoja alijenga nani? Au Wizara za Mipango na Wizara za kisekta zina kazi gani? Naomba Mheshimiwa Waziri kabla hujamaliza muda wako wewe mwenyewe uje uone mahali hapo, kwani si wewe wala Naibu wako aliyekuja kuona eneo hilo ambalo sasa ni kipaumbele kwa wana Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, makambi ya ujenzi katika barabara iendayo Songea - *Mbambabay* kuna kambi ya ujenzi ya Matomondo. Wananchi wa Kata ya Magagura kijiji cha Matomondo waliniagiza nimuandikie Waziri wa Ujenzi kuomba kubatilisha matumizi ya kambi hiyo ilikuwa sekondari kama zilizofanyika kambi nyingine. Lakini taarifa tuliyonayo ni kuwa kambi hiyo wameuziwa Kanisa la RC Jimbo la Songea ili kujenga chuo. Tunaomba Wizara itoe basi majibu kwa wananchi kuwa tayari kambi hiyo imeuzwa kwa matumizi hayo ili kuliweka suala hilo kuwa wazi na hasa kwa wananchi wa eneo husika.

Mheshimiwa Spika, uuzaji wa nyumba za Serikali Halmashauri ya Mji wa Songea wamesikitishwa sana na kitendo cha nyumba ya Mkurugenzi wa Halmashauri wa Mji kuuzwa kwa Mkurugenzi ambae hayupo na kufanya sasa Halmashauri hiyo sasa kutokuwa na nyumba ya mtumishi huyo. Sasa lini Serikali itajenga nyumba nyingine ili kupunguza gharama za kumpangishia nyumba Mkurugenzi.

Mheshimiwa Spika, rushwa kwenye mizani, mabasi yanajaza abiria mno lakini mara zote wanapokaribia maeneo ya mizani husimama hushusha abiria na abiria huvuka eneo la mizani kwa kutembea na baada ya mabasi kupima uzito kurejea tena katika mabasi hayo, hayo yote hutendeka wakati watu wa mizani wakiangalia hayo yote. Je, nini hiyo Mheshimiwa Waziri ni faida ya nani hiyo? Watumishi wa mizani wachunguzwe. Mfano halisi mizani ya Makambako.

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi kutenga fedha za barabara ya Wino - Ifinga, Songea - Mitomoni daraja la Mhimbasi - Litumbandyosi - Peramiho. Lakini tungeomba barabara ya Namatuhi kwenda Ndongosi nayo iangaliwe kwa kina.

Mheshimiwa Spika, mwisho niwapongeze wote katika Wizara kwa utendaji wao Mungu awabariki na naunga mkono hoja ya Wizara ya Ujenzi kwa asilimia mia.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimwambie Mzee wangu Mheshimiwa John Magufuli tulisoma wote Chuo Kikuu, *Degree* ya Kwanza na ya Pili. Nisaidie nirudi hapa baada ya Oktoba ili nikae kwenye lile jengo jipya la kisasa la Ukumbi wa Bunge.

Mheshimiwa John Magufuli, salaam sana *brother*, hii ni nukuu ya siku toka kwa mzee wa boma Mheshimiwa Pius Msekwa. Ni matumaini yangu kuwa utaichukulia kwa uzito mkubwa nukuu hii ili kuniondolea kero ya barabara toka Sanya Juu hadi Kamwanga.

**MHE. PHILIP A. MAGANI:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa John Magufuli, Waziri wa Ujenzi pamoja na timu yake ya Wizara hii ya Ujenzi.

Aidha, nachukua fursa hii kumpongeza na kumshukuru Waziri kwa kuamua kuichukua barabara ya Nangange - Mandawa mpaka Ngongo na kuifanya kuwa chini ya uangalizi wa Mkoa na hivyo kuipandisha *grade*. Barabara hii imefanyiwa usanifu na ninaona katika hoja ya Waziri ametenga shilingi 495,690,000 kwa ajili ya matengenezo ya barabara hii mwaka huu kwa kiwango cha changarawe na kuondoa sehemu zote korofi ili barabara hii ilete maendeleo kwa kasi mpya katika kipindi kijacho hususani katika utekelezaji wa mradi wa MKUKUTA, ambao kwa wananchi wa jimbo langu la Ruangwa na maana ya kupanua kilimo msingi mkuu wa uchumi wetu.

Napenda kuendelea kuwa Wizara ya Ujenzi na Waziri binafsi kwa kuamua kutoa daraja la chuma yaani *Bailey Bridge* iliyowezesha kuunganisha Wilaya za Ruangwa na Kilwa kwa barabara inayotoka Masasi-Nachingwea-Ruangwa na Kilwa kwa kupitia Nangurukuru. Kwa hivi sasa barabara hii ni ya Wilaya lakini kutokana na umuhimu wake katika utekelezaji wa mradi wa MKUKUTA kwa vile inapita katika eneo lenye ardhi yenye rutuba na maeneo makubwa yasiyo na msongamano wa watu na hivyo kufanya maeneo hayo ndiyo yanafaa kwa uanzishwaji wa mashamba makubwa ya mikoroshu, ufuta, mtama na mengineyo kama mifugo. Kutokana na sababu hizi uongozi wa Mkoa

kwa kupitia vikao vya *Regional Roads Board* umeomba sana barabara hiyo iwe barabara ya Mkoa.

Kwa kumalizia kwa vile barabara ile ya Nanganga-Mandawa inapitia sehemu zenye mabonde na mito ambayo kwa mtu asiyeifahamu sawa sawa eneo hili na ambaye anapita tu wakati wa kiangazi anaweza kushauri kuwa ni sehemu rahisi kuijenga barabara hii. Hivyo siyo kweli na ninaomba wakati wa kujenga barabara hii wataalam wawahusishe wakazi wa maeneo hayo wasije wakaweka makalvati kwa kudhani maji ni machache kumbe wakati wa masika inakuwa mito mipana na hivyo kuhitaji madaraja. Naunga mkono hoja na kumtakia Waziri kila la kheri.

**MHE. ZUBEIR ALI MAULID:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima zote, kwanza napenda nitoe rambirambi na pole kwa familia za Marehemu Wabunge mbalimbali waliotangulia mbele ya haki.

Mheshimiwa Spika, nitangulie kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wa Ujenzi pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Ujenzi kwa kazi nzuri ya Ujenzi wa miundombinu wanayoifanya. Miundombinu ina mchango mkubwa sana katika kuendeleza na kukuza uchumi wa nchi. Katika hili suala letu la MKUKUTA, ujenzi na uimarishaji wa miundombinu una mchango mkubwa na kwa hili ndio maana nasema Wizara ya Ujenzi wanastahili pongezi maalum kwa namna wanavyolisimamia suala hili. Wakati wa Kampeni za Uchaguzi wa mwaka 2000, uchaguzi ambao ulituweka madarakani. Ilani ya Uchaguzi ya CCM ilizungumza kwa kina kuhusiana na uimarishaji wa miundombinu Bara na Visiwani. Kwa kweli kwa asilimia kubwa pande zote mbili za muungano hili limetekelezwa. Kwa zile sehemu ambazo zinahitaji kujengwa barabara na bado suala hili halijatekelezwa, basi kwa namna moja au nyingine tunaridhishwa na juhudi za kuona kwamba mipango iko mbioni.

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu na kwa kusema hivyo ni kwamba nimebahatika kutembelea na kukagua kazi mbalimbali zinazofanywa au kusimamiwa na Wizara ya Ujenzi. Nimeshiriki ukaguzi wa barabara kutokea Dodoma - Manyoni - Singida - Nzega - Tinde - Shinyanga - Mwanza. Ukanda mzima nilioutaja ama kuna mkandarasi ameanza kazi au kwa maeneo mengine anamalizia kazi. Palikuwa na kasoro ndogo ndogo za baadhi ya kandarasi ambao wamechelewa kuanza kazi walizokatibiana. Hata hivyo ni imani yangu kwamba kutokana na utendaji wa watendaji wa Wizara hii, basi juhudi zitachukuliwa kuondoa kasoro zilizojitokeza katika hili.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kutoa tena pongezi kwa Wizara hii kwa bidii yao ya kazi na kazi nzuri wanayoifanya. Pia nipongeze Mashirika yaliyopo baina ya Wizara hii na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi ya Zanzibar ya kikazi ambayo ni kielelezo kizuri cha kudumisha Muungano wetu. Mungu awabariki wote.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, nitakapoanza kujibu hizi hoja nitajibu kwa niaba ya Waziri, lakini sasa hivi nazungumza mimi mwenyewe

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kutoa pole kwa Wabunge wenzetu sita ambao wamefariki wakati wa kipindi hiki cha miaka mitano. *Inshallah* Mwenyezi Mungu azipokee roho zao na aziweke mahali pema peponi. *Amin*.

Mheshimiwa Spika, nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Jakaya Kikwete, kwa kuteuliwa kuwa mshika bendera wa CCM kwenye kinyang'anyiro cha Uchaguzi Mkuu na Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, akiwa mgombea mwenza. Halikadhalika, Mheshimiwa Amani Abeid Karume, kule upande wa Zanzibar. Vile vile, nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kukaa katika Uwaziri Mkuu na kuamua kuacha, ni kitendo cha ujasiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nije upande wa shukrani. Kwa kawaida huwa tunaanza juu, mimi ningependa kuanza shukrani zangu na ile timu iliyokuwepo kule. Wale juu ya ujanja wetu wote Mheshimiwa John Magufuli na mwingine yeyote hao wakitaka kukuangusha huendi mbali, lakini wamekuwa msaada mkubwa sana kwetu na mimi nawashukuru kwa dhati kabisa katika muda huu wa miaka mitano. Kusema kweli miaka kumi tangu wakati wa Mheshimiwa Mama Anna Abdallah, yupo kama Waziri kule wa Ujenzi na Mheshimiwa John Magufuli, Naibu wake, hawa walikuwepo na mikakati hiyo ni endelevu, sisi tunaiendeleza lakini imeanzishwa na wengine. Tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimshukuru Waziri wangu, amekuwa mwalimu mzuri, kwangu mimi ni kijana hodari na amekubali kufanya kazi na mzee mkubwa kuliko yeye. Kwa hiyo, kwa heshima hiyo tunaheshimiana, ananiita mzee wangu, lakini kwenye ngazi ya Uwaziri ni mkubwa wangu. Amekuwa mtu mzuri sana. Lakini mno niwashukuru ninyi Wabunge, katika msukumo wenu na maswali yenu na kutuchapa, tunawashukuru mmetupa changamoto kubwa sana. Sina budi kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Morogoro Kusini kwa kunichagua na kunirudisha Bungeni na kunifanya Mwenyezi Mungu amwambie Mheshimiwa Benjamin Mkapa, anione, aniweke hapa. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shukrani hii ya mwisho, lakini ni kubwa sana nitaiieleza, ni shukrani kwa Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa kunateua mimi kuwa Naibu Waziri wa Ujenzi. Ninaieleza kwa sababu ni tofauti kabisa na uzoefu wenu ninyi wengine. Katika Jimbo la Morogoro Kusini tangu dunia imeumbwa, mimi ni Waziri wa kwanza, kwa hiyo, wananchi wangu wakasema, ulimshukuru kwa barua, lakini tunakutaka ukamshukuru hadharani. Hili ndilo ninalofanya sasa, Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, tunakushukuru sana kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa niende kwenye hoja, hizi nazijibu kwa niaba ya Waziri wangu. Kwanza, ahadi za Rais na viongozi wakuu wanapokuja kwenye Wilaya, Mikoa na kwingine pote. Tunapata migongano mingi sana, Waheshimiwa Wabunge mnaposimama mnazungumzia ahadi ambazo sisi wakati huo ndio tunazipata. Utaratibu wa ahadi za viongozi wakubwa ni kuzifuatilia kuhakikisha Mkuu wa Mkoa anazipeleka kwenye Wizara husika sio lazima Ujenzi ila husika, lazima Mkuu wa Mkoa azipeleke,



ndio zinaweza kufanyiwa kazi, Makatibu Wakuu wakizipokea. Ama sivyo ni ahadi ambazo zipo huko huko, ninyi mnazijua, huku Wizarani hawazijui.

Kwa hiyo, mara nyingi mnapokuja na ahadi za Rais hapa mkiuliza kwenye maswali sisi tunashangaa tu, lakini kwa heshima tunajibu, baadaye ndio tufuatilie. Lakini kwa sababu wengi mtarudi, kwa sababu CCM imefanya kazi nzuri, wengi wenu mtarudi, mfuatilie ahadi hizi ili Wakuu wa Mikoa wazipeleke Wizarani zifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Spika, mimi nitachangia michango ya Waheshimiwa Wabunge ambao walichangia kuanzia bajeti mpaka hotuba ya Waziri Mkuu. Naomba niwataje hawa ili kama hapa jina lako halipo na wewe ulichangia, tafadhali utuletee kwa sababu katika kipindi hiki hatukuahidi bali tutakuandikia barua muda huu huu upo hapa hapa, tutakuletea majibu yako kwa maandishi kwa sababu siwezi kutoa majibu yote haya katika nusu saa. Lakini wale ambao watakuwa wanajua kwamba walinukuliwa katika majibu yao hapa, basi pamoja na hayo nitakayoyasoma tutawaleteeni majibu binafsi ili mjue hoja zenu zimejibiwa vipi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wale ambao walichangia hotuba ya Waziri wa Fedha na hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji ni hawa wafuatao, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Paul Ntwina, Mheshimiwa Khalid Suru, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Lucas Seleli, Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Profesa Simon Mbilinyi, Mheshimiwa Frank Maghoba, Mheshimiwa Leonard Shango, Mheshimiwa Dr. Zanaib Gama, Mheshimiwa Venance Mwamoto na Mheshimiwa Mohamed Abdallah kutoka Pangani hawa ni 19. Kama ulichangia huko na jina lako halipo, tafadhali tulettee tutakupatia majibu yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, waliochangia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni Mheshimiwa Ismail Iwvatta, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Lydia Boma, Mheshimiwa Frank Maghoba, Mheshimiwa Gwassa Sebabili, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mheshimiwa Dr. James Msekela, Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Said Nkumba na Mheshimiwa Maria Watondoha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, waliochangia katika hotuba ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ni Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai na Mheshimiwa Gwassa Sebabili. Hao ndiyo waliochangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nianze na wale waliochangia katika hotuba ya bajeti. Lakini mengine tumeyafanyia kazi tutawajibu kwa maandishi kwa wale ambao muda wangu utakuwa hauniruhusu.

Mheshimiwa Ludovick Mwananzila yeye alikuwa anazungumzia barabara ya Tunduma - Sumbawanga, ijengwe kwa kiwango cha lami ili kutimiza ahadi ya

Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi aliyoitoa mbele ya Makamu wa Rais wakati wa ufunguzi wa madaraja 11 katika barabara hiyo. Mikataba ya usanifu na kuandaa nyaraka za zabuni kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami barabara ya Tunduma - Sumbawanga kilometa 230 inatarajiwa kusainiwa mwezi Julai, 2005. Ndiyo jibu lake.

Mheshimiwa Mwanne Mchemba, yeye alisema Serikali ifikirie kujenga barabara za Tabora - Mwanza, Tabora - Nzega, Tabora -Sikonge-Mbeya. Ujenzi wa barabara ya Tabora hadi Mbeya kupitia Rungwa utatekelezwa kwa awamu. Katika awamu ya kwanza ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kati ya Mbeya na Makongolosi unaanza katika mwaka wa fedha 2005/2006.

Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Viti Maalum pamoja na ujenzi wa daraja la Umoja Serikali ifikirie kujenga daraja la Mitomoni Mkoani Ruvuma iliyowekwa jiwe la msingi takriban miaka nane iliyopita. Mheshimiwa Jenista Mhagama hapa najua mbinu zake, urefu wa mpaka kati ya Tanzania na Msumbiji unakadiriwa ni kilometa 800. Sasa kuweka daraja moja dhahiri la Umoja halitasaidia kwa hiyo, kutahitajika na madaraja mengine huko mbele ya safari na ni dhahiri daraja la Mitomoni limo katika mipango hiyo.

Mheshimiwa Paul Ntwina, Serikali ijenge barabara za Ileje na Chunya kwa kiwango cha lami ili ziweze kupitika mwaka mzima ambazo ni Mbeya-Chunya-Makongolosi, Makongolosi-Mkwajuni- Mbalizi-Mbeya na Makongolosi-Itigi-Guba - Mpanda. Ie barabara ya Mbeya-Chunya-Makongolosi tumekwishaizungumzia na kazi za usanifu wa barabara ya Mbeya hadi Makongolosi umekamilika mwezi Mei, sasa hivi ujenzi kwa kiwango cha lami kwa kutumika fedha za ndani ambazo zimetengwa katika bajeti hii utakuwa unachukua hatua kikamilifu.

Mheshimiwa Khalid Suru yeye amezungumzia barabara ya Iringa-Mtera-Dodoma- Kondo na wengi tu wamezungumzia barabara hiyo ya Iringa-Mtera- Kondo pamoja na Mheshimiwa Raynald Mrope na Mheshimiwa Semindu Pawa, naye aliigusia. Jibu lilikuwa wazi tangu mwaka jana katika bajeti ya mwaka 2004/2005 zilitengwa fedha na sasa hivi kuna fedha tena zimetengwa katika bajeti ya mwaka 2005/2006 na kuandaa nyaraka za zabuni kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu.

Mheshimiwa Spika, watu wanalalamikia sana upembuzi yakinifu na usanifu haviishi. Naomba labda nieleze kidogo tu kama barabara inafanyiwa upembuzi yakinifu mwaka huu na fedha zitapatikana baada ya miaka mitano, barabara hiyo itakuwa imekwishaharibika lazima ifanyiwe upembuzi yakinifu tena. Upembuzi yakinifu ni *design* ya hiyo barabara kama umeipanga *design* yake kwamba hapa patakuwa na kalvati baada ya miaka mitano pale ulipodhani hapatakuwa pamebomolewa na maji tena kwa hiyo pengine utahitaji kuweka kalvati ndiyo maana inabidi kufanya hivyo na hii inatokea kwa sababu ya kungojea fedha za misaada.

Mheshimiwa Spika, ni kwamba wanapokuahidi wanakuletea wanafanya upembuzi yakinifu mwaka huu, halafu baada ya miaka 10 sasa ndiyo wanakuwa tayari kukupa fedha lakini wafanye tena upembuzi yakinifu, mkopo hana sauti ndiyo dosari ya

fedha za nje. Ukikopa huna sauti, unapokwenda kuomba chumvi nyumba ya pili, husemi ninaomba kibaba unaomba chumvi. Kwa hiyo, akikupa chumvi nyingi kakupendelea, anakwambia nenda katie chumvi kwenye mboga kesho uje uombe tena na hii ndiyo desturi ya kukopa na ndiyo inatupa taabu kwamba tunaweza kufanya na kurudia na kurudia hatupendi sisi kurudi hii kitu.

Mheshimiwa Spika, kuna malalamiko mengi sana ya ujenzi wa barabara ya Kibiti kwenda Lindi kuhusu kipande kidogo kile cha Kimanzichana mpaka Kibiti. Kwa kusema kweli Serikali imejitahidi na tumefuatilia kweli kweli ahadi ya *Kuwait Fund* na Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi alinituma nikaenda, kufika kule nitawaambia kitu kinachofanyika ni bora mkajua nini tunafanya. Unateremka *Airport* unapokewa vizuri, lakini cha kwanza unaonyeshwa msikiti kwenda kusali na mimi nilijua kwa hiyo, nilivaa balangashia, tukasali baada ya kusali mazungumzo ya barabara yakaanzia hapo pamoja na kikombe cha kahawa. Mkitoka hapo asubuhi wale unaozungumza nao pale siyo utakaozungumza nao kwenye kikao, unaanza upya na hao unaozungumza nao kwenye kikao hawajui nini mmefanya, inabidi waitwe wengine kule kuna vurugu kupita kiasi wale ndiyo shughuli ya Mheshimiwa Aggrey Mwanri, hasa wenzetu wana fedha, lakini mipango ni shughuli hawana mipango. Kwa hiyo, inabidi hapo ukae ustahimili zitafutwe karatasi zenu baadaye wanasema kweli ni hizi hapa.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo wanakwambia sasa tumepeleka fedha usiwe na wasiwasi Mheshimiwa nenda. Unakuja huku hakuna kitu mpaka leo tunawasiliana nao. Huo ndiyo utaratibu wao ni mgumu sana. Sasa tumekaa mwisho tunafikiria ni bora kutafuta fedha zetu tukajenga kipande hicho na yeyote mwingine atakaeleta fedha basi tutazitumia kujenga hapo ama kwingine kokote. Lakini kwa kweli uvumilivu umefikia kiwango kwa mkopo huu. Huu ulikuwa ni mkopo, lakini sasa umefikia kiwango kikubwa sana haiwezekani tena. Wenzetu watakaokuja itabidi wapange kabisa kufuatilia mikakati ya kutumia fedha zetu za nje kujenga kipande hicho cha barabara. Lakini nia ipo kubwa sana.

Mheshimiwa Raynald Mrope naye alizungumzia hilo hilo na vilevile Mheshimiwa Abdillahi Namkulala naye aliomba kabisa barabara ya *Mtwara Corridor* ipitie Magamba-Tandahimba-Newala na kutokea Masasi pia na barabara ya Mpapura-Mnazi mmoja kutokea Masasi iboreshwe. Kusema kweli ni nia ya Serikali kujenga barabara zote kwa kiwango cha lami ila hali halisi Mheshimiwa Wabunge mnaiona hapa inabidi tuamue na mimi naomba muamue huko Mkoani kiwango kilichopitishwa kwenye Bunge kutengeneza barabara za charangwe ni hiki kwa Mkoa huu.

Sasa mwaka huu Mheshimiwa Aggrey Mwanri, hupati hata senti moja, atapata fulani, barabara hii itengenezwe kwa kiwango cha lami halafu uandike kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, lakini najua tatizo hilo kwa sababu mimi ni Mbunge na nyie Waheshimiwa Wabunge mtagongana kila mtu atataka barabara ya kwake. Kwa hiyo, naomba mkubali mipango ya Wizara ya Ujenzi kwa sababu inatilia maanani sana umuhimu wa kuwa na barabara hata kama kiwango cha udongo au kiwango changarawe kwa sababu itasaidia kwa kipindi kirefu sana watu kupata mawasiliano. Pale hali

itakaporuhusu ndipo fedha hizo sasa za kutengeneza barabara kwa kiwango cha lami itatengenezwa kwa kiwango cha lami. Siyo kwamba tunapanga ili wewe upate barabara ya kiwango hicho. Ingekuwa hivyo tu Mwenegoha angekuwa na barabara za lami huko kwake, lakini hakuna hata kipande kule kwangu, si suala la kujipendelea wala si suala la kupanga. Lakini kupanga ni kuchagua, kwa hiyo, tunachagua zile barabara ambazo ni muhimu.

Mheshimiwa Omar Kwaangw', yeye alikuwa anazungumzia mgao wa fedha wa barabara wa asilimia 80 na Halmashauri za Wilaya na asilimia 70 ya barabara kuu uangaliwe upya na barabara za Halmashauri za Wilaya ziweze kuongezewa fedha.

Mheshimiwa Spika, suala hili linatawaliwa na Sheria ambayo imepitishwa hapa Bungeni na nilikwishajibu swali hili. Suala hili linatawaliwa na sheria na umuhimu wa kuwapa *TANROADS* fedha hizi ninyi wenyewe mmeona jinsi *TANROADS* wanavyojitahidi kutengeneza barabara hizo zipitike kwa mwaka mzima. Sasa tukiwapunguzia hii asilimia 70 ili ziende kwenye Halmashauri tunatoa fedha nyingi sana kwenye Halmashauri ambapo hawawezi kuzitawala, tutawaongezea fujo na tutawaongezea wizi wa fedha. Sasa hivi kuna tatizo la Makandarasi kwenye Halmashauri tunawambia *Registration Board* wote wasajiliwe, wote wawe Makandarasi ili wajulikane kama kweli wanastahili kuwa Makandarasi huko.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile hawana nyenzo za kufuatilia barabara na hawana watu wa kufuatilia barabara. *Budgeting System* ya huko kwenye Halmashauri ni ngumu sana na tumekwishazizuia Halmashauri nyingi sana kupata fedha hizo. Halmashauri nyingi sasa hivi ambazo tumezizuia zimetumia fedha za barabara kwa shughuli nyingine, kuitisha mkutano na kuzifanyia mambo mengine hata kujengea nyumba za hospitali badala ya barabara.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tumezisimamisha baadaye wakishalipa tunawapa tena hizo fedha.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi jambo muhimu na kubwa ni usimamizi bora wa fedha zile ambazo TAMISEMI wanazipeleka kwenye Halmashauri. Fedha zile zikisimamiwa vizuri tutapata barabara za changarawe na barabara za udongo ambazo zinapitika. Nilichokuwa nashauri kwa mfano, Morogoro Vijijini nimekwenda, nimemshauri Mkurugenzi kwamba Morogoro Vijijini ina barabara nyingi sana, ina Mito mingi sana na ina madaraja mengi sana, fedha wanayopata ni ndogo, kinachotakiwa ni kuhakikisha *engineer* yule wa Wilaya anasimamia wananchi wanatengeneza barabara hizo za Wilaya, tutapata *mileage* nyingi, kulikoni Makandarasi ambao watakuja kufanya wenyewe isipokuwa zile barabara ambazo ni ngumu.

Mheshimiwa Spika, lakini kilichotokea ni maneno ya Diwani tu hayo, baada ya hapo Makandarasi wanaambiwa hakuna kazi tunagombana nao. Juzi nikagombana nao nikawaambia safari nyingine hamtapata fedha kwa sababu hakuna matokeo kwenye fedha hizo na hiyo ni kila mahali tusimamie tutapata matokea mazuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri naomba *Force Account* itumike sana kwenye barabara za Halmashauri za Wilaya ni kweli inawezekana, lakini *Force Account* hiyo ikitumika lazima *accountability* iwepo na *accountability* ni ngumu sana kwa *ma-engineer* wa Wilaya sasa hivi. Kwa hiyo, ni vizuri bado twende pole pole pale inapoweza kusimamiwa inaweza kusimamiwa.

Mheshimiwa Spika, barabara ya kuunganisha Makao Makuu ya Mkoa wa Manyara na Wilaya zake itajengwa lini? Hili ndiyo lilikuwa kubwa la Mheshimiwa Mbunge na alisema kabisa hapa bwana tutakwaruzana.

Mheshimiwa Spika, ni azma ya Serikali naomba nilisoma jibu hili kwa uhakika kabisa. Ni azma ya Serikali kuunganisha Makao Makuu ya Mkoa wa Manyara na Wilaya ya Simanjiro na Kiteto kwa kufungua barabara mpya inayoanzia Babati hadi Okesumeti na Kibaya yenye jumla ya kilometa 250 kuanzia mwaka wa fedha 2003/2004. Wizara ilianza kutenga fedha kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa barabara hiyo hadi sasa kiasi cha shilingi milioni 630 kimeshatolewa na kazi ya usanifu wa barabara hiyo umekamilika. Kazi za ujenzi wa barabara kuanzia Babati ulianza mwezi Novemba, 2004 na jumla ya kilometa 17.5 katika awamu ya kwanza zinaendelea kujengwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali itaendelea kutenga fedha ili kazi ya ujenzi iendeleo kiasi cha shilingi milioni 500 zimetengwa katika bajeti ya mwaka 2005/2006. Serikali itaendelea kutafuta fedha za kutosha za ndani na nje ili kugharamia ujenzi wa barabara hiyo muhimu ili kuwezesha mawasiliano ya moja kwa moja kati ya Wilaya husika na Makao Makuu ya Mkoa. Kwa hiyo, ile ahadi ambayo ilitolewa na Mheshimiwa Rais sisi tunaitekeleza pole pole, hatuwezi kuitekeleza kwa mkupuo kwa sababu bajeti yenyewe haituruhusu.

Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, yeye amelalamika kabisa kwamba bajeti hii haizungumzii chochote juu ya ujenzi wa barabara Tanga- Horohoro na Pangani-Dar es Salaam. Barabara ya Pangani-Dar es Salaam tumeiweka katika *BOT* ili sekta binafsi wanaotaka kuwekeza katika barabara hii waje wawekeze na tumeiweka huko kwa makusudi. Hii ni barabara ambayo ni ya kitalii na tunajua mtu atakayewekeza katika barabara hiyo ataweza kulipa gharama zake. Kwa hiyo, tumeiacha hiyo barabara hivyo.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile tunajitahidi kutengeneza barabara ya Tanga-Horohoro. Barabara ya Tanga- Horohoro, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, imekwama sasa hivi kwa sababu nina taarifa kubwa kiasi hiki kwamba wananchi waliokuwepo njiani wamegoma kwamba barabara imewakuta pale, siyo wao na wao hawakuikuta barabara hiyo. Kwa hiyo, Mkuu wa Mkoa ameunda Tume ya kuchunguza ukweli uko wapi. Mpaka Tume hiyo itakapokuwa imeleta taarifa kamilifu kwetu na kujua ukweli uko wapi, nani anatakiwa kulipwa ama kuondoka, basi kwanza tumalize mgogoro huo kabla hatujaanza kubomoa nyumba za watu ingawa sisi tunaamini tuko sahihi, lakini inawezekana Tume ikatwambia mko sahihi kwa sehemu hii na sehemu nyingine siyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Profesa Simon Mbilinyi, amesema Serikali iunganishe Mkoa wa Morogoro na Mikoa ya Ruvuma na Lindi kwa barabara za kudumu.

Mheshimiwa Profesa Simon Mbilinyi, anazungumzia kuunganisha Mahenge na Ruvuma kwa sababu kuna sehemu ndogo sana na Mheshimiwa Jackson Makwetta, huwa anaizungumzia sana hiyo sehemu. Katika upande wa Mahenge kuna kijiji kinaitwa Tanganyika hicho ni kipande kidogo tu ukishavuka hapo kuna msitu halafu unakwenda kwenye upande wa Mkoa wa Ruvuma. Mimi nafikiri uwezekano upo ni suala la kupanga na kukubaliana tuna Halmashauri pale na kama pana msaada kidogo tumewambia wananchi wa Morogoro na Songea wakae, wajadili tuone kutakuwa na ugumu gani wa kubomoa huo msitu kidogo.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara zote au Serikali nzima tutekeleze mradi wa *Mtwara Development Corridor* kama Mradi Mkuu unaotaka kufadhili *Major Project. Mtwara Development Corridor* imejibiwa sana leo asubuhi na maelezo aliyotoa Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi yanatosheleza ila tuwaambie tu tayari kuna miradi na anayesimamia miradi hii sisi tunaratibu kama Wizara, lakini anayesimamia miradi hii ni *NDC*. Sisi kama Wizara tunaratibu anayesimamia utekelezaji wa miradi hii ni *NDC* na huko ndiko kwenye Makao Makuu ya *Mtwara Development Corridor* kwa utekelezaji.

Mheshimiwa Frank Maghoba, yeye alizungumzia juu ya daraja la Kigamboni. Daraja la Kigamboni halina mgogoro na daraja la Kigamboni lina watu kabisa *NSSF* wako pale na tumewapa *authority* na wao wanaingia mikataba, wamo mbioni kabisa fedha wanazo na watakopa kwingine kujenga daraja hilo halina mgogoro kabisa wa kujengwa. Lakini haliwezi kujengwa haraka kiasi hicho, najua Waheshimiwa Wabunge tunataka vitu haraka, haiwezekani kujenga daraja kama lile haraka sana, ila awape matumaini wananchi kwamba litajengwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, amechangia kwa maandishi, ameeleza juu ya barabara yake ya Mpanda - Konga, yeye analalamika kuna Mkandarasi anakwenda pole pole.

Mheshimiwa Spika, tatizo si Mkandarasi kwenda pole pole tu, tatizo lingekuwa kama kusingekuwepo fedha, fedha za barabara hiyo zipo wananchi wa Mpanda na wa Mashariki kule wawe na uhakika kwamba barabara hiyo ya Mpanda-Konga inatengenezwa na sasa hivi yuko kule Mkandarasi aliyechaguliwa anaendelea na kazi hiyo. Kwa hiyo, barabara hiyo inajengwa bila matatizo na sisi tutaifuatilia kwa bidii.

Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, yeye alikuwa anataka barabara kuu inayotoka Dar es Salaam kwenda Mbeya hadi Tunduma au Arusha-Lindi na Mtwara pia inayotoka Dar es Salaam mpaka Bagamoyo Mkoa wa Pwani hauna barabara za lami aliandika mambo mengi ndani akayaweka pamoja. Mimi nafikiri majibu sahihi na ya kuridhisha kwa Mheshimiwa Dr. Zanaib Gama, atayapata kwa maandishi.

Mheshimiwa Venance Mwamoto, yeye amemwomba Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi atimize ahadi yake ya kujenga barabara ya kutoka Ilula kwenda Mlifu na Watisori-Sagwa-Mparavua -Mkaranga- Kisinga-Rulazi mpaka Kilolo kabla hatujatoka Wizara ya Ujenzi. Mimi hapa naweza kumwambia Mheshimiwa Venance Mwamoto, kwamba ahadi ipo na Mheshimiwa Waziri kama ameitoa, ameinukuu na ameipeleka Wizarani sasa Mheshimiwa Waziri hapa akisema atajenga barabara hiyo bila wataalam

kumwambia fedha zipo na kama ipo kwenye bajeti Mheshimiwa Waziri atakuwa anamyumbisha kidogo Mheshimiwa Venance Mwamoto. Niseme tu ahadi yake imefika Wizarani na Wizara itashughulikia ahadi hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, yeye alizungumzia juu ya maendeleo ya Pangani, lakini vile vile alizungumzia barabara ya kutoka Bagamoyo kwenda Tanga. Hawa ndiyo waliozungumzia kwenye bajeti hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimesikia kengele imenionya hapa. Sasa labda ni vizuri nikazungumzia wale waliozungumzia kwenye Wizara ya TAMISEMI watatu tu.

Mheshimiwa Abdulkarim Shah, ambaye anataka mfuko wa barabara uwasaidie kwa ajili ya mitambo na ujenzi wa barabara Wizara inafahamu matatizo hayo na maombi yamekuja hapa sasa hivi na mengi yamezungumziwa juu ya mitambo, lakini uwezo wa Wizara kununua hiyo mitambo haupo.

Mheshimiwa Spika, hii ni mipango ya Halmashauri, ipange Halmashauri yake vizuri na iseme inataka kununua nini na ipitishie kwenye ngazi zinazostahili mpaka kwenye Wizara ya TAMISEMI halafu wakikubali Wizara ya TAMISEMI watawajibu hoja yao. Lakini sasa hivi kusema hapa mtanunuliwa ni uongo, mtambo mmoja unachukua bajeti ya kikao chote hiki, kwa hiyo, si kitu rahisi sana kwa mtambo kusema kwamba Halmashauri tutawanunulie hasa kutoka Wizarani si rahisi sana.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya JOZ iitwayo *TANHOPE* iliwaajiri wananchi Mafia na haikuwalipa. Hii Mheshimiwa Mbunge naomba tuonane ili tuweze kufuatilia kabisa tuone kama kuna Kampuni yoyote inakuwa tapeli, sisi tutaifuatilia na kuifuta. Hatuwezi kuruhusu watu wanaajiri wananchi huko halafu wanachukua fedha wanaondoka. Wanao *register* Kampuni wako hapa, wanasikia na hiyo Kampuni tutawapa hao *Registration Board* waifuatilie kwa nini wamewatapeli wananchi.

Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, yeye anataka barabara ya zamani Bagamoyo ifufuliwe upya tumelisikia tatalifanyia kazi tuone ni kwa kiwango gani.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni barabara za Dar es Salaam. Barabara za Dar es Salaam ni kama barabara za Dodoma zina mamlaka tele. Kwa hiyo, sisi Wizara ya Ujenzi mnavyotupa kwamba tupange barabara za Dar es Salaam na kubomoa hatuwezi, kuna Majiji pale matatu na kuna Jiji Kuu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni mipango yao waje wawasiliane na sisi. Ukiingilia kwenye mipango hiyo utapata taabu sana. Wanapoomba msaada ndiyo unakaa nao pamoja, ama sivyo utajishtukia unafanya vitu ambavyo wengine wote watakuachia ufanye wewe na Sheria ya *Road Reserve* iko pale pale mkitaka kupitisha barabara mbomoe lazima muwalipe hao.

Mheshimiwa Spika, sasa kama wao wana mipango hiyo wanaipanga, wanakubaliana na mipango yao ikiwa ni mizito zaidi wanawasiliana na Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi ili kuangalia ni jinsi gani Wizara ya Ujenzi inaweza kusaidia.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoahidi kwamba wengine wale ambao nimewataja hapa watapata majibu yao kwa maandishi kabla hatujamaliza Mkutano wetu wa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana wewe, ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza hasa hasa namshukuru Mheshimiwa John Pombe Magufuli, kwa kuniruhusu kujibu na niseme ninaunga mkono hoja hii mia kwa mia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyokwisha kueleza, sasa tutakwenda kwenye mapumziko ya mchana ili Mheshimiwa Waziri mtoa hoja apate nafasi ya kuandaa majibu yake vizuri na aweze kupewa nafasi tutakaporejea saa 11.00 jioni.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo hayo sasa nasitisha Shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 06.28 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba niombe radhi sana kwa sauti yangu ya leo si kama ilivyo siku zote, lakini nitajitahidi ili kusudi Waheshimiwa Wabunge waweze kusikia majibu ya zile hoja walizozijadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge waliochangia katika hoja ya Wizara ya Ujenzi wako 101. Waliochangia kwa maandishi ni 31, waliochangia kwa kuzungumza humu nao ni 31, lakini wapo wengine waliochangia wakati wa hotuba nyingine zilizotangulia. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mwenyekiti kama utakavyoona, itakuwa ni vigumu sana kujibu hoja zote za Wabunge 101 ingawaje ni kweli majibu yote tunayo hapa. Tutajitahidi majibu yote ambayo tayari tumeshayachapisha tuweze kuwakabidhi Waheshimiwa Wabunge baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitambue wale wengine waliochangia katika Wizara nyingine, walitambuliwa na Mheshimiwa Naibu Waziri asubuhi. Basi naomba nitambue wale Wabunge waliochangia kwa maandishi. Waliochangia kwa maandishi ni pamoja na Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti, Mheshimiwa Dr. Willbrod P. Slaa, Mheshimiwa Prof. Henry R. Mgombelo, Mheshimiwa Prof. Pius P. Mbawala, Mheshimiwa Leonard N. Derefa, Mheshimiwa Jackson M. Makwetta, Mheshimiwa Prof. Juma A. Kapuya, Mheshimiwa Shamsa S. Mwangunga na Mheshimiwa Omary Mjaka Ali. *(Makofi)*



Wengine ni Mheshimiwa Dr. Thadeus M. Luoga, Mheshimiwa Stephen M. Kahumbi, Mheshimiwa Beatus R. Magayane, Mheshimiwa Charles H. Kagonji, Mheshimiwa John Z. Chiligati, Mheshimiwa Dr. Maua A. Daftari, Mheshimiwa Halimenshi K. R. Mayonga, Mheshimiwa Venance M. Mwamoto, Mheshimiwa Paul E. Ntwina, Mheshimiwa Prof. Phillemon M. Sarungi, Mheshimiwa Leonard M. Shango, Mheshimiwa Elizabeth N. Batenga na Mheshimiwa Abdulkarim E. H. Shah. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Basil P. Mramba, Mheshimiwa Margareth A. Mkanga, Mheshimiwa John L. Mwakipesile, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Stephen M. Kazi, Mheshimiwa Mizengo K. P. Pinda, Mheshimiwa Juma S. Kidunda, Mheshimiwa Dr. Pius Y. Ng'wandu, Mheshimiwa Ramadhan H. Khalfan, Mheshimiwa Maria D. Watondoha, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri, Mheshimiwa Philip A. Magani pamoja na Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid.

Waliochangia kwa kuzungumza humu Bungeni ni pamoja na Mheshimiwa Henry D. Shekiffu, Mheshimiwa Mohamed Juma Khatib, Mheshimiwa Paschal C. Degera, Mheshimiwa Bernadine R. Ndaboine, Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah, Mheshimiwa Omary S. Kwaangw', Mheshimiwa Joel N. Bendera, Mheshimiwa Raynald A. Mrope, Mheshimiwa Edward N. Ndeka, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Anne K. Malecela, Mheshimiwa Abdillahi O. Namkulala, Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mheshimiwa Hadija K. Kusaga, Mheshimiwa Njelu E. M. Kasaka, Mheshimiwa Mariam S. Mfaki, Mheshimiwa Stanley H. Kolimba, Mheshimiwa Ali A. Karavina, Mheshimiwa Edson M. Halinga, Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri,

Mheshimiwa Dr. Raphael M. Chegeni, Mheshimiwa Frank G. Maghoba, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa John E. Singo, Mheshimiwa Kilontsi M. Mporogomyi, Mheshimiwa Lydia T. Boma, Mheshimiwa Suleiman A. Sadiq, Mheshimiwa Lucas L. Selelii, Mheshimiwa Mohamed A. Abdulaziz, Mheshimiwa Prof. Jumanne A. Maghembe pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda tu niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri sana na ushauri mwingi sana ambao wameutoa kwa Wizara ya ujenzi. Ni kweli kabisa kwamba michango yao yote kama nilivyosema inawezekana nisipate nafasi ya kuwajibu wote kwa sababu ni wengi, ni 101. Lakini nitajitahidi yale ya jumla niyazungumze lakini haya majibu mengine tutaweza kuwachapishia, kesho au keshokutwa waweze kupata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla Wabunge wote waliochangia wameipongeza Wizara ya Ujenzi. Kwa hili, kwetu sisi pamoja na wataalam wote wa Wizara ya Ujenzi imetufaraji sana. Imetufaraji kwa sababu imeendana tofauti na yale maneno yaliyoandikwa na baadhi ya magazeti leo na jana. Kwa mfano juzi waliandika; Magufuli kabanwa, Kakabwa na mengine mengi. Lakini ninyi Waheshimiwa Wabunge mmewaeleza hao Waandishi kwamba ni waongo kwa sababu sikubanwa kwa sababu tumeshangiliwa wote. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunawashukuru sana na hii inadhihirisha wazi kwamba pongezi zinazotolewa zina-*reflect* hata pongezi ambazo zimekwishatolewa na Mheshimiwa Rais. Mtakumbuka wakati wa Mei Mosi wafanyakazi waliochaguliwa kutoka Wizara ya Ujenzi ambao walikuwa wafanyakazi bora katika nchi hii, badala ya kuchaguliwa mmoja walichaguliwa 15 na wakaweza kutunukiwa vyeti na Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, pongezi zilizotolewa hapa na Waheshimiwa Wabunge, nasema ukweli kabisa kwamba sasa Wahandisi watacharuka na watafanya kazi kubwa sana, tunawashukuru sana. Kwa hiyo, ningewaomba na hao Waandishi wanaoandika nao wacharuke katika kutoa pongezi mahali panapostahili kutolewa pongezi. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtandao wa barabara za Tanzania kwa ujumla ni mkubwa. Barabara zinazoshughulikiwa na Wizara ya Ujenzi ni zaidi ya Kilomita 35,000. Lakini lengo kubwa la Serikali yetu ilikuwa ni kubadilisha mandhari ya barabara zetu kwa sababu katika miradi mingi ambayo tumekuwa tukiishughulika nayo siku za nyuma, kila barabara ilikuwa ikitengenezwa kwa changarawe. Kama mlivyochangia Waheshimiwa Wabunge wengi, barabara za changarawe hazidumu.

Katika Mradi wa *IRP* ambao ulifadhiliwa na *World Bank*, jumla ya Dola milioni moja zilitumika lakini *percentage* ya barabara kubwa zilizotengenezwa zilikuwa za changarawe na barabara ya changarawe inaweza ikakaa mwaka mmoja, haipo tena.

Kwa hiyo, nakubaliana kabisa na mawazo mengi yaliyotolewa ikiwa ni pamoja na Mheshimiwa Kilontsi M. M. Mporogomyi kwamba barabara za changarawe haziwezi kukidhi haja ya Watanzania. Kwa hiyo, baada ya kuona hili, Wizara ya Ujenzi tuliamua kupanga mikakati ya kuweza angalau kuhakikisha tumeanza kutengeneza barabara za lami. (*Makofi*)

Katika *transport Corridors* ambazo ziko tisa, tuliamua sasa angalau kila *transport Corridor* ianze kupata angalau uwezekano wa kutengenezwa kwa kiwango cha lami.

Barabara zote kuu Tanzania zina jumla ya Kilomita 100,700. Tumepanga na kwa pongezi hizi ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge nina uhakika kuja kufika mwaka 2012 barabara zote, yaani *Trunk Roads* zitakuwa zimetengenezwa kwa lami. Hii inatokana na hali ya uchumi na Sera nzuri za CCM zinavyendelea na nina uhakika hata miaka inayokuja CCM itaendelea kutawala. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mikakati hiyo ambayo ilipangwa, pamoja na kuendelea kupata fedha za wafadhili lakini tuliamua kuanza kutenga fedha zetu wenyewe kwa ajili ya kuanza kujenga barabara. Tuliamua kutumia mtindo ambao haujatumiwa mahali pengine katika Afrika, ni mpango wa *Design and Construct*. Huu ni mpango mpya na bahati nzuri umepata *support* kubwa sana kwa nchi nyingine maskini katika Afrika, hata Ulaya wametumia *support* kwenye huo mpango. Mpango huo ni wa kufanya *design* wakati huo huo na wakati huo huo unaanza kujenga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kilomita ambazo zinajengwa sasa hivi ni zaidi ya Kilomita 826, zinajengwa kwa kiwango cha lami ambapo jumla ya Dola za Kimarekani 375 zitatumika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi iko kwenye hatua mbali mbali, lakini nataka kuwathibitishia Waheshimiwa Wabunge, miradi hii inakwenda vizuri sana. Nataka nimthibitishie Mheshimiwa Raynald A. Mrope kwamba miradi hii inakwenda vizuri tofauti na takwimu zilizotolewa kwenye gazeti moja linalojiita gazeti la Serikali kwa kuandika kwamba zimepotea zaidi ya Shilingi bilioni 560 katika ujenzi wa barabara. Huu ni uongo mkubwa na nashangaa hilo gazeti kwanini liitwe la Serikali. Kwa sababu miradi inayotumika na ambayo imetajwa katika ile barabara ni Shelui - Nzega, Melela – Chalinze, Dodoma – Manyoni, Makuyuni – Ngorongoro ambao tumepewa *grant* na Wajapani; Nangurukuru – Mbwemkulu, Mbwemkulu – Mingoyo, Somanga – Matandu, Songwe – Tunduma, Manyoni – Singida; miradi yote hii gharama yake ni Shilingi bilioni 315. Yeye anazungumza zimeshapotea Shilingi bilioni 560. Gharama ya miradi hii ni Shilingi bilioni 315, yeye anasema zimepotea Shilingi bilioni 560. *It's nonsense!* (*Kicheko/Makofi*)

Katika miradi hii iliyotajwa katika hilo gazeti, kuna barabara ya Makuyuni – Ngorongoro, Kilomita 77. Ni juzi tu imefunguliwa na Mheshimiwa Rais, imemalizika kabla ya muda wake. Kuna barabara ya Somanga – Matandu, Kilomita 33 pamoja na Daraja la Matandu. Mtakumbuka Waheshimiwa Wabunge, sehemu hii ilikuwa ijengwe kwa Shilingi bilioni 50 kwa mipango ya *ORET* tukawafuta, imejengwa kwa Shilingi bilioni 13. Lakini huyu wa gazeti la Serikali ndiye anaandika haya mambo ya uchafu ya kuchafua kazi nzuri zinazofanywa na Serikali anayoiongoza Mheshimiwa Benjamin William Mkapa. Ninasema ukweli kwa sababu msema kweli ni mpenzi wa Mungu. Kwa hiyo, nataka kuthibitisha kwamba mpango huu wa *Special Project* unakwenda vizuri na huu ni *challenge* hata kwa wengine kwa sababu barabara kwa mfano ya *Central Corridor* ilikuwa imekosa Wafadhili.

Kila mahali wafadhili wanaanza upembuzi yakinifu ambao ninyi Waheshimiwa Wabunge mnaukataa. Tukaamua kufanya *Design and Construct* na ndiyo maana kwa sasa hivi kutoka Dodoma hadi Manyoni kuna Kandarasi, Kilomita 40 zimeshamaliza kuwekewa *Stabilization*. Hela zote Shilingi bilioni 65 zinatolewa na Serikali. Mtu wa kawaida anaweza akaona kuna uchelewesho kidogo, lakini sio kweli kwa sababu kazi ya kwanza kabla ya kujenga ni kufanya *design*. Kwa hiyo, ule Mkataba ukishasainiwa Kandarasi ni lazima atangulie kwenye *site* na kufanya *design*.

Kwa hiyo, ukiona mtu anafanya *design* utasema wamechelewa. Hawajachelewa! Ni pamoja na barabara hizo za Nangurukuru - Mbwemkulu, barabara ya kutoka Manyoni - Singida na kadhalika. Nataka kuwathibitishia Waheshimiwa Wabunge kwamba barabara hizi zitakamilika na fedha zipo na bahati nzuri Kandarasi halipwi pesa bila kuleta *Certificate*. Akishaleta *Certificate* ndipo analipwa pesa. Kwa hiyo, huyu mtu aliyeandika Shilingi bilioni 560 hakufanya hata *research*, kwa sababu mradi wote wa *Special Project* ni Shilingi bilioni 375, yeye anasema Shilingi bilioni 560; Je, alikuwa ameleva? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zinazofanywa na Wizara ni nyingi, lakini nataka kuwathibitishia Waheshimiwa Wabunge wa Tabora na Kigoma kwamba barabara ya kutoka Itigi – Tabora – Kaliua - Maragarasi hadi Kigoma kwa sasa hivi itaitwa *trunk road* na iko kwenye *first priority* ya barabara zilizo kwenye *Central Development Corridor*. (Makofi)

Katika Bajeti ya mwaka 2003/2004, barabara hii ilitengewa Shilingi bilioni 1.98. Katika Bajeti ya mwaka 2004/2005 barabara hii mpaka Kigoma ilitengewa Shilingi bilioni 5.05. Katika mwaka huu tumeweka Shilingi bilioni 8.684 na lengo letu kubwa, kwa sababu hapo kutoka Kaliua mpaka Maragarasi mpaka Uvinza palikuwa hakuna barabara. Ni kweli palikuwa hakuna barabara, lakini tumechukua hatua mbali mbali za kuhakikisha kwamba barabara hiyo inatengenezwa. Katika hatua zilizofikiwa sasa hivi, sasa hiyo barabara inaweza ikapitika kutoka Tabora mpaka kwenye mpaka wa Kigoma.

Lakini pia katika Bajeti ya mwaka huu kuna Kilomita 154 ambazo zitatengenezwa tuta ikiwa ni pamoja na Daraja lile la Malagarasi ambalo linaweza likapitisha tani 45. Kwa hiyo, nataka kuwathibitishia Waheshimiwa Wabunge kwamba lengo kubwa ni kuhakikisha kwamba ile *Central Development Corridor, main road* ni kutoka Itigi – Tabora - hadi Kigoma. *Branches* zake nyingine ndizo zinakwenda Ipole mpaka Mpanda, nyingine zinakwenda mpaka Mwanza. Hiyo ndiyo *Central Corridor*.

Lengo kubwa la Serikali ni kuhakikisha kwamba tunavuna sasa uchumi kwa sababu *DRC* kusafirisha mizigo yao kwenda *Durban* wanatumia zaidi ya Kilomita karibu 2000. Lakini kutoka kwenye Bandari ya Kigoma kuja Dar es Salaam ni karibu zaidi. Kwa hiyo, tutasafirisha mizigo mingi na kule *DRC*, wanaweza ku-*produce* hata zaidi ya tani milioni 12 kwa mwaka.

Kwa hiyo, tuna uhakika kwa kufungua hiyo *Central Corridor* itaweza sasa ku-*develop* sehemu hizi ambazo siku zote zimekuwa zikibaki nyuma. Ndiyo maana hata *design*, kwa sababu ilibidi kwanza tufanye *design*, tumeishafenya kwa kiwango cha lami kutoka Itigi hadi Tabora hadi Ipole na kwa sasa hivi tunafanya *design* kuunganisha Kigoma yote. Utaona katika ramani yetu tumeweka *dash*, *dash* ni kwa sababu siku za nyuma hii barabara haikujulikana kama *trunk road*, sasa ni miongoni mwa *trunk roads* zinazokuwa *considered* katika nchi yetu. Sasa mtauliza kwa nini sasa, na mimi sijui, lakini tunafahamu kwamba barabara hii ni muhimu sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara hii ya Tunduma - Sumbawanga: Hii barabara ya Tunduma – Sumbawanga; kuna fedha ambazo zimeshatolewa na Benki ya Dunia, lakini lengo kubwa ni kuiunganisha Tunduma, Sumbawanga, Kigoma, Nyakanazi, Mtukula Hadi Kampala. Kuna hatua mbalimbali ambazo zimeshachukuliwa kutoka Tunduma hadi Sumbawanga, kule *design* inaendelea vizuri. Kutoka Sumbawanga kuja mpaka Nyakanazi, Mikataba imesainiwa jana ya kuanza usanifu kwa kutumia fedha zetu.

Kwa mfano, usanifu wa barabara ya Tabora - Urambo – Kaliua, Mikataba imesainiwa jana kwa Kampuni moja inaitwa *M Consult Engineering*. Usanifu na

upembuzi yakinifu kwa ajili ya barabara ya Kigoma – Kasulu – Nyakanazi, Kampuni iliyoteuliwa ni *Crown Tech-Consultant*, nayo imesainiwa jana. Usanifu wa kutoka Bwanga – Biharamulo, *Data Consult* nao imesainiwa jana. Usanifu wa kutoka Makutano Nyamuswa hadi *Fort Ikoma Gate* nao umesainiwa jana, *consultant* aliyeteuliwa ni *M Consultant*. Upembuzi yakinifu na Usanifu wa awali kwa ajili ya barabara ya Sumbawanga – Mpanda ambapo mwanzoni ilikuwa ni kutoka Sumbawanga hadi Tunduma, nao umesainiwa jana na Kampuni iliyoteuliwa ni *Inter Consultant*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo letu kubwa ni kuhakikisha nchi yote inaunganishwa kwa mtandao wa barabara za lami. Hilo ndiyo lengo kubwa, kwa sababu hata tunapoomba fedha huwezi ukaomba fedha bila barabara kuifanyizia *design*. Nakumbuka Mheshimiwa Njelu Kasaka barabara yake ilianza kufanyiziwa *design* karibu miaka mitatu iliyopita. Mwaka huu zimetengwa Shilingi milioni 10 kwa ajili ya kuanza kuijenga kwa kiwango cha lami. Ni kwa sababu *design* ile imekamilika. Lakini kwa sasa hivi pia katika mwaka huu 2005, tunakamilisha *design* za barabara kutoka Minjingu, Babati, hadi Singida. Katika mwaka huu zimetengwa Shilingi milioni 900. Kwa hiyo, watakapomaliza watatangaza *tender* kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maeneo hayo ni ya barabara ya Babati hadi Dodoma. Sehemu hii ilifanyiwa makisio ya upembuzi yakinifu katika miaka ya 1990. Kwa hiyo, ilikuwa ni vigumu kutangaza *tender* ya ujenzi kwa *design* zilizofanyika kabla ya mwaka 1990. Bahati nzuri Benki ya Dunia pamoja na nchi za *NORDC* zimekubali kufadhili barabara hii kwa sababu ina umuhimu wa pekee katika nchi hii. Kwa hiyo, mwaka huu itafanyika hiyo *design* ikihusishwa na *design* iliyofanyika katika miaka ya nyuma ili napo *tender* zitangazwe kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa barabara ya Dodoma hadi Iringa, tuliomba fedha kutoka *ADB*. *ADB* wamechelewa kidogo, lakini tumeweka fedha zetu na tumetangaza *tender* tarehe 1/6/2005 kuanza usanifu wenyewe. Wafadhili watatukuta mbele tukiwa tunaendelea na hatua mbalimbali katika ujenzi wa kiwango cha lami. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni baadhi ya hatua tu zinazochukuliwa na Serikali katika kuhakikisha kwamba barabara zote katika nchi hii zinatengenezwa kwa kiwango cha lami. Katika ujenzi, kuna matatizo yake na ndiyo maana tumekuwa wakali sana na tumechukua hatua kali sana kwa makandarasi. Hadi sasa hivi kuna zaidi ya makandarasi 1700 waliofukuzwa. Sasa Mheshimiwa Mbunge, anasema nifukuze wengi zaidi. Lakini tumekuwa tukichukua hizi hatua katika kuhakikisha kwamba kazi ya ukandarasi isichukuliwe na watu ambao ni *briefcase contractors* ambao kazi yao ni kupiga maneno. Kwa hiyo, tutaendelea kuchukua hatua kwa kutumia hiyo Sheria Na.17 ya mwaka 1997 katika kuhakikisha kwamba kazi za makandarasi zinafanywa na makandarasi pekee. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejitahidi katika miradi mbalimbali ikiwa ni pamoja na miradi ya *RUSIRM* ambapo zaidi ya bilioni 34 zinatumiwa katika kuhakikisha barabara hizo zinatengenezwa. Maendeleo yanakwenda vizuri mpaka kwa Mheshimiwa Kolimba

na kule Ruvuma. Lakini pia hata katika suala la *Mtwara Development Corridor*, suala la *Mtwara Development Corridor* linazungumzia sana kuhusu barabara pia ya kutoka Mtwara – Masasi hadi *Mbamba Bay*. (Makofi)

Kwa hatua zilizofikiwa sasa, kwanza Marais wote wanne wameshasaini. Kwa hiyo, ni *commitment*, mtu mwingine hawezi akabadilisha *Mtwara Development Corridor* itaendelea kuwa *Mtwara Development Corridor*. Lakini miongoni mwa Marais, pia Rais wa Msumbiji na Rais wa Tanzania wameshasaini makubaliano ya kwamba daraja la *unit bridge* ni lazima lijengwe na fedha zetu. Hii ni kwa sababu baada ya kuomba wafadhili ikawa inashindikana kuzipata. Fedha zile zimekuwepo na zimetengwa katika Bajeti hizi. Tuna uhakika kwenye mwezi wa Tisa jiwe la msingi litawekwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hata katika *ferry* ya *TAMOFA* ambayo inaunganisha Tanzania na Msumbiji baada ya kushindikana kuendeshwa na wenzetu wa *TAMOFA* Serikali iliamua kuinunua na kuiendesha yenyewe na kwa sasa tumeshaifanyia ukarabati kwa ajili ya kuunganisha hizi nchi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika barabara ya Mtwara – Masasi hadi *Mbamba Bay* sehemu ya Masasi hadi Tunduru, Serikali ya Japan imesema itatoa fedha kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami. Serikali ya *Kuwait* nao wameonyesha nia ya kusaidia fedha hizo. Lakini katika Bajeti ya mwaka huu tumeweka Shilingi bilioni 5.86 tumalizie *design* kwenye sehemu iliyokuwa imebaki na tutangaze *tender* kwa ajili ya kuanza kujenga kwa kiwango cha lami pole pole. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa ujumla, lengo kubwa la Wizara ni kuhakikisha kwamba barabara zinatengenezwa kwa kiwango cha lami na ndiyo lengo la Serikali ya Awamu ya Tatu na awamu zitakazokuja kwa sababu ni lengo la Serikali ya CCM ambayo itaendelea kutawala milele. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala lingine ambalo limezungumziwa kwa kina sana ni suala la nyumba. Suala la nyumba limeanza kuzungumzwa tangu mwaka 1963 wakati Tume ya Adri ilipoteuliwa. Mwaka 1975 ikaja Tume ya Msekela, baadaye ikaja Tume ya Mramba ndipo tukaja tukapitisha hili kwa kutumia *Executive Agency* Na.30 ya mwaka 1967. Kwa hiyo, suala la nyumba siyo geni. Lakini pia hata katika Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2000 ya Chama cha Mapinduzi, inazungumzia kuhusu nyumba. Ukurasa wa 64, 65 na 67 ningemwomba Mheshimiwa Lwakatare na Kambi yake ya Upinzani wakasome hii ilani ili kusudi wajue malengo ya Chama cha Mapinduzi kwa sababu Kambi ya Upinzani, imezungumza mengi kutoa *challenge* ya hizi nyumba wamesema ni makambi. Katika *definition* ya Kamusi ya Kiswahili kambi ni mahali popote ambapo watu wanaweza kukusanyika kwa muda. (Makofi)

Kwa hiyo, kuna kambi ya wakimbizi, kuna kambi labda ya Jeshi, maana yake wakishamaliza ile kazi wanatatawanyika. Labda ni kambi kwa ajili ya Kambi ya Upinzani. Nyumba hizi ambazo zimejengwa Dodoma ziko 300 na 300 ndogo ndogo. Eneo la *plot* ni mita 40 kwa mita 80. Nyingine ni mita 50 kwa mita 80, nyingine ni mita 50 kwa mita 65 upana wa *plot*. Upana wa kawaida wa *plot* za *high density* ni mita 15 kwa 24. Sasa zile nyumba zinazouzwa kwenye Miji, *plot* zinapimwa za mita 15 kwa 24 siyo

makambi. Leo hizi tunazozijenga kwa sababu ni nyingi, huyu Msemaji wa Upinzani anasema makambi.

Lakini napenda nitoe mfano, zile nyumba za *Oysterbay* ukiamka siku moja miti yote imekatwa, nyumba zote zitaonekana makambi kwa sababu zinafanana. Nyumba za *NSSF* au nyumba za Bima ambazo tunakaa hapa *Area 'D'* miti yote ikikatwa yataonekana makambi. Kwa hiyo, nyumba za Dodoma siyo makambi. Mpaka sasa hivi tumeshapokea maombi ya watu 721 wakiwemo Wabunge 81. Sasa hii Kambi ya Upinzani inataka kuniambia Wabunge 81 wanataka kwenda kwenye makambi? Sina utaalum wa makambi sana kwa sababu sijawahi kukimbilia shimoni. (*Makofi/Kickeko*)

Lakini ninachotaka kusema ni kwamba haya si makambi. Katika ilani ya uchaguzi ukurasa wa 65 wanazungumzia katika nyumba za kuuzwa inasema kwa kupitia Shirika la Taifa la Nyumba imezifanyia matengenezo nyumba 10,027 na imewauzia wananchi wa kawaida nyumba 1738. Kwa hiyo, suala la kuwauzia nyumba halikuanza leo. Lakini pia katika hizi nyumba ambazo zinajengwa na kuuzwa tumeshajenga hivi sasa nyumba zaidi ya 171 na kwa sasa hivi nyumba hizi zingine 885 ziko kwenye *stage* ya mwisho. Lakini katika nyumba hizo zipo nyumba za ghorofa. Niliwawakea wenzangu wa Upinzani picha kwenye hotuba yangu waone ghorofa inavyojengwa lakini wao bado wanasema hiyo ghorofa ni kambi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, JKT wamekuwa wakifanya hii kazi nzuri na ningependa nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Wanajeshi wetu ambao wanafanya kazi kwa uadilifu mkubwa. Lakini kwa ndugu zetu wa Upinzani, wao wanasema wanawajengea makambi. Basi tutajenga makambi dunia nzima ili kusudi siku moja watu wote wawe kwenye makambi. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninachotaka kuthibitisha ni kwamba hakuna makambi, ni nyumba za kuishi wananchi na ni kubwa zaidi kuliko hata nyumba ambazo zimepangwa kama zile za *high density* na *low density*. *Low density* ni mita 30 kwa mita 40, hizi ni mita 40 kwa 80. Yale mengine ambayo tumeambiwa na Kamati ya Miundombinu kwa mfano kujenga *fence*, kubadilisha *infrastructure* mle tutayazingatia *infrastructure* mle ili kusudi mahali hapo pawe pazuri pa heshima na pasihesabike kama kambi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nijitahidi kujibu haraka haraka baadhi ya hoja zilizotolewa. Mheshimiwa Shekifu, amezungumzia masuala mengi, amezungumzia pia suala la kuchelewa kwa barabara. Napenda kumthibitishia kwamba hii *design and contract method* inakwenda vizuri na barabara zitakamilika kulingana na hatua zinazochukuliwa. Matatizo haya madogo madogo tutaendelea kuyashughulikia. Lakini napenda kuthibitisha kwamba yale mengi yaliyozungumzwa humu na Kamati ya Miundombinu tutayazingatia katika kuboresha na hasa katika kipindi kijacho ili tuhakikishe yale yanayowezekana kutimizwa yatimizwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Msemaji wa Upinzani ndiyo amezungumzia hili suala la nyumba, lakini pia amezungumzia mambo mengi, kwamba sera ya nyumba haikubaliki

kwa wananchi. Sasa sijui ni wananchi gani anaowawakilisha kwa sababu nafahamu hii ni sera ya CCM na wananchi wameichagua CCM. Kwa hiyo, inakubalika kwa wananchi ambao wengi waliweka CCM madarakani. *(Makofi)*

Lakini pia amesema kwamba nyumba inanunuliwa kwa Shilingi milioni 30 anaiuza kwa Shilingi milioni 300. Nyumba hizi za Serikali haziuzwi mtu akishauziwa haruhusiwi kuiuza mpaka baada ya miaka 25. Kwa hiyo, kama wapo ambao mnawafahamu, Waheshimiwa Wabunge ambao wamejaribu kuziuzua, basi tupewe majina yao tuchukue hatua. *(Makofi)*

Lakini hii nyumba akishauziwa mfanyakazi wa Serikali hatakiwi kuiuza mpaka baada ya miaka 25 na miaka 25 ni mingi, wafanyakazi wote watakuwa wameshamalizika kufa kabla hawajaziuza hizi nyumba. Huo ndiyo ukweli na mimi nikiwemo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge amezungumzia pia kwamba Serikali inajenga barabara za lami Mjini tu, lakini Vijijini zinaachwa. Huyu ni Msemaji wa Upinzani. Hili nalo si kweli. Barabara zinajengwa hata Vijijini. Tumezungumza kutengenezwa barabara kutoka Mwanza hadi Mtwara. Anataka kuniambia inafika Kijiji cha mahali inarukia Mjini! Kwa sababu barabara ni ya moja kwa moja, kwa hiyo, inapojengwa kwa vyovyote ni lazima ipite hata sehemu za Vijijini. *(Makofi/Kicheko)*

Lakini pia katika kupitia fedha ambazo zimekuwa zikiongezwa katika barabara zetu za Vijijini, zimekuwa zikiongezwa kutoka mwaka hadi mwaka. Kwa hiyo, si kweli kwamba barabara zinajengwa za Mjini tu, lakini tunaendana pia na hali halisi ya fedha zilizopo, kwa sababu nchi yetu bado ni maskini tutaendelea pole pole kuimarisha miundombinu yetu zikiwemo na hizi barabara za Vijijini.

Pia, amesema bado wapo makandarasi wababaishaji. Tutaendelea kutumia sheria Na.17 ya mwaka 1997. Amesema fedha za *Road Fund* zinatoshia kujenga Kilometa 436 za lami kwa mwaka. Sasa sifahamu wakati tulipokuwa tukipitisha sheria ya *Road Fund Amendment Act No.2* ya mwaka 1998, yeye alikuwa wapi? Kwa sababu sheria inasema *90% of the money should be used for the road maintenance only.*

Kwa hiyo, fedha za *Road Fund* asilimia 90 inatumika kwenye *maintenance* ya barabara tu na ndiyo maana huwa tunazipeleka *TANROAD* kwa ajili ya kuzishughulikia kufanya *maintenance*. Ndiyo sheria tuliyoipitisha hapa Bungeni. Yeye anasema inatoshia kutengeneza barabara ya lami tofauti na sheria tuliyoipitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia amejiwekea matumaini kwamba wao Wapinzani wakipata madaraka watatengeneza barabara, watafanya nini, hizo mimi nafikiri za ndoto za usiku au za mchana kwa sababu hawatapata madaraka. Kwa hiyo, hawatapata nafasi ya kutengeneza barabara. Nafasi ya kutengeneza barabara itabaki kwa Chama cha Mapinduzi (CCM). *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Degera ametoa pongezi kwa Wizara na mimi namshukuru sana. Amezungumzia juu ya barabara zake za Kwamtoro, Mpendo,



pamoja na Daraja la Mgululi, anasema tutafute angalau Shilingi milioni 100 ambazo wanadaiwa huko tuweze kuzilipa ingawaje barabara hiyo ni ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Lakini pia amezungumzia kuhusu barabara ya Minjingu – Dodoma hadi Iringa. Nimetoa maelezo, akasema kila mwaka katika miaka 15 imekuwa ni upembuzi yakinifu.

Nataka kukuthibitishia Mheshimiwa Degera kwamba barabara hii sasa kwa vile *tender* zimeshatangazwa kwa ajili ya kuanza usanifu na kwenye mwezi wa saba tutasaini huo Mkataba kwa sababu *no objection* ya *World Bank* pamoja na *NORDC*, wakishamaliza kufanya hiyo kazi tutatangaza *tender* kwa ajili ya ujenzi.

Lakini nataka kukuthibitishia kwa sababu sasa uchumi unakwenda vizuri na fedha zinaendelea kupatikana, tukiona Wafadhili wamechelewa tutajenga kwa kutumia fedha zetu. Mimi nakubaliana kabisa na wakazi wa barabara hii kwamba itakuwa ni aibu kuendelea tunazungumzia *the great northern road* bila kuitengeneza kwa kiwango cha lami. Ifike mahali iwe ni mwisho, tuanze kuzungumzia ujenzi wa kiwango cha lami kwa barabara hii. Kuhusu haya maombi sasa hivi siwezi kutoa ahadi, lakini tutajaribu kuzungumza na sisi tuangalie ni namna gani tunaweza tukasaidia. (*Makofi*)

Halafu Mheshimiwa Ndaboine, ametoa shukrani nyingi na amezungumzia kuhusu barabara zake nyingi katika Mkoa wa Kigoma. Mheshimiwa Ndaboine ametoa pongezi kwa ajili ya Ilagala na amezungumzia pia umuhimu wa kuitengeneza barabara ya kwenda Karya. Katika Bajeti ya mwaka huu, zimetengwa zaidi ya Shilingi milioni 616 ambazo Shilingi milioni 400 zitatumika kwa ajili ya ujenzi wa daraja na Shilingi milioni 216 zitaendelea kwa ajili ya kufungua ile barabara kutokana na ahadi ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa wakati wa uzinduzi wa Kivuko cha Ilagala. (*Makofi*)

Pia, amezungumzia barabara ya Tabora - Kigoma na amezungumzia barabara Kigoma Nyakanazi na sehemu nyingine. Kama nilivyoeleza, sasa hivi umuhimu uko mkubwa. Lakini pia amezungumzia barabara ya Nyalonga - Nyamtukuza haipitiki, amezungumzia juu ya Mwandiga - Manyovu na katika mwaka huu tumeweka Shilingi milioni 800 kwa ajili ya kufanya *otter seal*. Lakini pia kuna fedha nyingine ambazo zimetengwa za kuhakikisha kwamba barabara hii inapitika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka haraka, mwingine aliyechangia ni Mheshimiwa Shaweji. Amezungumzia kuhusu ile barabara ya kutoka Korogwe ya Mikumi – Kilosa – Dumila – Magole- Mziha – Handeni hadi Korogwe. Barabara husika ilitengewa fedha kiasi cha Shilingi 202.5 mwaka jana 2004 kutoka kwenye Mfuko wa Barabara kwa ajili ya kufanya maandalizi ya usanifu. Fedha hizi zilichelewa kidogo kuanza kutumika kwa sababu tulipozungumza na *DANIDA* wakawa wamekubali nao kutoa fedha kwa ajili ya ukarabati wa barabara hii.

Kwa hiyo, tukaona tusikae tukaanza kufanya usanifu mapema halafu tukazikosa hizo fedha. Kwa hiyo, *DANIDA* wametoa Shilingi milioni 1,600 ambazo wamezitenga katika Bajeti ya mwaka huu kwa ajili ya kuanza kufanyia ukarabati, wakati huo huo tukiendelea na kufanya *design* ili kusudi hii barabara nayo iweze kutumika kwa umuhimu

wake kama ambavyo Mheshimiwa Shaweji amekuwa akizungumza na Waheshimiwa Wabunge mnaelewa haya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Shaweji amezungumzia mambo mengi. Amezungumzia kuhusu makandarasi wanaofanya Morogoro - Dodoma angalau wajenge mabwawa na kadhalika. Sasa lile ni vigumu sisi Wizara kuwaambia kwa sababu nikiwaambia tu wataleta *variation wa-include* kwenye Mkataba wao. Lakini ningeomba Uongozi wa maeneo hayo watumie masuala ya kuzungumza ya ujirani mwema, nina uhakika watafanya hivyo na wamekuwa wakifanya hivyo na hasa Mheshimiwa Shaweji akienda kuwaomba nina uhakika watatekeleza hili kwa kujenga mahusiano mazuri na wananchi wanaokaa katika maeneo hayo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Shaweji amezungumzia pia kuhusu daraja la Mkata na Kapete. Tumejaribu kuyafafanua kadri tutakavyokuwa tunaangalia namna gani tunaweza tukayashughulikia.

Halafu Mheshimiwa Omar Kwaangw' amezungumzia kuhusu barabara ya *great northern road*; kama nilivyotoa ufafanuzi Serikali inaifanyia kazi. Lakini amezungumzia kuhusu ile barabara inayounganika Babati. Napenda kumthibitishia Mheshimiwa Mbunge kwamba hoja hii tumeipokea, ni kweli kwamba hadi sasa Serikali imekwishatoa Shilingi milioni 630 ambazo zimeshughulikia tu Kilometa 17 wakati barabara ina Kilometa 250.

Katika Bajeti ya mwaka huu, tumeongeza tena Shilingi milioni 500. Lakini usanifu wa eneo hilo ambalo kwa bahati ulichelewa sana kutokana na kwamba ilikuwa inapita kwenye hifadhi ya barabara, umekwisha kamilika kwa hiyo, napenda kumthibitishia Mheshimiwa Kwaangw' kwamba maombi na *concern* yake tumeichukua tutaendelea kuifanyia kazi vizuri ili kwa mwaka kesho awe na fedha nyingine nyingi zaidi. Lakini tuendeleo pia kuwaomba wafadhili ikiwezekana hiyo barabara iweze kupata wafadhili na kutengenezwa kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Bendera, amezungumzia juu ya Makandarasi wabovu hasa kwenye Halmashauri zetu za Wilaya. Suala hili tutalichukua na Bodi ya Makandarasi tutaweza kuwasiliana na Mheshimiwa Bendera tuone namna gani tunaweza tukajaribu ku-check. Lakini amezungumzia pia Miji mipya kama Mji wa Korogwe, upatiwe fedha maalum kwa matengenezo ya barabara. Amezungumzia barabara kadhaa zipandishwe daraja.

Wizara inaipitia Sheria ya *Highway Audience* ya mwaka 1967 baada ya kukamilika barabara zote za Wilaya na za Mikoa ambazo zitatakiwa kupanda daraja au kushuka, tutazileta Bungeni kwa ajili ya majadiliano na kuweza kuzishughulikia. Sheria hii inapitiwa na Wizara zote mbili, Wizara ya Ujenzi pamoja na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, pamoja na Wizara ya Mambo ya Ndani. Mheshimiwa Bendera pia amezungumzia pia barabara ya Mikumi – Kilosa – Dumila ambayo maelezo yake nimeshayatolea majibu. Tena amezungumzia katika hifadhi ya barabara. Hili tunamshukuru na amesema tufanye hivyo hivyo kwa nchi nzima. Kwa sasa hivi tunafanya hivyo, tunaweka alama kwa kila miradi yote inayojengwa na kutekelezwa katika nchi nzima. (Makofi)

Halafu Mheshimiwa Raynald Mrope, ametoa pongezi lakini pia alizungumzia kuhusu mgema akisifiwa sana tembo huweka maji. Sisi Wizara hatutaweka maji, tutaendelea kuweka pombe humo humo ndani. Lakini wapo wengine ambao wanataka tu kuamua kuchafua tu kama huyu aliyedai zimepotea Shilingi bilioni 560 wakati hana *information*. Mradi wenyewe *cost* yake ni Shilingi bilioni 315. Kwa hiyo, hao nao hawapendi kutamka ukweli, lakini hawataki hata kujivunia kile kizuri kinachofanywa na Watanzania. Hawa Wahandisi wanajituma sana, wanafanya kazi sana. Suala la rushwa Wizara ya Ujenzi limepungua sana. Zaidi ya Wahandisi 221 wenye *degree* walifukuzwa kazi, lakini hawa bado wanasema zinaibiwa. *Procurement Act* Na.3 ya mwaka 2001 tunaifuata kila mahali. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa sijui wanataka tufanyeje katika hii Wizara! Tungewaomba watu wanaopinga angalau waangalie historia ya Wizara ya Ujenzi. Tangu tulipopata uhuru mpaka sasa hivi ili kusudi wapime kutokana na matokeo na mafanikio yanayopatikana. Viongozi wetu wa kitaifa kila siku wanaweka mawe ya msingi, kila siku wanafungua barabara, sasa wangukuwa wanafungua kama zingekuwa hazitengenezwi? Kwa hiyo, Mheshimiwa Raynald Mrope, nashukuru umeelewa hili sisi si mgema akisifiwa tembo hulitiwa maji, hatutaweka maji, itaendelea pombe iwe *concentrated*. Kila siku hawa Wahandisi wataendelea kufanya kazi usiku na mchana kubuni mambo mapya ili kusudi Serikali iendelee ku-*move* na barabara ziendelee kutengenezwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Raynald Mrope amezungumzia juu ya madaraja tisa ya Masasi, yale yatakuwa *included* kwenye mradi wa *Mtwara Development Corridor*. Mheshimiwa Mbunge amezungumzia juu ya *Mtwara Development Corridor* na kwamba upembuzi umezidi sana kwenye ile barabara. Bila kufanya upembuzi yakinifu ndiyo *variations* zinatokea na ndipo hasara ya Serikali inatokea. Upembuzi yakinifu na usanifu (*feasibility study and detail design*) ndizo zinasaidia kujua daraja litawekwa wapi, mfereji utawekwa wapi, udongo utakuwa na ukubwa gani na barabara itapita wapi.

Bila kufanya hivi vitu, tutaendelea kupata hasara katika miradi ya barabara na ndiyo maana miradi ya barabara sasa hivi imeanza kushuka chini. Kwa mfano, Mradi wa Mtukura hadi Mhutwe ni barabara pekee nafikiri inaweza ikaongoza katika hata dunia kwa kuwa ya bei nafuu kuliko barabara zote zilizowahi kutengenezwa duniani. Kilomita moja imegharimu Shilingi milioni 146. Kutoka Mtukula hadi Mhutwe Kilometa 112. Kwa hiyo, tunayafanya haya yote ili kuhakikisha kwamba tunalinda fedha za wananchi. *(Makofi)*

Halafu Mheshimiwa Ndeka ametoa pongezi nyingi, amezungumzia barabara ya Itigi Tabora, ametoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais, amezungumzia pia kuhusu lile tamko la Shilingi milioni 100 ambazo tuliahidi tukiwa kule. Zile fedha zitatumika katika Daraja la Msombwezi kiasi cha Shilingi milioni 50 na msingi wa daraja la muda la chuma *bail bridge* katika Mto Lugufu, ujenzi napo utagharimu Shilingi milioni 50. Kwa hiyo, ahadi niliyoitoa bado ipo na fedha ndivyo zilivyotengwa hivyo. Lakini kwa ujumla barabara ya kutoka pale kwenda Karya itatengenezwa kulingana na ahadi iliyotolewa na Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Kilasi ametoa pongezi kwa Wizara lakini amesema kuhusu barabara ya Lujewa Madibira, Mafinga. Upembuzi yakinifu wa barabara hiyo umekamilika na Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami ianze. Aidha, hii barabara ya Lujewa Madibira ipitike bila matatizo Kilometa 75, Kilometa 71 zitakarabatiwa chini ya mpango wa *Agriculture Marketing System Program*. Mkandarasi amekwishapatikana na ataanza kazi mara moja wakati tukisubiri hiyo. *(Makofi)*

Amesema pia barabara ya kwenda Makao Makuu ya Wilaya ya Mbarali, ambayo ni Kilometa tano tu angependa angalau itengenezwe kwa kiwango cha lami. Ombi tunalisikiliza, tutaangalia namna gani angalau tunaweza tukatengeneza kwa kutumia *otter seal*.

Halafu Mheshimiwa Anne Kilango, amezungumzia kuhusu barabara ya *Great North* lakini pia Mkomazi – Ndungu – Ngoja - Same kwamba barabara hiyo nayo ishughulikiwe. Katika mwaka wa fedha wa 2005/2006 barabara ya Same Mkomazi itafanyiwa matengenezo ya kawaida. Aidha, Serikali imetenga jumla ya Shilingi milioni 90 kwa ajili ya matengenezo ya muda maalum. Barabara inayoshughulikiwa na Wizara yangu ni Mwembe – Mamba – Ndungu yenye urefu wa Kilometa 93 na Kilometa 30 za kwanza kati ya Mwemba na Manka na Kilometa 10 za mwisho kati ya Nyamba na Ndungu ni nzuri na zinapitika bila matatizo. Kilometa 53 za kati ya Manka na Nyamba haziko katika hali nzuri na zinapitika kwa shida.

Wizara yangu imepanga kuzifanyizia matengenezo kilometa 12 na jumla ya Shilingi milioni 199.1 zimetengwa kupitia mpango wa *STABEX*. Lakini pia Wizara imepanga kufanya matengenezo maalum katika barabara hii kwa kutumia fedha karibu Shilingi milioni 80.

Mheshimiwa Namkulala ametoa pongezi kwa Wizara na amezungumzia juu ya barabara ya Mtwara-Tandahimba-Masasi iwekewe lami. Ukweli barabara itakayowekewa lami ni ya Mtwara-Mnazi Mmoja-Masasi hadi Mbambay. *(Makofi)*

Ile nyingine itaendelea kwa kiwango cha changarawe mpaka barabara zote zile *trunk road* zitakapotengenezwa kwa kiwango cha lami kwa sababu barabara ya Mtwara-Tandahimba-Masasi ni ya Mkoa. Kwa hiyo, huwezi ukaanza kutengeneza barabara ya Mkoa kwa lami wakati kuna uwezekano wa kutengeneza ya *trunk roads*. *(Makofi)*

Lakini amesema pia Wapigakura wa Biharamulo wanirudishe mimi Magufuli na yeye wamrudishe Mtwara Vijijini. Kwa kweli na mimi nasema wamrudishe Mtwara Vijijini kwa sababu Mheshimiwa Namkulala anafanya kazi nzuri sana na wasipomrudisha watakuwa wamefanya kosa kubwa sana. *(Makofi)*

Amezungumzia pia juu ya barabara ya Mtwara-Kitaya na barabara za ulinzi. Tutaifanyia kazi tuone ni namna gani tunaweza tukasaidia katika barabara hizi. Mheshimiwa Lubeleje ametoa pongezi, amezungumzia hiyo barabara ya Minjingu-

Babati, kama nilivyotoa maelezo juhudi za Serikali zinafanywa. Amezungumzia pia barabara ya Mbade-Mpwapwa na daraja la Godegode.

Daraja hili liko katika barabara ya Halmashauri ya Wilaya. Kwa hiyo, ningemwomba sana aandike ombi maalum kupitia Tawala za Mikoa ili kusudi fedha zitolewe kupitia Mfuko wa fedha za *Road Fund* ili waweze kulishughulikia hili daraja na ni kweli hili daraja umelilia siku nyingi mno. Kwa hiyo, ningeomba uwaandikie watu wa Tawala za Mikoa waweze kukusaidia hili daraja. (*Makofi*)

Amesema pia Halmashauri zenye uwezo wa kununua mitambo ya kutengeneza barabara kwa fedha zake, zinaruhusiwa kufanya hivyo kama vile inavyofanya Halmashauri ya Temeke. (*Makofi*)

Mheshimiwa Lubeleje amezungumzia pia kuhusu uhaba na uduni wa vifaa vya kutengeneza barabara. Tumepokea ushauri wake, lakini napenda niseme tu wazi kwamba tutaendelea kushirikiana na Mheshimiwa Lubeleje katika kuhakikisha barabara zile zinazotuhusu zote zinatengenezwa katika kiwango cha kuweza kupitika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Hadija Kusaga amezungumzia ratiba ya ujenzi wa barabara ya Kilwa. Barabara ya Kilwa tumepata fedha kutoka Serikali ya Japan zaidi ya Shilingi bilioni 16 na zitatengeneza barabara yote kilometa 12 mpaka Mbagala na itakuwa barabara ya njia nne pamoja na njia ya watu wa kwenda kwa miguu. (*Makofi*)

Kwa hiyo, nataka kumthibitishia Mheshimiwa Mbunge kwamba hii barabara imeshapata fedha na tenda za kumpata *consultant* zimeshatangazwa Japan kwa sababu fedha zote zitatolewa na Serikali ya Japan na sisi tutachangia kiasi fulani. Kwa hiyo, Mheshimiwa Kusaga watu wa Temeke labda watafute sababu nyingine. Lakini sababu ya barabara ya Kilwa imeshapata fedha. (*Makofi*)

Amezungumzia pia kuhusu Kituo cha Mafuta, fedha tumezipanga na tumezitenga katika kukarabati Vituo vya Mafuta ambavyo viko chini ya Serikali ikiwa ni pamoja na Kituo cha Mafuta cha Dar es Salaam. (*Makofi*)

Lakini katika mpango tu wa kuendeleza barabara za Dar es Salaam, hata barabara ya Mandela nayo imepata fedha kutoka *European Union* zaidi ya Shilingi bilioni 34 pamoja na barabara ya Sam Nujoma. Barabara ya Sam Nujoma nayo tutaanza kuijenga mwaka huu kuanzia Mwenge mpaka pale Ubungo na katika bajeti ya mwaka huu tumetenga Shilingi bilioni 5.85. (*Makofi*)

Mheshimiwa Njelu Kasaka, ametoa pongezi na nafikiri anashukuru sana kwa barabara yake ya Chunya-Makongorosi na hii ni kujibu hoja ya kwamba wengine wanasema barabara za Magharibi hazijengwi. Nafikiri alisema Mheshimiwa Selelii. Kwa hiyo, Chunya-Makongorosi ni Magharibi na imetengewa Shilingi bilioni 10. Kwa hiyo, Mheshimiwa Njelu Kasaka ningeomba umwambie rafiki yako Selelii kwamba hata Magharibi zinajengwa barabara. (*Makofi*)

Lakini amezungumzia kuhusu ku-*connect* barabara hizo na barabara ya Chunya-Mbeya-Rungwa-Tabora-Ipole hadi Mpanda na wamempongeza *TANROAD Manager* wa Mbeya. Ushauri wote tutauzingatia katika kuhakikisha kwamba tunaboresha miundombinu katika kuwawezesha wananchi. Sasa na kengele imelia. Mheshimiwa Stanley Kolimba amezungumza mambo mengi, *RUSIRM* na kadhalika.

Mheshimiwa Karavina amezungumzia juu ya *transport corridors*, nashukuru sana kwa *contribution* yake aliyoitoa. Lakini nataka kumhakikishia kwamba *central transport corridor* ni kutoka Dodoma-Itigi-Tabora-Kaliua-Malagarasi-Uvinza hadi Kigoma. (Makofi)

Lakini pia ina *route* zake nyingine za kwenda mpaka Mpanda na nyingine za kwenda Mwanza. Lengo kubwa lilikuwa ni kuanzisha hii *transport corridor* katika *kubust* uchumi wa maeneo hayo ambayo kweli *economically they are very potential*. (Makofi)

Mheshimiwa Stanley Kolimba, amezungumzia juu ya barabara zake za Mkiu-Madaba. Tatizo la barabara za milimani na pembezoni mwa Ziwa Nyasa, tutazingatia ushauri huu ili tuone kadri tunavyoendelea tutawezaje kushughulikia barabara zake.

Mheshimiwa Halinga, naye amezungumzia kuhusu barabara za Mbalizi-Ileje-Kyela Road, anashukuru barabara ya Mlowo-Kamsamba na mengine mengi amezungumza. Kulingana na muda niliopewa naona saa zinakwenda kwa haraka sana. Mheshimiwa Mwanri naye amezungumzia kuhusu barabara yake. Lakini katika mwaka huu tumeweka fedha za kuanza *design* kutoka Kamwanga mpaka Sanya Juu ili kusudi kwa baadaye sehemu hiyo nayo iweze kutengenezwa kwa kiwango cha lami. (Makofi)

Mheshimiwa Chegeni, naye amezungumza mengi kuhusu barabara na amezungumzia barabara ya kupitia Ramadi. *Feasibility study* yake imekwishafanyika. Tutajaribu kuangalia ni namna gani tunaweza kuanza kuifanyia *design* ile barabara kwa sababu ndiyo *shortcut* ya watu wanaokwenda Musoma. Lakini amezungumzia juu ya barabara ya Nyanguge-Musoma. Katika bajeti ya mwaka huu 2005/2006 fedha karibu Shilingi bilioni 10 zitatolewa na *European Union* lakini tunaendelea na mazungumzo nao kwa ajili ya kufanya *ceiling*. (Makofi)

Lakini pia ni pamoja na barabara ya Kisesa kuja Usagara ambayo nayo itaunganishwa kwa kiwango cha lami. Mheshimiwa Maghoba, ametoa pongezi na pia amezungumzia daraja la Kigamboni. Daraja la Kigamboni tuliingia kwenye mazungumzo na wenzetu wa *NSSF* ili liweze kujengwa kwa njia ya *BOT*. Wanatakiwa kuleta taarifa zao mwezi huu ili kusudi Kandarasi aweze kujenga mapema. Lengo letu ni kuhakikisha kwamba pale panatengenezwa daraja ili wananchi waweze kupita bila matatizo.

Lakini pia zile *ferry* zetu tutaendelea kuziimarisha katika kuhakikisha kwamba wananchi wanasafiri bila matatizo yoyote. Mheshimiwa Hamad Mohamed Rashid amesema kwamba tumejenga Kilometa 1,319 tu kwa miaka 10.

Hii si kweli, kwa sababu ajumlishe hizo Kilometa zilizo kwenye kiambatanisho hicho lakini ajumlishe tena Kilometa 826 za *special project*, ajumlishe pia barabara nyingine ambazo sasa hivi zinakamilika. Kwa mfano, kama Nzega-Shelui Kilometa 110, ajumlishe barabara nyingine ambazo nazo zinaendelea kujengwa kwa mfano Singida na Shelui na nyingine nyingi ambazo zitaendelea katika mpango wa kujengwa.

Kwa hiyo, sio kweli kwamba tunajenga Kilometa 1,300 tu katika miaka 10. Kuna barabara nyingi sana na akisoma vizuri kwenye kitabu, ningemwomba asome ukurasa wa 133 na ukurasa wa 134 na 135 ili kusudi ajue idadi ya madaraja yanayoshughulikiwa. Tumeandika kwenye kitabu. Ni bahati mbaya nafikiri wakati anachangia alikuwa hajakisoma kitabu. Madaraja yatakayotengenezwa katika kipindi cha mwaka huu ni zaidi ya 2000 na kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kujitahidi kujibu kwa ufupi pamoja na kwamba ni masuala mengi sana ambayo yamezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge. Ningewaomba sana kwa heshima zote waweze kutupitishia Bajeti yetu katika kipindi cha mwaka huu wa 2005.

Kwa hiyo, ningeomba ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu na malengo yake ya mwaka 2005/2006, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe bajeti ya jumla ya Sh.344,831,318,500/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya nakushukuru na naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(*Hoja ilitolewa na Kuafikiwa*)

## **KAMATI YA MATUMIZI**

### **MATUMIZI YA KAWAIDA**

#### **FUNGU 47 – Wizara ya Ujenzi**

Kifungu 1001 – *Administration And General* ... .. Sh. 2,094,675,400/=

**MWENYEKITI:** Wasimame wote, tutaandika. Sasa kaeni, tutaanza na Mheshimiwa Lwakatare. Mtataja kifungu.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Vote 47, Programme 10, Sub-Vote 1001* - Mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kupata ufafanuzi wa ziada ukiachilia mbali suala ambalo amelifafanua kwa urefu la kuhusiana na nyumba na kambi iliyozungumzwa kama kambi ambalo kimsingi jambo hilo lilizungumzwa na Kamati, lilizungumzwa na Wabunge na hata wa Chama Tawala.

Lakini tukiachia hiyo, kwa bahati nzuri amewajibu kupitia kivuli cha Wabunge

wa Upinzani. Lakini ufafanuzi ninaoutaka kuhusiana na jambo ambalo tulijaribu kulizungumza la kuhusiana na boti za *lake fast ferries*. Kwa bahati nzuri kwa namna moja ama nyingine Mheshimiwa Waziri ni kwamba amekuwa mhusika mkuu katika kukwamisha boti hizi ambazo zilipashwa kupelekwa kule Mwanza kwa kuziwekea *stop* zisipite katika barabara.

Sasa ufafanuzi ninaoutaka kuupata kutoka kwake pamoja na kuiombea Serikali ya CCM kushinda uchaguzi mwezi Oktoba ingawa ni ndoto, lakini hili asiache viporo viporo kupitia Bunge hili. Ningetaka kujua kauli anayoitoa kwamba boti hizi zimeshindikana kabisa! Mazungumzo yameshindikana! Anachukua jukumu gani au jitihada gani kuweka mazingira ya kuwezesha hilo suala likamalizika kabla ya kipindi cha awamu hii ya Serikali kabla sisi hatujachukua madaraka tukasafirisha hizo boti? Naomba ufafanuzi. (*Makofi*)

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la boti ni suala la kisheria na ninakumbuka kabisa Mheshimiwa Lwakatare alipokuja hapa aliapa kwa Spika kwamba atalinda Katiba na Sheria. (*Makofi*)

Kwa hiyo, tunachotekeleza ni Sheria Na.30 ya mwaka 73 na ya *Highway Ordinance* ya mwaka 1967 kipengele cha 167. Katika Sheria hii inazungumzia kuhusu uzito unaotakiwa kupita barabara za Tanzania na kwa bahati mbaya sana barabara za Tanzania zinaruhusu mpaka tani 56. Lakini wenzetu wa nchi zilizoendelea kama Norway wanaruhusu tani 40. Switzerland wanaruhusu mwisho tani 28. Kwa hiyo, katika hatua ambazo zilichukuliwa, alipewa masharti yule msafirishaji. Kwa hiyo, mpaka sasa hivi hajayatimiza hayo masharti. Akiyatimiza yale masharti kulingana na sheria za nchi zinavyosema atasafirisha boti zake. (*Makofi*)

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Nakushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo mazuri ambayo ni *very convincing* na tunapozungumzia suala hili kwa bahati mbaya au nzuri, kaka yangu Magufuli naye ni mdau katika suala hili la boti kwa sababu zinakwenda huko huko ambako na yeye Jimbo lake lipo. Ni kwamba limekuwa ni suala ambalo lina utata kiasi kwamba sisi tulioko nje ya *cabinet* tumeshindwa kuelewa *cabinet* inafanyaje kazi.

Kwa sababu sisi wenyewe tuliweza kujionea wenyewe Waziri mmojawapo wa Mawasiliano na Uchukuzi akiwa bandarini akitaka aruhusu zile boti kusafirishwa. Na naamini kabla hajafanya hivyo bila shaka alitokea kwenye *cabinet* hiyo hiyo ya Mheshimiwa Mkapa. Lakini ukiachilia hiyo, ni kwamba zimekuwepo jitihada mbalimbali, ushauri mbalimbali, hata Kamati ya Bunge imejaribu kuliingilia kati suala hili.

Sasa sijui anachotaka kueleza hapa Mheshimiwa Waziri. Ni kwamba pamoja na ushauri na jitihada zote ambazo zimefanywa na vikao mbalimbali na Taasisi mbalimbali, kwamba bado sheria hii Na.30 haitoi nafasi yoyote ya suala hili kuzungumzika kiasi cha kuruhusu hizi boti zikapita. Ukiachilia mbali sisi wenyewe ni watumiaji wa barabara



hizi, tumekuwa tunashuhudia mizigo mingine mikubwa mipana tu ambayo imekuwa ikisafirishwa hata wakati mwingine kuzuiwa barabarani ili hiyo mizigo ipite.

Iweje leo hili suala ambalo hata yeye mwenyewe linamhusu huko Jimboni, linawahusu wananchi walio wengi Wapigakura, ni kero kwa wananchi wa Kanda ya Ziwa ambao hata nauli ya Ndugu yangu Mongella anayekwenda Nansio huko, imepanda mara mbili kwa sababu ya mwingiliano wa safari hizi za meli kwa kukosekana usafiri wa meli. Anasemaje Mheshimiwa Magufuli katika hili? Limeshindikana kuzungumzika?

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kutoka Kagera na suala la Sheria ni mambo mawili tofauti. *(Makofi)*

Hapa tunatekeleza sheria. Tuliapa kuzilinda na katika Sheria hizi zimeshawakumba watu wengi. Napenda nitoe mfano, Jeshi la Wananchi walipokuwa wakisafirisha *Roll Loader* kulipeleka Loliondo tuliwapiga faini ya Shilingi milioni 43 na wakalitenganisha. *(Makofi)*

Wizara ya Maliasili wakati wanasafirisha boti kwenda Kigoma ilibidi wazipakie kwenye *train* kwenda mpaka Zambia. Katika kiwanda cha migodi kule Musoma ilibidi vile vifaa vikae karibu miezi mitatu vitenganishwe. Bohari za Madawa hawazidishi kwa sababu lazima wapeleke kwenye ule uzito unaotakiwa. Sasa anachotaka kama hawa wengine mpaka Wanajeshi mpaka wametekeleza, hivi ni ugumu gani huyu mtu kutenganisha vitu hivi kuvipeleka huko? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ziwa Victoria lina boti nyingi sana. Lina *MV Victoria*, ni kubwa haikupakiwa kwenye barabara; ina *MV Bukoba* ambayo ilizama, haikupakiwa kwenye barabara; kuna *MV Ukara* ambayo imezinduliwa na Rais, kutoka Wizara ya Ujenzi tumeipeleka sisi kwenye vipande vipande. Huyu Mheshimiwa Lwakatare anang'ang'ania kitu hiki ni cha nini. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. HALIMENSHI K.R. MAYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fungu 47, programu 10, *Sub-Vote* 1001. Niombe tu kwamba mwaka jana nilisema sana kuhusu hii barabara ya Mwandiga-Manyovu. Kwa bahati nzuri hii barabara ameiona na Viongozi wote wa kitaifa wamepita hii barabara, hakuna Kiongozi wa kitaifa ambaye hajatembelea hii barabara ya Mwandiga-Manyovu.

Nimshukuru tu kwamba sehemu moja ndogo sana ndiyo iliyotengenezwa na ahadi zote. Hii barabara ni mbaya kweli. Ukisema kwamba kuna Shilingi milioni 800 ya kutengeneza barabara kwa *otter seal*, Shilingi milioni 800 zinatengeneza hatua ya namna gani ukilinganisha kwamba hata hizo kokoto zenyewe inabidi zitoke au kule kutengeneza kwa changarawe, inabidi zitoke Tabora! Bado ninaona kabisa hatuna Wakandarasi ambao wanaweza wakaomba ile tenda kwa Mkoa wa Kigoma, inabidi watoke labda Mikoa jirani na wa kutoka Mikoa jirani hakuna, anaweza kupata Shilingi milioni 800.

Mwaka jana ilikuwa Shilingi milioni 400, mwaka huu Shilingi milioni 400. Ina maana Waziri zitakuwa Shilingi milioni 400! Shilingi milioni 400 mpaka mwaka 2025 huko! Maelezo ya barabara hii ni yapi? Watu wanabeba mizigo yao kwa baiskeli,

tunaendelea namna hiyo na hii barabara! Niambie hapo kwanza. Naomba maelezo. (Kicheko)

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba barabara ya Mwandiga – Manyovu kwa sasa hivi imeharibika na hii inatokana na hali halisi ya udongo wa sehemu ile na mimi mwenyewe nimeshaitembelea hiyo barabara. Napenda kumthibitishia Mheshimiwa Mayonga kwamba mwaka huu tumeweka Shilingi milioni 800 ili kusudi zianze kutengeneza kwa *otter seal* hasa kwenye zile sehemu zina matatizo.

Lakini pia tumetenga fedha nyingine. Ukiangalia katika viambatanisho vilivyoko katika Mkoa wa Kigoma, kuna fedha ambazo zimewekwa kwenye *packages* katika Mkoa mzima. Kwa hiyo, kuna fedha mle ambazo zitatumika pia kuiendeleza ile barabara. Nataka kumthibitishia Mheshimiwa Mayonga na Wapigakura wa sehemu hiyo kwamba ile ahadi niliyoitoa wakati nikiwa kule, tutaitekeleza katika Bajeti hii. (Makofi)

Kuhusu Makandarasi kwamba watoke wapi, mkandarasi anatafuta fedha. Kwa hiyo, Shilingi milioni 800 na zile za 400 za mwaka jana si haba, lazima watapatikana. Ningependa pia kutoa wito kwa wananchi wa Kigoma akiwemo Mheshimiwa Mayonga mwenyewe kwa sababu mkandarasi hata ukiwa Mbunge unaweza ukawa mkandarasi na bado tukaendelea kukupa kazi.

Kwa hiyo, ajaribu kuwahamasisha wananchi wa Kigoma pia kuanzisha Kampuni za ukandarasi ambazo hiyo ni njia mojawapo ya kuwasaidia kuimarika kiuchumi na kifedha katika Sekta hii ya Ujenzi. Kwa hiyo, nataka kumthibitishia Mheshimiwa Mayonga fedha hizi zipo pamoja na nyingine ambazo zitahusika kuikarabati barabara hii. (Makofi)

**MHE. HALIMENSHI K.R. MAYONGA:** Ninachokiomba Mheshimiwa Mwenyekiti katika hili, ni maelezo tu kwamba ukikaa ukahesabu kwamba pesa zipo miaka yote, mimi ni Mbunge tangu mwaka 1990, hakuna Waziri wa Ujenzi hata mmoja ambaye amesema kwamba hakuna pesa! Yuko wapi? Kiula ndiyo niliyeanza, naye alikuwa na maelezo ya namna hii hii. Ifikie hatua kwamba tunapokuwa hapa, tuseme kinachowezezana, kama hakiwezekani, tunasema hatua hizi bado tunaendelea na hilo, wananchi wanaelewa kuliko kuwapa matumaini halafu yasifanyike.

Nimekwenda Wizara ya Ujenzi mara 25, aangalie kitabu, kipo pale, *twenty fifth times* sasa anataka niende mara ngapi kule. Ninachokiomba, atoe maelezo ya kina ambayo atanihakikishia kwamba inaweza ikaanza tarehe ipi, siyo mpaka mwaka kesho, kwa sababu sisi mvua inaanza na mvua ikishaanza watu wanatembea kwa miguu na baiskeli. Au hizo hela tunazifanyia nini sasa zikiwepo? Kama hakuna utaratibu wa zana ambazo zinaweza zikaenda, atutafutie zana, ndiyo hicho ninachokitaka ziende mara moja kuanzia sasa. Hapo sasa! Niko *serious!* (Kicheko/Makofi)

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mayonga kwanza namshukuru kwa jinsi anavyofuatilia hii barabara. Amesema Mawaziri wengi

wamekuwa na lugha hii hii tangu mwaka 1990. Ningemwomba Mheshimiwa Mayonga naye aniamini mimi kwa sababu Mawaziri wengi walikuwa wanatoa ahadi hawakufika huko, mimi nimefika huko. *(Makofi)*

Nilikuwa naye na nikafanya Mkutano na wananchi. Nasema uongo Mheshimiwa Mayonga?

**MHE. HALIMENSHI K.R. MAYONGA:** Sawa sawa!!! *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Sasa kama amethibitisha kwamba nimefika, aniamini haya ninayoyazungumza kwa sababu niliyaona mwenyewe. Waheshimiwa Wabunge wakishapitisha hii bajeti mambo yatakwenda vizuri, akizuia hata hizo hela Shilingi milioni 800, watamshangaa wananchi wa kule kwa sababu tunataka kupitisha Bajeti hii tutangaze tenda mara moja ya kutengeneza barabara ya Mwandiga-Manyovu. *(Makofi)*

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii. Najua kwamba Mheshimiwa Waziri alikuwa na maelezo mengi. Fungu 47 na fungu dogo Na.1001 na kifungu kidogo kabisa 250100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri alikuwa na maelezo mengi na ninajua kwamba alikuwa na maelezo hata ninayouliza. Kwa hiyo, ningependa atupe mwanga kidogo kuhusu maombi yetu ya *belly bridges* kwa ajili ya Mwanga *by pass road* na maombi yetu kuhusu kuweka lami ya *otter seal* katika Mwanga *escapment*.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa Mheshimiwa Profesa Maghembe alitoa maombi Wizarani kwa ajili ya kuweka *belly bridge* ili ziweze kusaidia katika barabara yake ya *by pass*.

Katika maelezo yangu ya siku za nyuma nilimwahidi kwamba yakipatikana tutaweza kutoa. Sasa napenda tena kupitia Bunge hili nimwahidi tena Mheshimiwa Profesa Maghembe, kwanza ametupongeza sana sisi Wizara, tumefurahi sana na pongezi zako nyingi.

**WAZIRI WA UJENZI:** Kwa hiyo, kwa kupitia hayo maneno ya pongezi ambayo ninauhakika umeyatoa moyoni, nataka kukuthibitishia kwamba hizo *bell bridge* kwa sababu sasa hivi kuna barabara nyingi zinatengenezwa za *trunk road* tutazitafuta kwa sababu ni za madaraja mawili ili tuweze kukusaidia kwa ajili ya sehemu yako. *(Makofi)*

Kuhusu zile fedha za *otter seal* kutokana na hali halisi ya bajeti, tumeshindwa kutekeleza hilo. Lakini ombi lako litaendelea kukaa kwenye vitabu ili siku fedha zitakapopatikana ziweze kutolewa mara moja.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kitabu cha pili *vote 47 program 10, sub-vote 1001, item 250.100 basic salary*. Nilizungumzia barabara ya *central corridor* nikimaanisha inanzia Dodoma - Itingi - Tabora - Kigoma na

nikazungumzia umuhimu wa *central corridor* ambayo kwa sasa ilivyoonekana kwenye kitabu chake inaambaa hadi Nzega - Tinde Kahama au Nzega Mwanza. Sasa katika majibu yake, amesema kwamba ameweka kipaumbele katika barabara hiyo na katika kitabu cha nne inaonekana kweli kuna pesa zimetengwa bilioni tano kwa barabara ya kutoka Itingi kwenda Mkalio Malagalasi mpaka Kigoma kwa kiwango cha changarawe.

Lakini nimezungumza kwamba, ujenzi wa barabara kwa sasa au kukopa pesa kwa sasa si kujenga kwa kiwango cha changarawe, ni kwa kiwango cha lami na nikasema mbona isifanyike hata *feasibility study* sasa hivi na *design* kwa sehemu ambazo zinatakiwa zijengwe kuibua uchumi na hasa *central corridor*, wanapozungumzia kuunganisha Mikoa ya Mbeya, Rukwa na Tabora. Kwa sababu Tabora ni Mkoa peke yake ambao umebanwa bila barabara kuu zozote kupita pale na nikazungumzia umuhimu wa Kigoma kwa kuibua kwa kutumia nchi zile za Magharibi za Burundi, Rwanda pamoja na Kongo. Lakini bado majibu yake yanaonekana kama alivyojibu pale kwa Chunya, anaunganisha Chunya na *central corridor* au nchi za Magharibi. Hivi Mbeya tangu lini imekuwa Mkoa wa Magharibi? Mimi ningedhani aliambie Bunge kwa usahihi kitu gani ambacho kinatakiwa kifanywe katika *central corridor* pamoja na hiyo Mikoa ya Magharibi.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana Mheshimiwa Seleli hakunielewa vizuri wakati nikizungumzia juu ya *central corridor* na nikiweka msisitizo wa *central corridor* nilizungumza Itigi - Tabora hadi Kigoma na Wabunge wote ni mashahidi. Nikaeleza kwamba katika ule mtandao wa *central corridor* kuna Mtwara *corridor*, kuna *central corridor* ina matawi ya kwenda Mwanza pamoja na nyingine ya kwenda Mwanza pamoja na nyingine ya kwenda Mpanda. Sasa kama niliweza kuzungumzia *central corridor*, nafikiri sikuwa nimekatazwa kuzungumzia sehemu nyingine za Chunya, Mtwara, Lindi na sehemu nyingine.

Ile ilikuwa ni katika kuthibitisha juhudi zinazofanywa na Serikali katika kuhakikisha barabara nyingi zinatengenezwa kwa kiwango cha lami. Barabara anayoizungumza ya Itigi – Tabora imeshamaliza kufanyiwa *feasibility Study na detail design* mpaka Ipole. Kwenye bajeti ya mwaka huu tumetenga fedha zaidi ya kilometa 100 za kufanya *design* kutoka Kigoma kule kuja mpaka Kaliuwa Ilundi. Sasa anataka umuhimu gani mwingine ambao kama sikuanza kufanya hizo *design*, hata barabara yake ya Nzega kuja Shelui tulianza kwanza kufanya *design*.

Mtakumbuka katika historia ya Mheshimiwa Seleli alikuwa kila siku anasema kiwango cha udongo, cha udongo. Siku hizi hazungumzii Nzega - Shelui kwa sababu imeshamalizika kutengenezwa kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, kama tulivyomaliza Nzega na Shelui, nataka kumthibitishia Mheshimiwa Mbunge kwamba na ile sehemu iliyobaki tutaendelea kuishughulikia ili kusudi iweze kutengenezwa kwa kiwango cha lami kulingana na kupatikana kwa fedha na uwezo wa uchumi wa nchi yetu.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika mchango wangu nilinukuu majibu ya Mheshimiwa Waziri alipokuwa akijibu swali langu. Kwa mantiki hiyo, naomba nimwulize kwa kupitia Vote 47 program ya 10

kifungu kidogo cha 1001. Katika majibu yake haya ya swali langu la nyongeza siku ya jana swali Na. 147, Mheshimiwa Waziri aliniambia ametenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa daraja litakalounganisha nchi ya Tanzania na Msumbiji kupitia eneo la Mhukulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wananchi wa Mkoa wa Ruvuma wamefurahi na wamepokea kwa shangwe kauli ya Mheshimiwa Waziri wakati akijibu swali langu hilo siku hiyo ya jana. Lakini bahati mbaya baada ya kupitia maelezo yote ya Waziri na vitabu vyake vyote sijaona mahali popote palipotengwa fedha hiyo. Kwa hiyo, nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri anisaidie sana mimi pamoja na wananchi wa Mkoa wa Ruvuma waliomsikia akijibu swali langu jana, kusherekea pamoja naye kwa kunionyesha tu eneo gani fedha hizo amezitenga ili basi tuanze kushirikiana kwa pamoja katika ujenzi wa daraja hilo. Ahsante.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Ruvuma na Mtwara, unapakana na Msumbiji na una urefu wa zaidi ya kilometa 800. Swali la Mheshimiwa Mhagama lilizungumzia daraja la kuunganisha na wenzao wa Msumbiji. Jibu langu la nyongeza nililojibu jana ni kwamba kwa sasa hivi kuna daraja la umoja ambalo limetengewa Shilingi bilioni 4.5 za Tanzania na Dola milioni 4.5 za Msumbiji ambazo zitaweza kuiunganisha Msumbiji. Kwa hiyo, kama ni kusherekea, ninamwomba Mheshimiwa Mhagama akasherekee kwa sababu watakuwa wanatumia daraja la umoja kuvuka kwenda Msumbiji. Lakini kwa sababu eneo hilo ni refu, kuna mipango mingine ya baadaye ambayo itaendelea ili kusudi pawepo na *unity bridge number two* na *unity bridge number two* ndio itakayokuwa imepangwa kutengenezwa katika upande wa Ruvuma.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu ya Waziri ingawa kwa kweli jana nilikuwa *very specific* na nilizungumza eneo la Mkoa wa Ruvuma katika Kijiji cha Mhukulu na sio Daraja la Umoja. Nilipongeza Daraja la Umoja, lakini nashukuru kwa majibu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hata hivyo katika eneo la Mkoa wa Mtwara, nchi yetu ya Tanzania inaunganishwa na Msumbiji kwa matarajio ya ujenzi wa daraja hilo kubwa sana katika eneo la Masasi, sehemu inayoitwa Mtambaswala. Lakini katika Mkoa huo huo wa Mtwara, yako tena mahusiano ya nchi ya Tanzania na Msumbiji kwa kutumia *ferry* ambayo ni ya mahusiano ya kiurafiki kupitia *TAMOFA* ambayo inafanya kazi katika eneo la Kitaya ndani ya Mkoa huo huo wa Mtwara.

Sasa kwa hali hiyo: Je, Mheshimiwa Waziri wakati tunasubiri wananchi wa Mkoa wa Ruvuma kujengwa daraja la pili la umoja, yuko tayari aidha, kuhamisha *ferry* hiyo kutoka katika Mkoa huo wa Mtwara na kuileta katika Mkoa wa Ruvuma kwa sababu Daraja la Umoja linajengwa kule ama Mheshimiwa Waziri yuko tayari kutujengea hata daraja la chuma wakati tukisubiri ili kutengeneza uwiano wa mahusiano kati ya nchi ya Tanzania na Msumbiji kwa kutumia Mkoa hiyo miwili?

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua nikizungumzia juu ya kuhamisha *ferry* ya Chilambo kuipeleka pale Mtomoni, wananchi wa Mtwara na Wabunge wa Mtwara hawatakubali. Lakini kuamua pia daraja linalojengwa sasa hivi

Mtambowa Swala linalounganisha *province* Kepudegado ya Msumbiji pamoja na Tanzania ambayo Rais Mheshimiwa Benjamini William Mkapa na Mheshimiwa Chisano, walisaini Mkataba katika Mji wa Pemba kwa ajili ya kulitengeneza lile daraja, itakuwa ni kukosa nidhamu na hasa sisi Wana-CCM.

Kwa hiyo, ombi la Mheshimiwa Mhagama, sisi tunalichukua kama *challenge* kwa Wizara na kwa vile tumeshapatambua pale Mtomoni kwamba pana uwezekano wa kutengenezwa daraja, ningemwomba dada yangu Mhagama kwa ahadi zote na kwa vile wataalam wote wako hapa, tutaanza kulifanyia kazi angalau tujue ikiwezekana tutakapopata fedha hata mwaka kesho hata mwaka kesho kutwa pale napo litengenezwe daraja. (*Kicheko*)

Lakini kwa sasa hivi ningemwomba Mheshimiwa Mhagama atubane kwa barabara ya kutoka Masasi – Tunduru - Songea hadi Mbambabay ambayo nina uhakika wananchi wa Songea na Ruvuma wanaihitaji pia, lakini na daraja lile ni muhimu kwa sababu kwanza ni *mile* kama 100 tu kwenda pale. Kwa hiyo, hayo ndio maelezo ambayo ningeweza kuyatoa.

**MWENYEKITI:** Mhagama atasubiri. Anafuata Mheshimiwa Omar S. Kwaangw’.

**MHE. OMAR S. KWAANGW’:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *vote* ni hiyo hiyo 47 *program* ni 10 *sub vote* ni hiyo hiyo 1001. Ni suala la ufafanuzi ambao ningependa nijitoe mashaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipochangia kuhusu ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kujenga barabara ya kudumu kutoka Babati kwenda Wilaya ya Simanjiro na Kiteto, Naibu Waziri wakati anahitimisha wakati anajibu alisema kwamba, utaratibu wa kufikisha ahadi ya Mheshimiwa Rais ni lazima Mkuu wa Mkoa huo apeleke Wizarani. Sasa kwa sababu kati ya waliyozungumzia ahadi za Rais ni mimi, nataka mashaka haya yaondoke kwamba hivi ni kweli kwamba labda Mheshimiwa Naibu Waziri anataka kuniambia kwamba Mkuu wangu wa Mkoa hajawahi kuleta ombi hili kulifikisha Wizara ya Ujenzi? Hilo la kwanza.

La pili, nitakuwa nimeliondoa kwa sababu Mheshimiwa Waziri amekubali kwamba sasa ahadi ya Rais imepokelewa rasmi kama ombi maalum Wizarani kwake. Kwa hiyo, hilo nimeliondoa, lakini katika maelezo ya Naibu Waziri wakati anajibu hoja, alisema jambo ambalo ilibidi niangalie kitabu mara moja, alisema kwamba yeye kwake kule kwa bahati mbaya hana barabara ya lami na kwa kweli sio vizuri kwa Wabunge pengine kuamua kusema fedha ziende kwenye barabara ipi. Akasema kazi hii ni vizuri ikafanywa na Wizara ili kuondoa upendeleo na pengine kutokuelewana.

Sasa nilipokuwa naangalia kwenye kitabu, nataka tu ufafanuzi na kuniondoa mashaka kwenye ukurasa wa 144 kama vigezo. Nataka kujua vigezo ambavyo Wizara inatumia kupanga sasa barabara zipi zitengenezwe. Katika ukurasa wa 144 chini ya *Regional Roads under consolidated financing* na nitatoa mfano kwa Mkoa wake wa

Morogoro, una barabara kama 23 pamoja na madaraja ambayo yako chini ya *rehabilitation* katika utaratibu huo. Lakini nikaangalia na Mkoa wa Manyara ni mbili, hata ukichanganya na tulivyokuwa Mkoa mmoja wa Arusha ziko tano chini ya kifungu hicho. Sasa nataka kujua ni vigezo gani vinatumika na uwiano gani katika kuchagua barabara kwamba Mkoa mmoja unaweza kuwa na barabara mbili tu chini ya *rehabilitation*? Nyingine 23 na ukiangalia hata Mikoa mingine, hoja hii inahitaji kutazamwa vizuri sana kama kweli ni wataalamu wanafanya hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Mkoa wa Manyara naufahamu vizuri sana, unao matatizo mengi ya barabara ambazo nyingi zingeweza kufanyiwa *rehabilitation*. Sasa ningepomba Mheshimiwa Waziri anisaidie kuhusu kunitoa mashaka kwamba Mkoa haukuwasilisha kwake kama alivyoelekeza Naibu Waziri au alikuwa na maana ya Mikoa mingine na hilo lingine? Ahsante.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Kwaangw'. Kuhusu majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri alizungumzia kuhusu utaratibu, kwamba Mheshimiwa Rais anapofanya ziara katika Mkoa au katika Wilaya yoyote na anapotoa ahadi katika taratibu za kiserikali, uongozi wa Mkuu wa Mkoa huwa wanaandika na kuzileta kwa kila Wizara inayohusika kutokana na zile ahadi zilizotolewa. Lakini kwenye suala hili la barabara inayounganisha Mji Mkuu wa Manyara – Babati, ahadi ya Mheshimiwa Rais ilitolewa kwa maandishi kwa kuandikiwa sisi na kuingizwa. Aliagiza kupitia Wizara ya Tawala za Mikoa pamoja na sisi Wizara ya Ujenzi.

Kwa hiyo, isingeweza kuanzia Mkoani wakati tayari tulikuwa tumekwishaagizwa huku. Ninachotaka kumthibitishia Mheshimiwa Kwaangw' hili agizo la Mheshimiwa Rais limeshatolewa kwetu Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Tawala za Mikoa, tunajukumu la kulitekeleza na ndio maana siku ile ulipozungumza humu Bungeni nilikusikia nikawaambia wataalam wangu wekeni Shilingi milioni 500 na tulifanya hivyo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Kwaangw' nataka kukuthibitishia kwamba tutaendelea kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais, wala hatuhitaji kupata barua kutoka kwa Mkuu wa Mkoa kwa sababu tayari tumeshapewa maelekezo hapa.

Lakini nataka kukuthibitishia pia kwamba hiyo barabara tutaitengeneza tutaanza kuitengeneza. Kama nilivyojibu kwa majibu yangu ya msingi, nilisema tutaendelea kuangalia kutafuta hata Wafadhili ambao wanaweza kutusaidia katika kuiwezesha hiyo barabara itengenezwe. Barabara ni ndefu, kilometa 250 lakini tutajitahidi kwa uwezo wetu kuifanya ipitike.

Kuhusu mgao wa fedha ambazo zinatolewa katika kitabu hiki, ukianzia kiambatanisho Na. 4 mpaka viambatanisho Na.9, tumezungumzia kuhusu barabara za *trunk roads* na *regional roads*. Kwa hiyo, kiambatanisho hiki kiko kwenye ukurasa wa 144 hakiwezi peke yake kutumika kama fedha ambazo zimetengwa katika Mkoa wa Morogoro. Kuna viambatanisho vingine ambavyo vimetaja fedha kwa ma-*group* ukiangalia kwa mfano kiambatanisho No. 4D utaona Tanga wamewekewa Shilingi

milioni 62, unakuta Manyara wamewekewa Shilingi milioni 188. Ukiangalia viambatanisho vingine, vinatofautiana hivyo hivyo.

Kwa hiyo, lengo kubwa ni ku-include miradi mingi iliyomo kwenye barabara ambayo inaweza kushughulikiwa na Wizara kulingana na fedha zinazopatikana. Kuna fedha za *road fund*, kuna fedha za *development fund* na kuna fedha nyingine zinazotoka kwa Wafadhili, utaona kwa mfano katika fedha za *STABEX* Wilaya ya Karagwe imepata barabara nyingi sana katika fedha za *STABEX*. Karibu fedha zote za Karagwe zimekuwa *included*. Wakati Biharamulo hakuna barabara hata moja pamoja na kwamba tunalima kahawa. Kwa hiyo, haya yanatokea. Ukiangalia Ruvuma wana fedha za *RUSIRM* zaidi ya Shilingi bilioni 34 lakini Mikoa mingine hawana fedha za *RUSIRM*. Ukiangalia Singida, wanafedha za *ADB* pamoja na Tabora na Mtwara. Ukiangalia kwa mfano *Coast* wanafedha za *DANIDA* na Tanga, Mikoa mingine hawana. Kwa hiyo, haya ndio yanayotengeneza *differences* kutoka Mkoa hadi Mkoa. (*Makofi*)

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, kifungu ni 47 *program* ya 10 mshahara wa Mheshimiwa Waziri. Wakati ninachangia Ofisi ya Waziri Mkuu nilizungumzia suala la barabara hasa kutoka Mkuranga kufika Kibiti. Barabara hii inakwenda kwa mwendo wa kinyonga. Serikali inaweza kutuambia toka Bajeti ya mwaka 2000 hadi hii leo wametengeneza Kilometa ngapi? Ahadi ya Serikali kwamba tutakwenda kwa *taxi* kutoka Mwanza mpaka Mtwara kama kipande hiki hakitengenezwi na niliomba katika mchango wangu kwamba, basi tunaomba kama Serikali inakwenda taratibu, yale mashimo ya lami yaliyopo eneo lilobaki toka Mkiu kufika mpaka Kibiti wayakwangu. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, katika mchango wangu wa maandishi nimezungumzia juu ya alama za barabarani za mkandarasi wa kutoka Nangurukuru kwenda Mbwemkulu, alama zile ni fupi mno, ni ndogo! Kama upo kwenye gari, labda uwe kwenye gari dogo *salon* ndio alama zile utaziona kwa urahisi. Ni fupi, vialama vyembamba, vidogo na vinawekwa papo kwa papo: Je, mtumishi wa Wizara aliyeko pale anaridhika na alama za barabarani? Haoni kwamba tunaweza kusababishiwa ajali kwa kuwekewa alama ndogo sana kana kwamba sisi Kusini hatuna mbao? Naomba maelezo.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona leo kila mmoja anataka mshahara wangu. Lakini mshahara ninaoupata ni wa Ubunge. Uwaziri nafanya bure. (*Kicheko*)

Suala la Mheshimiwa Watondoha kuhusu barabara ya Mkuranga Kibiti ni muhimu. Sehemu hii ya barabara ilikuwa inatengenezwa kutoka fedha za wa *Kuwait Fund*, ni kwa bahati mbaya wakandarasi waliokuwa wanashughulika pale *TANROADS* hawakuweza kupata fedha kutoka Kuwait. Kwa hiyo, mradi ukawa umedorora kuanzia mwaka jana. Sasa kutokana na fedha ambazo zilikuwa haziletwi na matatizo ya *consultant* aliyekuwa hapo, Wizara tumekwishachukua hatua. Kwanza yule *consultant* aliyekuwa anasimamia kazi pale tumeshamfukuza na tumetenga zile fedha zilizokuwa kwenye Bajeti ya mwaka jana 2004 kwa ajili ya barabara ya Kilwa, kwa vile ile ni barabara moja tumezisogeza kwenda mbele kwenye barabara ya Mkuranga - Kibiti.



Kwa hiyo, kandarasi ataendelea kutengeneza pale na kilometa zitapungua. Nataka kumthibitishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika bajeti ya mwaka huu 2005/2006 hiyo sehemu itaweza kushughulikiwa vizuri. Lakini pia katika bajeti ya mwaka huu tumetenga karibu Shilingi milioni 675 ukiangalia katika *paved trunk roads* ukurasa wa 125. Kwa hiyo, nataka kumthibitishia Mheshimiwa Watondoha kwamba hiyo sehemu itaendelea kutengenezwa kwa kiwango cha lami.

Lakini pia lingine ambalo lilizungumzwa la sehemu ya Ndundu Somanga napo kuna *consultant* ambaye anaendelea kufanya *design*, anatakiwa amalize kwenye mwezi wa tisa au wa kumi na moja na katika kipindi hicho zitatangazwa *tender* kwa ajili ya kuanza kutengeneza napo kwa kiwango cha lami kutoka Ndundu hadi Somanga. Kwa hiyo, hii ndio taarifa ya Mkuranga - Kibiti.

Kuhusu alama za barabarani za kandarasi, sasa kandarasi yuko kule, wewe unakimbia, *speed* ya nini? Lakini tutaliangalia. Lakini kitu kikubwa wananchi wanahitaji barabara iliyotengenezwa kwa lami, tumuache kandarasi aendelee kutengeneza barabara yake ya lami, sasa hizi alama zitawekwa wakati barabara ya lami itakapokamilika. Alama zilizoko sasa hivi ni za *temporary*, za kukujulisha hapa kuna shimo au nini, barabara ikishamalizika kutengenezwa kwa lami, alama za barabarani zitawekwa.

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, sisi tunafahamu kwamba alama za barabarani zitawekwa, lakini wakati wanajenga kuna *diversions*, kuna matuta, sasa hizi *diversion* wanaweka hapo hapo kwenye *diversion* ndio unakuta kibao tena kifupi, lakini ukiangalia barabara hii inatoka Morogoro kuja huku, *diversion* zinaonekana mbali *at least half a kilometre away* unaona alama. Hawa wanaweka alama pale pale. Sasa ndio nauliza, hivi wataalam wetu wanaridhika alama zetu kuweka papo kwa papo? Sio alama za barabarani za kawaida? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili nampongeza Mheshimiwa Waziri kwamba ametutengea fedha za kutoka Mkiu kuelekea Kibiti: Je, hizi zitafika mpaka Kibiti? Kama hazifiki atatuhakikishia kwamba yale mashimo ya lami yanakwanguliwa angalau tupunguze kuvunja *spring*? Nakushukuru.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeeleza kwamba fedha zilizokuwa zimetengwa mwaka jana kwa ajili ya barabara ya Kilwa zimehamishiwa kwenye barabara hiyo. Mwaka jana 2004 palikuwa na Shilingi bilioni mbili na mwaka huu tumeongeza nyingine. Sasa hizi fedha ni idadi tosha ya kuweza kumaliza kilometa 45 za barabara.

La pili, kuhusu huyu kandarasi kuweka alama za barabara fupi, nitawatuma Wahandisi wangu wakaangalie na wakausome Mkataba wao yanasema nini. (*Makofi*)

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na mimi kusemea *vote 47 program Na.10 sub vote 1001, 250 na 100* mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napenda nieleze kidogo. Kwanza ningependa kuishurukuru Wizara ya Ujenzi pamoja na Wizara ya Fedha, kwamba majibu waliyotoa kuhusu ujenzi wa barabara ya kutoka Tunduma kwenda Sumbawanga yameturidhisha wote na tunaishukuru Serikali kwa hatua hiyo. Kwa hiyo, sina hoja yoyote ya kutoa Shilingi na wenzangu tumefurahi pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili Mheshimiwa Waziri anajua huu ni mwaka wa tatu na mimi sijawahi kulalamika hapa Bungeni kuhusu Wizara hii. Kwa sababu ninaamini kwamba kukutana kwenye Ofisi za Mawaziri kunasaidia, sio lazima mtu upige kelele humu. Sasa tunazo barabara mbili, barabara ya kutoka Mamba kwenda Kasansa mpaka Muze. Barabara hii Naibu wake alikwishakuja akaiona, haipo! Kwanza na usafiri wa kule sasa watu hivi leo miaka 40 ya uhuru wanatumia punda kubeba mizigo, Naibu Waziri aliona.

Fedha ambazo zimetengwa tangu miaka mitatu iliyopita, ni Shilingi milioni 60 ambazo kwa kutengeneza barabara hii kutoka Mamba mpaka kwenye Jimbo langu itachukua miaka sita na barabara hiyo inaunganisha Wilaya mbili, Wilaya ya Mpanda na Wilaya yetu. Sasa barabara hii inatengenezwa kuanzia ile Wilaya nyingine.

Kwa hiyo kwangu itakuja kufika baada ya miaka sita, lakini kwenye jina inasomeka Mamba – Kasansa – Muze, lakini Muze itakuja kufika baada ya miaka sita. Kwa hiyo, nilikuwa nataka kuwaomba Mawaziri wanieleze sasa tunafanyaje? Maana hata mwaka huu umetenga fedha Shilingi milioni 60. Shilingi milioni 60 ni kilometa sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, kuna barabara ya kutoka Kizwite mpaka Mpui kupitia Mkima Kilometa 56 nayo mwaka jana 2004 ilitengewa Shilingi milioni 50 na mwaka huu 2005 Shilingi milioni 50 na mabasi sasa yameacha kupita njia hii kwa sababu ya ubaya wa barabara. Kwa hiyo, nilikuwa nataka nipate maelezo kwa Waziri, tunafanyaje katika jambo hili? Maana kuandikiana sasa nimechoka labda niseme hapa hapa.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anachozungumza Mheshimiwa Mzindakaya ni kweli nimekwenda, nimeiona barabara hii. Hii barabara imekufa na tunachojaribu kufanya ni kutoa pesa kidogo kidogo ili barabara hii iendelezwe. Ni bahati mbaya tu kwamba kiwango chenyewe cha pesa hakitoshelezi mara moja.

Lakini tumepanga Shilingi milioni 60 kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge na nadhani tutajitahidi tuone kwamba hiyo miaka sita anayozungumza yeye haifiki, kwa sababu mwaka jana 2004 tumepanga Shilingi milioni 60 na mwaka huu tumepanga Shilingi milioni 60. Kwa kawaida katika utekelezaji huo kuna madaraja vile vile na makalvati ambayo tumeyapangia. Naomba Mheshimiwa Mbunge aangalie hilo vile vile kwamba kule kwake kuna makalvati na madaraja mengi sana ambayo tumepanga na nilipita kwenye mito kusema kweli na kuna madaraja haya.

Kwa hiyo, tunajitahidi kwa uwezo wetu wote kusaidia, kuhakikisha kwamba barabara hii inatengenezwa. Najua inatoka kwa Mheshimiwa Mizengo Pinda inakwenda kwake na anaiona inakwenda pole pole, lakini haikuwepo kabisa. Kwa hiyo, kwa juhudi hii sasa hivi tunaifufua.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sidhani kama hayo ni majibu. Siyo majibu kwa sababu mimi nataka barabara kwenye Jimbo langu. Hii barabara inatoka Mpanda itafika kwangu baada ya miaka mitano na hayo *ma-drifter* anayosema hayatengenezwi kwenye barabara ya Wilayani kwetu. Mwenyewe ameona mimi sisemi, huwa sizui mambo, nasema jambo ambalo ameona kwa macho yake. Kwa hiyo, nasema kutenga Shilingi milioni 60 kila mwaka, kwangu itafika baada ya miaka sita. Sasa mimi nafanya kazi gani ya Ubunge?

Halafu Jimbo langu ndio linalisha Serikali, linatoa ziada ya mpunga hata katika eneo hili na punda ndio wanabeba. Mwenyewe kaona punda wamebeba mpunga. Sasa kwa sababu mimi sitaki tubishane, naomba Waziri mwenyewe akubali tufanye kikao kati yangu mimi, Waziri mwenyewe na Waziri wa Fedha waniambie watasaidiaje hili jambo ili tusipoteze muda wa Bunge. Maana sisi wote ni binadamu. Barabara zangu zote naomba Waziri akubali tufanye kikao na Waziri wa Fedha, tuone watanisaidiaje kuhusu barabara hii, lakini hilo sio jibu analotoa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakubali kufanya kikao kati ya Mheshimiwa Mbunge na Waziri wa Fedha tuone tutamsaidiaje. (*Makofi*)

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif.1002	-	<i>Finance and Accounts...</i>	Sh. 288,418,100/=
Kif.1003	-	<i>Policy and Planning ...</i>	Sh. 420,817,300/=
Kif.2001	-	<i>Electrical and Mechanical...</i>	Sh.2,162,310,300/=
Kif.3001	-	<i>Supplies and Services ...</i>	Sh.1,844,898,500/=
Kif.5001	-	<i>Buildings ...</i>	Sh.3,488,385,800/=

*(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif.6001	-	<i>Trunk Roads ...</i>	Sh. 61,858,028,800/=
----------	---	------------------------	----------------------

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi hii na nitakwenda moja kwa moja kwenye *Sub vote 6001 item* ya kwanza kabisa *Basic Salaries* ya 2025100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiwa Singida Mjini ukaelekea Singida Kaskazini katika Kijiji cha Mtinko, kuna Hospitali ambayo Naibu Waziri anaifahamu sana, ni kubwa na maarufu, ilijengwa na wenzetu kutoka Uholanzi. Wizara imeipa hadhi ya

Hospitali, lakini barabara yetu kwenda Mtinko kila baada ya mwaka mmoja inaharibika kabisa. Kwanza kutokana na hali ya udongo na kutokana na mvua zinavyoendelea, haijawahi kutengenezwa ile barabara ikakaa miaka miwili. Hali kadhalika ukitoka Mtinko kwenda Jimbo la Iramba Mashariki kuna Hospitali nyingine ya Kanisa la Kilutheri. Katika hizo Hospitali mbili wagojwa wengi sana wanapoteza maisha kutokana na ubovu mkubwa sana wa barabara, kunakaa watu zaidi ya laki tatu hadi laki nne katika yale maeneo na wote wanatumia hizo Hospitali. Ningeomba nimwombe tena Mheshimiwa Waziri kama nilivyochangia huko nyuma, ni lini hii barabara kutokana na heshima yake na kutokana na umuhimu wake wa hizi Hospitali mbili kama ambavyo Serikali imefanya kwa baadhi ya Wilaya, ni lini wataipa kipaumbele hii barabara ijengwe kwa kiwango cha lami?

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii barabara anayoizungumzia ya kwenda Hospitali ya Mtinko, kwanza nafikiri hii barabara ya kwenda Hospitali ya Mtinko haiweze ikawa *Trunk Road*. Kwa sababu kwenye *item* tunayoishughulikia hapa ya *Trunk Roads* ni barabara inayotoka Singida kuja Manyoni na kutoka Singida kwenda Shelui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii anayoizungumza, nafikiri haiwezi ikawa katika *item* hii. Lakini kwa heshima ya Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, yeye anaomba barabara ya lami wakati hata ile Singida – Manyoni bado haijatengenezwa kwa lami ambayo ni *Trunk Road*. Wakati hata Tunduma, Sumbawanga hadi Kigoma ambazo ni *Trunk Roads* bado hazijatengenezwa lami, wakati hata Geita hadi Mwanza ambayo ni *Trunk Road* haijatengenezwa kwa lami, wakati hata Itigi – Tabora, Kaliuwa hadi Kigoma haijatengenezwa kwa lami. Kwa hiyo ni ombi ambalo liko nje ya uwezo wangu na liko nje ya uwezo wa Wabunge hawa wote. Lakini kama barabara hiyo anayoizungumzia inapita kwenye *Trunk Roads*, basi kuna hatua ambazo zimechukuliwa na Serikali sasa hivi za kutengeneza barabara ya *Trunk Road* ya kutoka Manyoni hadi Singida mpaka Shelui kwa kiwango cha lami na makandarasi wako kule.

Hicho ndicho naweza nikasema. Lakini kama hizi barabara anazozitungumzia ni michepuo kutoka kwenye *Trunk Roads*, basi labda atulettee tuzungumze tuone ni namna gani tunaweza tukafanya, kwa sababu inawezekana barabara ni ya Wilaya au ni *regional roads* na kadhalika. Lakini ukweli tunazingatia sana umuhimu wa Hospitali zetu kupata barabara nzuri katika kuokoa wananchi wanaopelekwa kwenye Hospitali hizo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif.7001 - *Regional Roads* ... .. Sh.1,606,450,400/=

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Tafadhali Mheshimiwa Waziri, naomba ufafanuzi zaidi katika *Sub vote Na.7001 Regional Roads*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge naomba umwambie Mwenyekiti.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi zaidi katika *Sub vote 7,001 Regional Roads*. Kuna mpango gani rasmi kwa ajili ya kuboresha barabara ya Nangurukuru kwenda Lindi ili iweze kupitika kipindi chote na kutoka Nangurukuru kwenda Liwale na kutoka Liwale kwenda Nachingwea, kwa kuwa kuna kilometa 30 kutoka Liwale ambazo zina mchanga mwingi sana na kilometa 230 kutoka Nangurukuru kwenda Liwale hazipitiki wakati wa masika? Kwa hiyo, wananchi wa Liwale kipindi chote wanakuwa hawana usafiri wa aina yoyote kuwafikisha katika Wilaya hiyo.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa maelezo kwamba mkandarasi anayefanya kazi kati ya Nangurukuru na Lindi amepewa jukumu pia la kuihakikishia hiyo barabara iwe inapitika kwa wakati wote, wakati akiendelea kutengeneza hiyo barabara. Kuhusu barabara ya Nangurukuru – Liwale katika Bajeti ya mwaka huu 2005 napenda kumthibitishia Mheshimiwa Mbunge kwamba kuna fedha ambazo tumezitenga ambazo zitatumika kwa ajili ya kuhakikisha ile barabara ya Nangurukuru – Liwale inapitika katika siku zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana 2004 tulishughulikia baadhi ya madaraja, mwaka huu tunashughulikia barabara yote iweze kupitika. *(Makofi)*

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi kama utekelezaji utafuatia.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

#### **MIPANGO YA MAENDELEO**

Kif.1001 – *Administration and General...* Sh.100,000,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif.6001 – *Trunk Roads...* Sh.248,789,933,900/=

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Vote 47 Sub vote 6001 Trunk Roads item 4180* barabara ya Tunduma – Sumbawanga inaendelea mpaka Mpanda – Kigoma. Fedha zilizotolewa ni Shilingi bilioni 1.7, ambazo naziona ni fedha ndogo sana ukilinganisha na maeneo mengine ambayo wamepewa fedha na barabara hii kwa muda mrefu tumekuwa tukiilalamikia. Nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri aniambie hasa fedha chache kiasi hiki zinafanya kazi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, katika Mkataba waliosaini jana kama alivyotueleza hapa, barabara itakayoendelea kutoka Sumbawanga mpaka Mpanda

naomba nijue tu inapitia sehemu gani inapotoka Sumbawanga kwenda Mpanda. Maana kilio cha wananchi ni kwamba barabara ipitie Makao Makuu ya Wilaya kama vile Mheshimiwa Rais alivyoahidi na wewe mwenyewe kwamba itapitia huko. Nilikuwa naomba tu nifahamu itapita wapi?

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ponsiano Nyami aliposimama kuzungumzia kuhusu Tunduma – Sumbawanga nikakumbuka na maneno ya Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya ambayo ameyasema dakika chache zilizopita kwamba hana matatizo na Tunduma – Sumbawanga. Lakini ninachotaka tu kueleza hapa ni kwamba fedha zilizotengwa kwa ajili ya Tunduma – Sumbawanga ni Shilingi bilioni 1.705.

Huu mradi unashughulikiwa na Benki ya Dunia. *Feasibility study* za mwanzo zimekwishamalizika, *detail design* ndizo zinamalizia pamoja na kutangaza *tender* ya kuanza ujenzi. Sasa zilitengwa hizi bilioni 1.7 ni katika *estimate* kulingana na fedha za Wafadhali. Lakini Wafadhali *wameshaji-commit World Bank* kwamba wataishughulikia hii barabara kwa kutoa fedha zote kwa Kilomita 230 kwa ajili ya kutengenezwa kwa kiwango cha lami. (*Makofi*)

Kuhusu sehemu ya Sumbawanga – Mpanda kwamba itapitia wapi, ndio maana tumetangaza *design*. Kwa hiyo, sifahamu itapitia wapi. Ie *design* iliyosainiwa jana ikishamalizika ndio watatueleza ni mahali gani *economically* panafaa kupitishwa barabara. Nina uhakika kwenye Makao Makuu ya Wilaya lazima barabara ipite pale ili kusudi wananchi wengi waweze kusafiri na kuitumia ile barabara katika kuendeleza nchi na kuleta uchumi na kujenga uchumi wao pia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hayo ndio majibu ambayo ningeweza kuyatoa kwa rafiki yangu Mheshimiwa Ponsiano Nyami.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nishukuru kwa majibu hayo mazuri, lakini kidogo yamejificha. Pale aliposema wataalam watakapokuwa wanafanya *PVV*, wao ndio wataona *economically* ipite wapi. Lakini mwishoni anasema inazingatiwa kupita Makao Makuu ya Wilaya ambako kuna wananchi wengi. Endapo *PVV* yao itasema kwamba haitapita huko Wilayani *economically*, lakini Rais alisema itapita hapo na yeye mwenyewe alisema itapita hapo. Je, ahadi hizo zitakuwa zimedharaulika au itakuwaje?

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ni kama kuanza kubishana ng’ombe ambaye yuko tumboni na bado hajazaliwa. Mimi ningeomba tusubiri hii *design* imalizike, kwa sababu katika uamuzi wa barabara inapita wapi, pia kuna *political decision*. Kwa hiyo, wakati ule utakapokuwa imemalizika *design*, jibu litatoka la uhakika. Mimi sikuteuliwa jana kufanya *design* ya barabara hiyo, ndio maana zinalipwa hela mamilioni mengi kwa ajili ya kuanza kufanya *design*. Kwa hiyo, ningemwomba Mheshimiwa Ponsiano Nyami avumilie wamalize *design*. Wakishamaliza, *decision* ile itatolewa. Lakini ninachotaka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge ni kwamba barabara zinajengwa kwa ajili ya watu. Kwa hiyo, haiwezi ikapitishwa mbali na Makao Makuu ya

Wilaya kwa sababu lengo kubwa ni kutoa huduma kwa wananchi walio wengi, hicho ndicho naweza nikamthibitishia. (Makofi)

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukura sana. Kifungu hiki cha 6001, *item* 2352 Singida – Shelui. Wakati nikichangia nimepongeza kazi nzuri ambayo Wizara inafanya na nikakumbusha kwamba sasa hivi kuna wakandarasi ambao wamepewa kipande cha barabara hiyo ya Shelui mpaka Singida. Lakini barabara ya kutoka Mwanza mpaka Dodoma pabovu kuliko mahali pengine popote, ni pale mlimani Sekenke na kwa utaratibu wa Wizara mkandarasi akishapewa kazi uhakikishe sehemu zote anazifanyia marekebisho. Sasa nilishauri, kwa sababu sehemu ile watakayoifanyia itapita nje ya mlima ule wa Sekenke: Je, Wizara itaangalia kutengeneza pale mlimani kuhakikisha barabara ile inapitika wakati wote, wakati matengenezo yakiendelea katika eneo lile lingine? Wakati nikichangia nimepongeza na kutoa shukrani za wananchi wa Nzega kwa kazi nzuri ambayo imefanyika na hadi lami ikaingia hadi Mjini Nzega. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikumbusha kwamba katika ile *diversion* ya kuingia Nzega kutoka kwenye *highway* ipo kona kali sana ambayo inaangusha magari na tumeiita kona ya Magufuli. Sasa nikaomba ili kuepusha vifo na ajali mbalimbali pawekwe *round about* ambayo haitafanya kona ile paangushe magari mbalimbali na kusababisha vifo. Sasa wakati akijibu, Mheshimiwa Waziri hakusema kabisa kama pale atapafanyia marekebisho ili angalau magari na watu waweze kupita bila matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya Singida – Shelui kwa sasa hivi ina kandarasi tatu. Ile sehemu ya Kilomita 108 imegawanywa kwa makandarasi watatu na fedha zimetolewa na Benki ya Dunia zaidi ya Shilingi bilioni 50. Lakini kwa kandarasi yoyote anapopewa kazi ya kutengeneza barabara, huwa anawajibika kutengeneza ile barabara nyingine kwa ajili ya kuifanya ipitike. Kwa hiyo, nataka kumthibitishia Mheshimiwa Mbunge kwamba sehemu ya Sekenke ambayo ndiyo itakuwa inatumika kama *diversion*, ataendelea kuitengeneza huyo kandarasi ili iendelee kupitika wakati akitengeneza hii barabara ya chini. Kuhusu hii kona ya Magufuli kwa vile wananchi wa Nzega wananisikia hata sasa hivi na wanania, waiite ile kona ya Selelii. Kwa sababu ni Mheshimiwa Lucas Selelii ndio amesababisha barabara ya Nzega hadi Shelui iweze kupatikana kwa juhudi zake kubwa ambazo amezifanya. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo mengine ambayo yatakuwa yanajitokeza ile barabara inategemewa kufunguliwa mwezi unaokuja na Mheshimiwa Rais. Kwa kawaida barabara ikifunguliwa huwa inakaa chini ya uangalizi wa kandarasi kwa mwaka mzima. Kwa hiyo, tutamweleza kandarasi aweze kuiangalie pia hiyo kona ya Selelii isiendelea kuangusha magari na kusababisha vifo. (Makofi)

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kifungu 7001 – *Regional Roads* ... .. Sh.20,977,400,000/=

**MHE. ABDULKARIM ESMAIL HASSAN SHAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Mimi labda kwanza nimfahamishe Mheshimiwa Waziri kupitia kwako kwamba katika mchango wangu wa maandishi niliouchangia, nimeeleza masuala ya vifaa vya barabara pamoja deni ambalo wananchi wa Mafia wanam dai mkandarasi.

Lakini labda tu niseme kwamba kuhusu vifaa vya barabara nilikuwa namwomba tu Mheshimiwa Waziri, aliniambia kwamba kabla hajakwenda Biharamulo Kagera katika hii shughuli iliyofanyika hivi karibuni na Mheshimiwa Rais, kwamba atahakikisha anawaambia Watendaji waweze kufanikisha Wilaya ya Mafia yaani *kuwa-commit* kwamba Wilaya ya Mafia tuweze kupata vifaa hivi ama kwa kushirikiana na Wizara ya TAMISEMI. Sasa nilikuwa nataka hili aliseme hapa ili liwe katika *Hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili nimepitia katika hii *Sub-vote 7001 item Na.4132 Regional Roads*, nimepitia kitabu hiki chote cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri aliyoitoa nimeona hakuna mahali palipozungumza barabara ya Rasimkumbi – Utende - Mafia, barabara ya Mkoa. Barabara hii sasa hivi ni mbaya sana, yaani ni mtihani mkubwa sasa hivi ukitamka Kiongozi yoyote, Mheshimiwa Waziri yoyote anapotamka *Southern Corridor*, basi Wabunge wa Mkoa wa Lindi, Mtwara, Ruvuma wanapiga makofi mengi sana. Lakini nilivyotaja Mafia ni mtu mmoja tu maskini mama yangu pale amepiga makofi. (*Makofi*)

Sasa labda inaonekana kama hakuna uzito mkubwa sana kwa Mafia. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri atueleze tu, atuhakikishie: Je, hii barabara mwaka huu ina maana ndio tutaendelea kuwa vile vile au itatengenezwa? Halafu hivi sasa katika utengenezaji wa hii barabara kama nilivyozungumza kwamba kuna watu ambao wanadai mkandarasi Kampuni ya *TANROAD* ambayo anadaiwa Sh.1,873,000/= na wananchi ambao alichukua au kukodisha vifaa vyao, sasa hivi hakuna kitu na kila ninapompigia simu, basi yule bwana hataki kusema.

Sasa nilikuwa nataka kupitia Bodi ya Wakandarasi, Mheshimiwa Waziri ananihakikishia vipi kuhusu kupatiwa pesa za hawa wananchi? Lakini la mwisho, nilikuwa namwomba ili aone uzito wa ile barabara, namwomba sana Mheshimiwa Waziri tufanye safari moja, tutafute *weekend* moja twende Mafia akaone yeye mwenyewe hali ilivyo sasa hivi ili apate kuona jinsi adhabu tunayoipata watu wa Mafia. Ni hayo tu nilitaka nipate malezo.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa maelezo kwa hoja iliyoulizwa na Mheshimiwa Abdulkarim Shah, kama ifutavyo:-

Ni kweli kabisa katika Kisiwa cha Mafia na Ukerewe vina suala ambalo ni muhimu kuhusu vifaa. Kwa sababu kandarasi zinapotangazwa, mtu kuamua kwenda kutengeneza kule barabara inabidi aweke gharama za kupakia kwenye meli au kukodisha kwenye meli. Kwa hiyo, gharama zinakuwa kubwa hata kama ni barabara ya udongo,



kwa hiyo, ombi la Mheshimiwa Abdulkarim Shah ni muhimu kweli na tumekuwa tukilizingatia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli pia kwamba maamuzi ya kuamua kwamba fedha za *road fund* zinunue vifaa, kikubwa kabisa yanatakiwa yafanywe na *Board* ya *Road Fund*. Lakini katika Sheria yetu tuliyoipitisha hapa *Amendment Act No.2* ya mwaka 1998 tulisema asilimia 90 ya fedha zinazokusanywa kwenye *Road Fund* ni lazima zitumike kwenye *road maintenance only, 10 percent* ndio zitumike kwenye *development project*.

Sasa kwa kuzingatia kilio cha watu wa Mafia cha siku nyingi, nataka kumthibitishia Mheshimiwa Abdulkarim Shah kwamba tutakwenda tukazungumze na wenzangu wa Tawala za Mikoa. Lakini kwa vile ile Sheria imempa mamlaka Waziri wa Ujenzi pia kuamua kuhusu matumizi ya fedha za *road fund*, nawaagiza *road fund* watenge fedha zitakazotokana na makusanyo ya mwaka huu ziweze kununulia *grader* moja kwenye Mji wa Mafia. *(Makofi)*

Lakini pia kuhusu zile barabara alizozitaja hadi ya Itende Mafia, sasa nilifikiri kwa vile sasa tutawanunulia *grader*, hiyo barabara mtaitengeneza nyinyi wenyewe. Kuhusu suala la madai wanayodai wananchi, hayo ni makubaliano yao na kandarasi. Kwa hiyo, ningewashauri Mheshimiwa Mbunge awasaidie wamshtakai yule mkandarasi. Lakini pia *Board* ya *Contractors, Registration Board* kwa kutumia Sheria Na.17 ya mwaka 1997 itafuatilia jina la huyu kandarasi ili haki iweze kutendeka kwa pamoja. *(Makofi)*

**MHE. ABDULKARIM ESMAIL HASSAN SHAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru na kumtakia kila la kheri, bahati nzuri hata kwenye mchango wangu nimeomba na dua kwa ajili yao. Lakini naomba tu niseme kwa kutumia Sheria hiyo Na.17 ya *Board* ya Wakandarasi, naomba sasa hivi Mkurugenzi aliyekuwepo hapo amesikia na bahati nzuri jana tumekutana tukazungumza na akanihakikishia. Naomba nitakapokuwa hapo nje baada ya kupitishwa hizi pesa, tuonane ili tupange mikakati mimi na yeye kuweza kuhakikisha kwamba watu hawa wa Mafia wanapatiwa pesa zao. Ahsante sana.

**MHE. EMMANUEL E. KIPOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu 47 na kifungu kidogo cha 701 nilitaka tu nipate ufafanuzi na ninaomba nihusianishe na hotuba ya Mheshimiwa Waziri katika ukurasa wa 144, kuna kiambatanisho Na.6 barabara za Mkoa wa Shinyanga. Kuna orodha ya barabara hapa na hapo mwishoni katika barabara za Mkoa wa Shinyanga kuna barabara imeandikwa Kahama Chambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ramani za barabara za Mkoa wa Shinyanga hii Kahama Chambo haionekani. Niseme tu kwamba, katika mapendekezo tuliyopeleka Wizarani ya kupandisha barabara kutoka katika Wilaya ya Kahama, tulisema hii itakuwa barabara ya Chambo Kahama Burige na barabara hii inaunganisha Mkoa wa Tabora kupitia Kahama kwenda Mkoa wa Mwanza. Sasa inavyotajwa Kahama – Chambo, mimi kidogo nashangaa kwa sababu ni barabara ndefu inayotoka mpakani mwa Mkoa wa

Shinyanga kwa maana ya Tabora kwenda mpakani mwa Mkoa wa Mwanza kupitia katikati ya Kahama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nipate maelezo hii barabara imepandishwa nusu ikaachwa nusu nyingine au namna gani?

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa maelezo ya Mheshimiwa Kipole kuhusu barabara ya Chambo – Kahama. Ni kweli hii barabara inaunganisha Mikoa miwili na barabara hii iko chini ya Halmashauri za Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tulipata maombi kutoka kwa Mbunge wa eneo hili. Sasa sifahamu hii Kahama – Chambo inamhusu nani. Kwa hiyo, baada ya kuletewa maombi hayo ambayo yanahusika na hii barabara tumetenga kiasi hiki ili kiweze kutengeneza hii sehemu iliyopo, sehemu nyingine itaweza kutengenezwa kutokana na upatikanaji wa fedha.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fungu 47, kifungu 7001, kifungu kidogo cha 4132, *Regional Roads*.

Katika mchango wangu wa maandishi pamoja na mambo mengine nilizungumzia ubovu wa barabara ya Kantoma – Kanyigo hasa katika eneo la Kaja. Eneo hili kwa kweli ni bovu sana kwa sababu ni bondeni, mvua ikinyesha maji yanakuwa mengi sana, panajaa. Eneo hili pamoja na kwamba sio eneo kubwa sana lakini kuna madaraja karibu 1000.

Nilikuwa nimemwomba Mheshimiwa Waziri kama Wizara au Serikali itafute njia ya kutengeneza sehemu hii kwa utaalum zaidi kuliko ilivyo sasa kwa sababu eneo hili ambalo ni Kilometa 42 la Kantoma - Kanyigo wakati mwingine tunapaona kama Ulaya maana inabidi uzunguke njia ndefu sana maana kipindi cha mvua nyingi sehemu hii haipitiki kabisa. Naomba Mheshimiwa Waziri anisaidie ni jinsi gani wataiangalia sehemu hii ili kuondoa dosari katika barabara za Mkoa wa Kagera hasa za Vijijini ambazo ni nzuri sana.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukifunua ukurasa 153 wa kiambatanisho Na.8, ukiangalia Kagera kuna kichwa cha habari kinachosema: “Miradi inayogharamiwa na mkopo wa Benki ya Afrika (*ADB*) na Ushirika wa Nchi Zinazouza mafuta (*OPEC*).” Chini kabisa kuna Kantoma – Kanyigo Kilometa 42. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Umekiona kifungu Mheshimiwa?

**MHE. ELIZABETH BATENGA:** Nimekiona Mheshimiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilivyoelewa kifungu hiki alichozungumzia Mheshimiwa Waziri kinatokana na kichwa cha habari kilichopo ukurasa wa 152, “Muhtasari wa utekelezaji wa miradi ya barabara za Mikoa katika mwaka wa fedha 2004/2005”.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia zaidi inaonekana kwamba katika mwaka huo Kilometa 184.9 katika barabara zilizotajwa katika kifungu hiki alichosema Mheshimiwa Waziri ni Kilometa 40 tu zilizotengenezwa. Kwa hiyo, naomba kufahamu sasa hii barabara basi imetengewa kiasi gani na je, itakamilika? Maana inaonekana mwaka jana 2004 au mwaka huu 2005 tunaomaliza ilikuwa haikutengenezwa.

**WAZIRI WA UJENZI:** Katika kiambatanisho Na.6.2, *Kagera Region*, Kantoma – Kanyigo, kinazungumzia fedha zilizotumika katika mradi unaoendelea. Kwa hiyo, ninachotaka kumthibitishia Mheshimiwa Mbunge ni kwamba barabara hii iko kwenye programu. Kwa sasa hivi siwezi kujua imefikia wapi kwa sababu katika taarifa tulizonazo hapa kuna fedha karibu Shilingi milioni 52 ndio zilikuwa zimetengwa. Lakini ninachotaka kumthibitishia ni kwamba hii barabara iko kwenye programu ya Wizara ya kutengenezwa na hata zimepatikana fedha kutoka *African Development Bank* na *OPEC Fund* ambao wamekubali kuitengeneza barabara hiyo ambayo ni mbaya sana hasa sehemu za madaraja. Kwa hiyo, hiyo barabara inashughulikiwa na Wizara na fedha zipo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati  
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Bunge Zima na kupitia kifungu kwa kifungu Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2005/2006 kwa ajili ya Wizara ya Ujenzi na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba makadirio haya sasa yakubaliwe.

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ujenzi kwa mwaka  
2005/2006 yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, Makadirio ya Wizara ya Ujenzi yamepita bila kupingwa na mtu yeyote na Mheshimiwa Waziri alikuwa na mafua lakini tunashukuru ameweza kumaliza. *(Makofi)*

Ninalo tangazo. Hapa Bungeni kuna baadhi yetu wamepokea fomu kutoka kwa *consultancy* wa *UNDP*. Mnaarifiwa kwamba wale Waheshimiwa Wabunge waliopokea dodoso kwa ajili ya kuzijaza wanaombwa sana kwa heshima na taadhima kuzirudisha leo au kesho asubuhi kwa kuwa wataalam husika wanaondoka saa 4.00 asubuhi. Mliokuwa na madodoso mnafahamu.

Kama sehemu ya kusheherekea Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Waziri Kapuya anatangaza kwamba timu yao ya Simba imeingia fainali katika Kombe la *Tusker* kwa kuibwaga *Villa* ya Uganda mabao manne kwa mawili kwa njia ya *penalty*. Kwa hiyo, mnaweza kusheherekea hiyo baada ya kazi nzuri iliyofanywa na Waziri wa Ujenzi. *(Makofi)*

Lakini lingine, napenda kusema kwamba tunapokuwa kwenye Kitabu cha Pili *(Supply Vote)*, kwenye mshahara wa Waziri mnaweza kuuliza maswali mengi pale hasa yanayohusiana na utendaji wa Waziri. Ukiuliza kwenye kifungu kingine unamwuliza Mkurugenzi wa Idara, atajibu wapi? Hawezi kufika hapa!

Kwa hiyo, yale maswali mazito yanaingia kwenye Kitabu cha Maendeleo. Nimeona kama Kitabu cha Maendeleo kina maeneo mengi. Kwa hiyo, naomba hii tuelewe kwa sababu tukiondoka kwenye fungu la Waziri kwa kweli tumekubali atajibu lakini sio maeneo yake mnakwenda kwenye *development* inakuwa rahisi zaidi.

Waheshimiwa Wabunge, naahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.26 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatano tarehe 29 Juni, 2005 Saa Tatu Asubuhi)*